ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma

		na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais

16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni

23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe

32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando

53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani

66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni

67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde

68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni

70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi

72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu

73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake

74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Saba - Tarehe 15 Februari, 2018

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Sheria, Utwala Bora na Idara Maalum ya Mwaka 2017/2018. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 36

Migogoro ya Usimamizi wa Mali za Taasisi za Dini

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: (Kny. Mhe. Omar Seif Abeid) - Aliuliza:

Kwa kuwa kumekuwa kukijitokeza migogoro mingi miongoni mwa Taasisi za Kidini jambo ambalo husababisha hadi viongozi wa kidini kupelekana mahkamani kwa kugombania usimamizi wa mali za taasisi hizo au uendeshaji wa taasisi hizo.

(a) Je, ni kwa nini serikali haitungi sheria itakayozuia malalamiko yote yanayohusiana na masuala ya kidini ya kiislam yanayomalizwa na Mufti badala ya kuruhusu kesi hizo kupelekwa mahkamani. Kama ambavyo *FIFA*

imefanya kuzuia kesi zinazohusiana na mpira wa miguu kutopelekwa mahkamani na badala yake kesi hizo ziamuliwe na vyama vya mpira wa miguu katika nchi zao.

(b) Je, serikali haioni kwamba kumpa mamlaka Mufti kumaliza migogoro yote ya waislam ni jambo ambalo litaleta suluhu ambayo hata Mwenyezi Mungu amesema ni jambo zuri kuliko kuwaachia waislam au dini nyengine kugombana mahkamani.

(c) Kwa kipindi cha Januari, 2015 hadi Disemba, 2017 ni kesi ngapi za usimamizi wa mirathi, usimamizi wa mali za misikiti na kadhalika ambazo zimefunguliwa pamoja na kesi za usimamizi wa mali za mayatima.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid, Mwakilishi wa Jimbo la Konde swali lake Nam. 36 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, majukumu makubwa ya Mufti Mkuu wa Zanzibar katika kutatua migogoro ya aina zote ni kufanya suluhu baina ya pande mbili husika. Mufti wa Zanzibar hana mamlaka ya kutoa hukumu katika migogoro kama mamlaka waliyonayo Makadhi, Mahakimu na Majaji. Naomba nimkumbushe Mhe. Mwakilishi kwamba pamoja na kuwepo zuio la kupeleka kesi za mpira mahkamani bado kesi hizo zinafikishwa mahkamani ambapo ndipo pahala pa kutafuta haki.

b) Mhe. Naibu Spika, Mufti Mkuu wa Zanzibar bado anaendelea na majukumu yake ya kuleta suluhu kwenye migogoro yote ya waislam. Lakini itakuwa vigumu kuimaliza migogoro yote

hiyo kwa suluhu kwani wapo ambao hawataridhika na suluhu yake na hivyo watalazimika kutafuta haki yao mahkamani, kwa sababu ndicho chombo kilichopewa mamlaka ya kuamua haki ni ya nani kati ya pande mbili husika.

c) Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi cha Januari, 2015 hadi Disemba, 2017 jumla ya kesi za usimamizi wa mali za misikiti zilizofunguliwa ni 29, na jumla ya kesi za mirathi 260 zimefunguliwa. Nashukuru.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri napenda kumuuliza maswali ya nyongeza yenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Je, hadi sasa kuna migogoro mingapi mahkamani.
b) Nini chanzo cha migogoro hiyo, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Yussuf Hassan Iddi, Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Spika, hadi sasa hivi idadi ya migogoro ambayo iko mahkamani kuna mgogoro mmoja ambao uko Unguja unahusisha msikiti uliokuwa karibu na *Amani Stadium*.

b) Sababu kuu ambazo za msingi zinazosababisha migogoro hii kutokezea, moja ni waumini kugombania uongozi wa msikiti, lakini pia namna ya zile mali ambazo msikiti wenyewe upo. Kwa sababu kuwa kiongozi bila shaka na zile mali za msikiti utasimamia, kwa hivyo mali nazo pia za msikiti zinasababisha vile vile migogoro kutokezea.

Lakini isitoshe mgogoro unaweza ukatokezea katika namna gani ya kuendesha ibada. Kama ninavyoelewa baadhi ya misikiti huwa baada ya sala wanaomba dua, lakini misikiti mingine baada ya sala hawaombi dua. Kwa hivyo, migogoro inaweza ikaibuka katika njia kama hizo. Nashukuru.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa ni asubuhi naomba muungane na mimi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu aliyeumba mbingu na ardhi na vilivyomo vyote.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimsifu waziri kwa majibu yake mazuri lakini na mimi nina swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Kwa kuwa zamani kulikuwa na utaratibu wa misikiti yote kutoa hotuba katika sala za ijumaa ili kuelezea kitu fulani ambacho kitakuwa muafaka kwa nchi yetu na wananchi wetu, lakini hivi sasa tatizo lile limeondoka na kila mmoja anatunga hotuba yake. Je, serikali imejipanga vipi kuhusu suala hili.

b) Huoni kwamba kumuachia kila mtu kutunga hotuba yake inasababisha uchochezi. Kwa nini serikali isingerudisha utaratibu ule ili kuweza kwenda katika mstari ambao tunaendana dini na serikali kwa pamoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) Mhe. Suleiman Sarahan Said, Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake kama ifuatavyo.

a) Mheshimiwa ni kweli utaratibu ulikuwepo kwa muda mrefu wa misikiti yote kupangiwa kutoa hotuba za Ijumaa za aina moja lakini kwa sasa hivi utaratibu huo baadhi ya misikiti

wanakiuka. Nimwambie tu Mhe. Suleiman Sarahan Said kwamba tutaendelea kuhakikisha hotuba zinatolewa kwa misikiti mbali mbali na ni vyema tukawa na hotuba ya aina moja.

b) Lakini nikumbushe Mhe. Sarahan kwamba kutoa hotuba ni kutoa ukumbusho, kwa hivyo ukumbusho unawezekana ukawa wa aina mbili na usiwe wa aina moja. Lakini kubwa zaidi ni kuzingatia namna gani miongozo sahihi ya dini yetu inavyotuongoza.

Kwa hivyo, suala lake tunaendelea kulichukua kuhakikisha kwamba tunaweza kufanya likawa bora zaidi na kuepuka migogoro ambayo ingeweza kuepukika.

Nam. 44

Ujenzi wa Milango ya Maduka Konde Sokoni

Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Kny Mhe. Omar Seif Abeid) - Aliuliza:

Kwa kuwa lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kwamba inawapelekea maendeleo wananchi wake kwa kustawisha hali zao za uchumi ili kuweza kumudu maisha yao. Kwa sababu serikali imetumia fedha nyingi kujenga soko la Konde jambo ambalo ni faraja kubwa sana kwa watu wa Konde. Kwa sababu katika eneo lililojengwa soko hilo kulikuwa na milango ya maduka na mkahawa ambayo baada ya ujenzi havipo tena.

a) Je, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ina mpango gani wa ujenzi wa milango ya maduka na kuwapatia wafanyabiashara waliokuwepo katika eneo hilo ili kuondoa manung’uniko ya kwamba ujenzi wa soko hilo

haukuzingatia uwepo wa wafanyabiashara hao kwa miaka mingi.

b) Je, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni haioni kwamba kukosekana milango ya maduka kwenye soko hilo kutapunguza kwa kiasi kikubwa kupatikana kwa makusanyo ya kodi ya soko hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 44 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia program ya *MIVARF* kwa kutujengea soko la kisasa la kuuzia samaki, nafaka na matunda katika eneo la Konde.

b) Mhe. Naibu Spika, ni kweli katika eneo lililojengwa Soko la Konde kulikuwa na vibanda vilivyokuwa na milango minane ya biashara ya maduka na mkahawa mmoja. Azma ya serikali kupitia program ya *MIVARF* ni kujenga soko kubwa zaidi kuliko lile ambalo limejengwa katika eneo la Konde. Lakini kutokana na ufinyu wa eneo la ujenzi ikalazimika kujengwa soko liliopo hivi sasa ambalo lina vizimba 52 vya kuuzia bidhaa, bucha moja, chumba cha baridi na vyoo 7 ambapo milango ya maduka haikupata nafasi tena. Mara soko hilo litakapokabidhiwa kwa halmashauri na kuanza kazi ya kugawa vizimba hivyo, kipaumbele kitatolewa kwa wale wote waliokuwa wakifanya biashara katika eneo hilo wakiwemo wale waliokuwa na milango ya maduka.

c) Mhe. Naibu Spika, ni kweli uwepo wa milango ya maduka kwenye soko la Konde na maeneo mengine ya mamlaka ya halmashauri kunachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la makusanyo ya halmashauri. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa eneo lililojengwa soko haikuwezekana kuweka maduka na vitu vingine katika soko jipya.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa mji wa Konde unakuwa siku hadi siku. Je, wizara ina mpango gani sasa wa kujenga soko kubwa zaidi la kisasa ili liendane na mji huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikiri kuwa katika Mji wa Konde kumekuwa na mabadiliko ya ongezeko la watu katika maeneo yale kama ambavyo Mheshimiwa anaelezea. Hata hivyo, kwa sasa serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni haijawa na mpango maalum wa kuweza kujenga soko jengine katika maeneo hayo ya Konde na badala yake inaendelea kukamilisha utaratibu. Pale itakapokabidhiwa ikionekana kuna haja ya kufanya hivyo kutokana na Bajeti za Serikali zitakazopatikana na zile juhudi za halmashauri, basi serikali kwa ushauri huo nadhani hatutokuwa na mashaka yoyote tutaweza kufanya kadri hali itakavyokuwa inaruhusu.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunijaalia fursa hii niulize swali la nyongeza. Kwanza

namshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kufika salama naomba pia aniwezeshe nimuulize swali la nyongeza Mhe. Waziri.

Kwa kuwa soko la Konde hivi sasa lina vizimba 52 vya kuuzia bidhaa mbali mbali na kwa uzoefu ninaouona wananchi mara nyingi sana huwa panajengwa sehemu soko lakini baadaye soko lile wakaliacha bure tu bila ya kulitumia. Hata juzi nimeona katika *ZBC* TV wafanyabiashara wa Mtemani Wete wanaondolewa na kupelekwa soko la Wete kulitumia.

Je, wana mikakati gani kulitumia soko la Konde ambalo lilijengwa lina vizimba 52 badala ya kufanya biashara za nje na vizimba vile vikakaa bila ya kutumiwa. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikiri kuwa kumekuwepo na migongano aina kama hiyo ya watu ambao baada ya kujenga masoko yetu mbali mbali hapa nchini kushindwa kutaka kuyatumia kwa visingizio mbali mbali. Hata hivyo, tutachukua juhudi mbali mbali kuhakikisha kwamba kwa soko la Konde na maeneo mengine wafanyabiashara wanaingia katika maeneo yale na kufanya biashara kwa mujibu wa sheria na si vyenginevyo na atakayekaidi basi hatua za kisheria zitachukuliwa kama zinavyostahiki.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa ujenzi wa masoko umeenea katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba lakini badala ya ujenzi huwo wananchi huleta manung'uniko kwa kutaka maeneo yao yaliyojengewa masoko hayo. Je, Wizara yako inampango gani kuwepo hati masoko hayo ili kuondosha manung'uniko hayo likiwemo Soko langu la Pujini ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako namuomba Mhe. Mwakilishi arejee swali lake.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa ujenzi huo wa masoko umeenea katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, lakini baada ya ujenzi huo wananchi huleta manung'uniko kwamba wamechukuliwa maeneo yao na kuanza kuyadai. Je, wizara yako ina mpango gani wa kuwapa hatimiliki masoko hayo ili wananchi kuondoa manung'uniko hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kumejengeka tabia hiyo baada ya masoko mbali mbali kujengwa hapa nchini wananchi kuwa na manung'uniko kadhaa. Lakini uzoefu unaonesha kwamba wananchi hao wamekuwa wakilalamika isivyo halali na kusahau mipango mikubwa ya serikali ambayo imeandaliwa kwa lengo lao au kwa manufaa yao. Hivyo basi, naomba niseme tu kwamba masoko yote ambayo yamejengwa kisheria na wakati wa maandalizi ya ujenzi huo serikali hufanya upembuzi yakinifu katika kuona kwamba masharti pamoja na haki za watu zinazingatiwa. Pale inapolazimika kuonekana kwamba kuna fursa ambayo mwananchi angestahiki kupata basi serikali kupitia

halmashauri zetu tunachukua juhudi mbali mbali za kuona kwamba hatua zinafuata ili kuonekana wananchi wetu wanapata fidia na si vyenginevyo.

Mhe. Naibu Spika, kupitia fursa hii niwaombe tu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba tujitahidi sana katika kuelimisha wananchi wetu katika kuona kwamba mipango hiyo ambayo imetekelezwa, miradi iliyotekelezwa ya serikali haina nia mbaya kuwakomoa wananchi na badala yake ina lengo la kuwasaidia wao ili kujikwamua na kipato, ili kuona kwamba wanafanikisha na kupata fursa mbali mbali za kibiashara na nyenginezo. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 64

Kuimarisha Kilimo cha Minazi

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi katika juhudi zake za kuleta maendeleo ya kielimu Zanzibar pamoja na kuwaboreshea walimu mishahara yao na katika jitihada zake za kukuza kilimo. Pamoja na jitihada hizo bado hutokea baadhi ya watu kutaka kupunguza jitihada hizo ama kwa makusudi au kwa shida za maisha kama katika suala la nazi kupotea Zanzibar kwa kukata minazi na kutokupanda minazi kwa wingi, kuangusha madafu, minazi ya nazi na kuwa biashara kubwa bila kuangalia athari zake na katika kipindi cha miaka ya nyuma ilikuwa si ruhusa kuuza madafu na minazi ya nazi.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kulirejesha zao la nazi kama zamani.

(b) Je, ile sheria ya kukataza kuuza madafu ya minazi bado ipo au ilikuwa hakuna sheria.

(c) Je, bado zao la nazi lina haja ya kurudishwa kama zao la biashara na matumizi bora au halina haja tena.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 64 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Naibu Spika, wizara imedhamiria kuimarisha na kuongeza uzalishaji wa zao la nazi nchini kwa kuanzisha na kutekeleza program maalum ya kuendeleza zao la nazi yenye shabaha zifuatazo:

i. Kuimarisha utafiti, upatikanaji wa mbegu bora na kuendeleza vitalu ili kuotesha miche bora;
ii. Kutoa elimu kwa wakulima juu ya mbinu bora za kilimo cha nazi pamoja na kujikinga na wadudu waharibifu;
iii. Kurejesha hadhi ya zao la nazi kwa kushirikisha wakulima kusarifu na kuongeza thamani bidhaa zinazotokana na nazi;
iv. Kuimarisha doria na kuhamasisha jamii kuepuka ukataji wa minazi kiholela;
v. Kudhibiti matumizi ya mbao za minazi.

(b) Mhe. Naibu Spika, sheria ya kukataza kuuza madafu ya nazi bado ipo kama ilivyopitishwa katika Sheria Mama ijulikanayo *The Protection of Fruits* ya mwaka 1964 na kufanyiwa mapitio mwaka 1965 na mwaka 1966. Sheria hii inaelekeza kuwa mtu yeyote atakayepatikana na matunda machanga isipokuwa embe shomari atakuwa ni mkosa kisheria.

Aidha, sheria imetamka kuwa Jeshi la Polisi ndio lenye jukumu la kumkamata mhusika wa kosa hilo na kumpeleka kwenye vyombo vya kisheria.

(c) Mhe. Naibu Spika, zao la nazi ni moja kati ya mazao ya biashara hapa Zanzibar na ni miongoni mwa mazao makuu yanayopatikana katika masoko yetu, ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, nimshukuru Waziri kwa mambo mengi aliyoniandikia humu mpaka sheria ambazo zilitungwa nilikuwa sizifahamu, kwa hivyo nimpongeze sana. Nataka nimuulize Waziri katika swali moja lenye kifungu (a) na (b).

a) Kwa kuwa amesema sasa hivi ana mpango wa makusudi wa kuendeleza minazi katika mbegu bora. Nataka kumuuliza Mhe. Waziri tulikuwa tuna minazi ambayo inatimia miaka kuanzia 100 mpaka kuendelea mbele na tuna minazi ya muda mfupi. Je, katika mbegu ambazo atatuletea ni mbegu gani ambazo ameziona ni bora, zitakuwa zile za miaka ile iliyopita au mbegu bora ambayo inazaa haraka na inakufa haraka.

b) Nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba katika masuala ambayo sasa hivi yamejitokeza kuna embe ambazo hazijakomaa zinaangushwa kwa kasi sana kwa ajili ya kutengenezea *juice*. Hali hii imepelekea Kisiwa cha Pemba asilimia 80 ya miembe sasa hivi yote imeingia mafunza na ukiisubiri iive ndio haipatikani tena na ndio watu wanaziangusha changa ili kupata angalau fidia. Waziri amejipanga vipi kurudisha hali halisi ya kuondoa mafunza hawa katika miembe iliyokuwepo Pemba.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza namshukuru sana

Mhe. Mwakilishi kwa maswali yake mawili naomba kumjibu kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, minazi hasa ambayo tumeizowea hapa Zanzibar ni minazi ya *east if control* na ndiyo minazi ambayo inahimili na inaishi vizuri hapa kwetu. Watafiti walifanya utafiti wakagundua kama kuna mbegu nyengine ambazo ni za muda mfupi zinachukua kama muda wa miaka 15 basi, ikifika miaka 15 haiendelei tena kuzaa, hata mimi nimeipanda mingi hiyo. Baada ya muda mfupi tu, kwanza haistahili hata maradhi.

Tafiti zilizofanyika sasa hivi tumeona na vizuri tuka-*cross breed* ile *east if control* na ile *high breed* tunaweza tukapata *product* ambazo ni nzuri sana. Ndiyo utafiti ambao tunafanya pale Chuoni sasa hivi tumeona hiyo inaweza kusaidia sana tuka-*mix* ile *east if control.* Kwa sababu ile inachukua muda mrefu sana kuzaa, hii mengine inachukua muda mfupi sana kuzaa, uki-*cross* unaweza ukapata mbegu nyengine nzuri zaidi hiyo *study* tunaifanya.

Hivi karibuni tumepata bahati nzuri kuna mkulima mmoja mzuri sana hapa alikuwa kiongozi, Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais amekwenda India akakuta kule *Goa* kuna mkulima wa mnazi mzuri sana na ameandika kitabu kizuri sana juu ya zao la nazi. Tunategemea sasa hivi kuwapeleka wataalamu wetu huko wakajifunze ukulima bora wa nazi ambao na sisi turudishe zao hili la nazi katika kiwango chake.

Lakini tatu kama mlifuatilia karibuni Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein alizungumza na Balozi wa Indonesia na yeye vile vile aliahidi kwamba ataweza kutupatia taaluma ya namna gani ya kuweza kulima nazi vizuri. Kwa hivyo, tuna program hizo za kufanya kuona tunapata *product* ya nazi ambayo itakuwa endelevu.

Cha msingi hapa kulima ni jambo moja na kutunza ni jambo la pili. Kwa bahati mbaya sana tumekuwa na ukataji mkubwa sana wa minazi kiasi ya kwamba huoni hata ile kazi inayofanywa ya kupanda minazi kwa sababu kasi ya kukata imekuwa ni kubwa sana. Mtu mmoja anakata minazi 20, 40 kama mchezo kwa kutumia misumeno ya moto.

Pili, kuna uvunaji mkubwa sana wa madafu kwa mujibu yanavyovunwa sasa hivi huwezi ukaona kiwango cha nazi kinapanda, ndiyo maana sasa nazi imefikia kiwango cha sh. 1,500 kwa nazi moja kwa sababu watu wanakata minazi kwa kasi lakini na uvunaji wa madafu nao umekuwa wa kasi. Madafu yanayotakiwa kuvunwa ni yale ya kitamli, lakini sasa hivi tumeamua kuvuna madafu ya kawaida kiasi ya kwamba nazi kama nazi haipatikani katika mji wetu hivi sasa. Kwa upande wa serikali tumejipanga na tunataka kuzitumia halmashauri zetu sasa zianzishe vitalu vya minazi kule chini ili kila shehia angalau iwe na shamba la minazi linalotambulikana ili kurudisha hadhi ya zao letu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu wadudu waharibifu ni kweli mazao yetu mengi yanapata matatizo juu ya wadudu waharibifu. Hivi karibuni tulikwenda China mimi na Waziri wa Fedha tukagundua kwamba kuna dawa ambazo zinasaidia sana kutibu haya matatizo ya wadudu wa mazao. Tunategemea baada ya …… China yatakapomalizika, jana nimepata ujumbe kwamba Waziri wa Kilimo anakuja tena na timu yake, moja katika jambo ambalo tulilizungumza ni kutusaidia katika kupambana na wadudu waharibifu hasa wa embe, nazi na kadhalika, hili tunalichukulia hatua katika kulitekeleza. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Nassor Jazira: Ahsante Mhe. Naibu Spika na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini katika majibu yake amesema kwamba wamefanya

doria kuhamasisha jamii kuepuka ukataji wa minazi kiholela, vile vile kudhibiti matumizi ya mbao za minazi.

a) Je, wizara imefanya tafiti gani kwa kila mwaka minazi mingapi inakatwa.

b) Ni athari gani ambazo zinapatikana baada ya kukatwa miti hiyo na kutumia mbao za minazi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa sina takwimu sahihi za minazi mingapi inakatwa lakini nasema kiwango cha ukataji wa minazi ni kikubwa sana. Moja ambalo tumeligundua tumepita kwenye viwanda ambavyo vinakata mbao za minazi. Nyuma walikuwa wanadai kwamba minazi inapokuwa mikongwe ndiyo wanayoikata lakini tumegundua kwamba sio kweli. Kila anayetaka kujenga nyumba kwa mfano sasa hivi anakata minazi maana yake nalo ni tatizo la pili. Kuna watu wanachukua viwanja wanakata minazi, kuna watu waliopewa eka za kulima wamegeuza kuwa ni viwanja wanakata minazi na miti mingine, *rate* ya kukata ni kubwa lakini tutaitafuta hesabu na *search* kidogo siwezi kusema kiasi gani lakini nasema kiwango ni kikubwa.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka tulikuwa tuna minazi kama milioni tatu na laki tano, sasa hivi nina hakika haiwezi kufika milioni mbili laki tano tena. Kwa hivyo, *rate* ya kukata ambayo ni kubwa, lakini sasa hivi tutaitafuta hesabu, siwezi kusema kama tutatoa kesho na kesho kutwa itabidi tupite, tuangalie na tufanye utafiti wa kutosha yale tuliyokuwa nayo mwaka juzi na sasa hivi iliyobaki ni kiasi gani. Halafu tutaleta hiyo taarifa pengine wakati wa Kikao cha Bajeti itakuwa ni wakati muafaka kuleta hii hesabu, sio hesabu ambayo unayoweza kuipata kwa haraka sana.

La pili, alichosema kwamba viwanda vya mbao vya mnazi ni kweli kama ukipita kwenye viwanda hivi vinavyotengeneza

furnitures inasikitisha sana kuona idadi ya mbao zinazofanyishwa kutokana na minazi, imekuwa ni biashara kubwa sana. Sisi tumejitahidi sana kufanya doria na kuhakikisha kabisa watu wanaacha kukata minazi, lakini bado hatujaweza kudhibiti suala hili. Lazima nikiri kabisa hatujaweza kulidhibiti kwa sababu kwanza ni sehemu.Vingi, vingi Zanzibar, tukizungumzia viwanda, viwanda vingi ni vya mbao, viwanda vidogo vidogo ndivyo viwanda vinavyotoa ajira kubwa sana.

Tunalo tatizo hili la msingi na ni lazima nikiri tu kwamba tumejitahidi kukaa viongozi pamoja kutafuta njia ya kuweza kulitatua kwa pamoja. Sisi wenyewe binafsi hatuna *solution* ya peke yetu lazima tukae pamoja na viongozi tuone ni njia gani tuweze kulitatua.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii asubuhi hii. Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ya suala hili. Lakini katika majibu yake amesema kwamba kuna sheria ya embe shomari kuweza kuchumwa zikiwa mbichi. Embe shomari ni embe zinazolimwa Mchangani shamba na ni maarufu zinazowaingizia watu wa Mchangani kipato kikubwa.

Je, Mhe. Waziri haoni sheria hii ya kuweza kuchumwa embe hizi zikiwa mbichi imepitwa na wakati kwa sababu embe hizi zinawaingizia watu wa Mchangani kipato kikubwa zikiwa mbivu na ni embe bora kuliko embe zote za duniani.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nasema sheria imepitishwa na kama kuna haja kuzi-*renew* sheria tutaifanyia. Ila utafiti kwamba embe shomari ndiyo embe bora kunahitaji kufanyiwa utafiti kwa sababu wanunuzi wengi sana wanapenda embe ambazo hazina nyuzi, zile embe ambazo zina nyuzi hazipendwi sana, hata ukenda kwenye masoko yote duniani unakuta embe ambazo zina nyuzi

hazipendwi na embe shomari zina nyuzi. Sasa sina hakika kama ni embe bora. Embe bora ni zile ambazo hazina nyuzi kwa mfano embe Muyuni haina nyuzi, marugo kule Pemba tunaita embe siagi haina nyuzi. Hizi ni embe ambazo zinatakiwa sana na mimi ningewashauri sana wananchi tulime sana embe ambazo zina soko la ndani na zina soko la nje, hizi ni embe ambazo zinasaidia sana katika soko la ndani na soko la nje. Lakini tusiache kulima embe shomari kwa sababu inasaidia watoto. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea.

Nam. 25

Upatikanaji wa Vifaa katika Bandari ya Mkoani

Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Aliuliza**:**

Kwa kuwa bandari ya Mkoani ni miongoni mwa bandari za Kimataifa na bandari hiyo kwa hivi sasa inakabiliwa na changamoto mbali mbali za upungufu mkubwa wa vifaa.

a) Je, ni lini bandari hii itapatiwa vifaa vya kisasa vinavyokwenda sambamba na vigezo vya bandari ya Kimataifa kama kreni na *fork lift* ya kushushia mizigo.

b) Je, kutoifanyia matengenezo makubwa bandari hii na kuipatia vifaa vya kisasa, si kuikosesha mapato serikali.

c) Je, Mhe. Waziri unaliahidi nini Baraza hili kuhusu upatikanaji wa vifaa hivyo ukizingatia kuwa Bandari hii ni ya pekee kwa umuhimu wake kwa usafirishaji wa abiria na mizigo kwa Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Shirika la Bandari imeanzisha mradi endelevu wa uimarishaji wa vifaa vya kufanyia kazi katika Bandari za Unguja na Pemba. Mradi huu ambao ulioanza tangu mwaka 2015/16 una lengo la kuzipatia vifaa vya kisasa Bandari za Malindi na Mkoani. Katika mwaka wa fedha 2015/16 Shirika lilifanikiwa kununua vifaa mbali mbali vya kufanyia kazi bandarini ikiwemo kreni 2, *terminal tractor 2, trailer 2, reach stacker 1* na kadhalika. Kati ya kreni zilizonunuliwa kreni moja ya tani 25 ilipelekwa katika Bandari ya Mkoani na inafanya kazi vizuri hivi sasa. Ndani ya mwaka huu wa Bajeti 2017/18 Shirika linakamilisha utaratibu wa manunuzi ya vifaa vyengine vipya ambapo Bandari ya Mkoani itapatiwa *terminal tractor* moja na *trailer* moja pamoja na *fork lift* moja ya tani 3.

b) Mhe. Naibu Spika, Shirika la Bandari katika mwaka 2016/2017 limefanikiwa kutengeneza eneo la kuwekea mizigo ya makontena katika Bandari ya Mkoani lenye uwezo wa kuhifadhi kiasi cha makontena 250 kwa wakati mmoja pamoja na kujenga ukuta wa uzio katika bandari. Mwaka huu wa fedha 2017/18 Shirika limepanga kulifanyia matengenezo makubwa ghala la kuhifadhia mizigo hapo bandarini.

c) Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu itaendelea kuimarisha Bandari ya Mkoani kwa kuipatia vifaa zaidi vinavyohitajika kila hali ya kifedha itakaporuhusu.

`

Moh'd Mgaza Jecha: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, mimi nina swali moja la kumuuliza Mhe. Waziri. Kwa vile bandari ya Mkoani imekuwa ikitangaziwa kwa muda mrefu kama ni bandari ya Kimataifa. Ni lini wafanyabiashara wa Mkoani watapata maslahi kwa ajili ya kuteremsha mizigo yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda tena kuchukua nafasi hii kumjibu Mheshimiwa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, hata hivi sasa wafanyabiashara wa Mkoani wanaendelea kupata maslahi yao na sisi tutaendelea kuhakikisha kwamba kila siku zinapoenda basi wataendelea kupata maslahi yao kwa ajili ya kufanikisha shughuli zao za kiuchumi na vile vile kuchangia katika pato la Taifa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

a) Kwa kuwa mlango mkubwa wa uingizaji bidhaa Bandarini ni Shirika la Bandari, na kwa hakika Wizara pamoja na Shirika kwa kipindi cha miaka 10 linafanya vizuri katika kuhudumia uchumi wetu. Hivi karibuni kumejitokeza deni la millioni elfu moja kwa lugha ya kifedha ni bilioni moja ambalo limeathiri bajeti ya Shirika la Bandari na hasa uchumi kwa namna fulani. Je, deni lile la minara Wizara imejiandaaje kimikakati ili liweze kulipwa.

b) Je, kuna kanuni au sheria au mwongozo uliorithiwa wa deni lile au tozo iwe inaendelea kulipwa mpaka maisha. Kama hakuna mkakati gani umewekwa wa kuweka kanuni na mwongozo ambao utarahisisha *frequently* tulipwe kila

baada ya miezi mitatu *three hundred million* kama tulivyosikia.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil maswali yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kuipongeza Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kuhakikisha kwamba deni ambalo amelisema Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil linafanyiwa kazi ili kuhakikisha kwamba linatatuliwa. Hivi sasa napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja Wizara zetu zote mbili, yaani Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa SMT na Wizara yetu ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji tumefanikiwa kulitatua tatizo hili. Hivi karibuni Mhe. Waziri husika wa Wizara amemwandikia Katibu Mkuu wake na Katibu Mkuu tayari ameshamwandikia Mkurugenzi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania kuhakikisha deni hili linalipwa. Ninawahakikishia wananchi kwamba deni hilo ni bilioni tatu hivi sasa wastani wake na litalipwa karibuni.

Kuhusu mkakati sisi tunajipanga kama nilivyosema mwanzo kwamba ilikuwa ni makubaliano kwa nia njema ya kuimarisha Muungano wetu. Sasa hivi tunajipanga kimkakati kuhakikisha kwamba hili suala linakuwa katika kisheria zaidi na kikanuni. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali dogo la nyongeza. Mhe. Waziri Mji Mkuu wa Pemba ni Chake Chake na Chake Chake ipo karibu na Wesha na wafanyabiashara wote karibu nusu ya Pemba wapo Chake Chake.

a) Je, wizara yako ina mpango gani wa kuongeza kina cha maji katika bandari ya Wesha ili kuhakikisha zile meli zinazoleta mizigo kama saruji na mizigo mingine kufunga gati Wesha ili kuondosha usumbufu kule Mkoani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Bandari ya Wesha ni bandari muhimu sana hasa katika kusafirisha mizigo kutoka Pemba kwenda Tanga na sehemu nyengine. Sisi tutaendelea na jitihada za kuhakikisha kwamba bandari ile tunaifanyia matengenezo na vile vile kina cha maji kile kinaongezwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba majahazi yanayokwenda yafunge gati wakati wowote bila ya tatizo lolote.

Nam. 50

Uimarishwaji wa Miundombinu Wakati wa Ujenzi wa Barabara

Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Kny: Mhe. Omar Seif Abeid) - Aliuliza:

Kwa kuwa serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji inategemea kujenga barabara kongwe ya Wete - Chake Chake ambapo kwa sasa serikali iko mbioni kulipa fidia ya mazao na vitu vyengine ikiwemo uhamishaji na uzikwaji wa

mkonga wa mawasiliano uliozikwa ardhini ambapo serikali inawajibika kulipa gharama hizo kabla ya ujenzi huo kuanza. Kwa kuwa kuna kazi ya uzikaji wa mkonga kama huo unaozikwa ardhini kwenye barabara ya Kilindini - Micheweni na barabara ya Mkoani ambapo unazikwa kutoka mita mbili na nusu hadi tatu pembezoni mwa barabara.

a) Je, serikali haioni kwamba kuzika mkonga huo kando kando karibu sana na barabara ni tatizo ambalo litaigharimu serikali kwa mara ya pili kwa ajili ya uhamishaji na uzikwaji wa mkonga huo pindipo barabara hiyo itakapohitaji kutanuliwa tena.

b) Je, wizara husika ina mpango gani wa kukaa pamoja na taasisi nyengine ili kuhakikisha kwamba matatizo ya uharibifu wa miundo mbinu ya mawasiliano, umeme na maji hayatoathirika wakati wa ujenzi wa barabara hizo kama ilivyotokea kwa barabara ya Mwanakwerekwe - Fuoni.

c) Je, wataalam wetu wana mpango gani wa kulisimamia jambo hili ili kuepuka kuitia serikali gharama za mara kwa mara pale inapotokea kuhamisha miundo mbinu wakati wa ujenzi wa barabara zetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, mkonga wa mawasiliano ni miundo mbinu ya mawasiliano kama ilivyo miundo mbinu ya umeme ikiwa na lengo la kutoa huduma za mawasiliano kwa Mashirika,

Makampuni ya Simu, Taasisi za Serikali na watu binafsi, hivyo miundo mbinu hiyo hupitishwa pembezoni mwa barabara ili kuwafikia walengwa na kwa usalama wake zaidi.

Kwa kuzingatia viwango vya kimataifa mkonga hupitishwa kwenye hifadhi za barabara yaani *road reserve* kwa kujengwa njia za kupitisha nyaya za mkonga na mengineyo yaani *utility corridor,* tatizo kubwa linalojitokeza kwetu sisi ni nyumba kujengwa ndani ya hifadhi ya barabara na kupelekea ugumu wakati wa kupitisha miundombinu hii ya mawasiliano.

b) Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mawasiliano imetoa mafunzo maalum ndani ya taasisi na idara zake, vipindi maalum vya redio na televisheni vimekuwa vikiendeshwa kuelimisha wanajamii umuhimu wa mkonga na juhudi zinazohitajika katika kuuhifadhi na kuutunza kwa maendeleo ya taifa letu kiujumla.

   Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mawasiliano imekutana mara kadhaa na Mamlaka ya Maji ambao ndio waendeshaji wakubwa wa miradi ya maji inayowekwa sambamba na njia za mkonga ili kushirikiana katika kuihifadhi miundombinu hii.

c) Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha gharama za mara kwa mara hazijitokezi, Idara ya Mawasiliano inasimamia kuhakikisha mkonga wowote unalazwa katika bomba na katika viwango vya kimataifa. Aidha, katika barabara ya Mwanakwerekwe - Fuoni mkonga umelazwa katikati ya barabara ili kuepusha uharibifu unaoweza kujitokeza mara kwa mara.

   Pia idara inatoa ushauri wa kutosha kwa waandaaji wa ujenzi wa barabara kuhakikisha wanaweka njia za kupitisha miundombinu ya mawasiliano kabisa *(utility corridor)* wakati

wa uandaaji wa ujenzi wa barabara husika. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kumuuliza swali moja la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Je, wizara imejipanga vipi kuhakikisha kwamba inawasimamia wajenzi wa barabara Unguja na Pemba wanaweka kabisa njia za kupitishia miundombinu ya mawasiliano *(utility corridor).*

b) Ni kiasi gani cha fedha kilichotumika kurejesha mkonga wa taifa ulioharibika katika ujenzi wa barabara ya Mwanakwerekwe - Fuoni.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Yussuf Hassan Iddi, Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Fuoni swali lake lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Wizara yetu siku zote imekuwa ikihakikisha kwamba kwa sababu wote hao ni wahusika ambao wako katika wizara yetu, UUB wako wizarani na Idara ya Mawasiliano iko wizarani, tunahakikisha kwamba wanaofanya kazi hizo wanashirikiana. Mfano mzuri tulipokuwa tunapitisha mkonga huu kwa ajili ya vituo vyetu vile vya *E-Health* pale Mkoani kulitokea tatizo hilo lakini baada ya kukaa pamoja hilo tatizo lilitatuka na tumewahimiza kwamba lazima wakati wanapotaka kupitisha miundombinu hii wakae pamoja.

b) Kuhusu gharama ambazo zimetumika katika kuhakikisha kwamba ule mkonga wetu tunaurejesha tena pale, gharama ya mafundi ilikuwa zaidi ya millioni themanini na nne

lakini gharama nyengine hizi zinakuwa sio kubwa sana kwa hiyo takriban wastani millioni tisini zimetumika katika kurejesha mkonga katika sehemu ya Mwanakwerekwe - Fuoni wakati wa ujenzi wa barabara. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ujenzi wa barabara ya Wete - Chake Chake umekuwa ukizungumzwa kwa muda mrefu hivi sasa.

a) Je, ni lini au ni mwezi gani ujenzi huo utaanza.
b) Na ni kampuni gani itakayojenga barabara hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa, Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Kiwani swali lake lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Barabara ya Wete na Chake Chake ni miongoni mwa barabara tatu ambazo zilikuwa zikijengwa na mkandarasi mzalendo yaani *MECCO*, barabara ya kutoka Wete - Konde tayari imeshamalizika kujengwa, barabara ya Wete - Gando tayari imeshamalizika kujengwa na barabara hii tupo katika hatua za mwisho katika kuhakikisha kwamba inajengwa na hivi sasa tunajitayarisha.

b) Kwa ajili hiyo, mimi napenda kumtoa wasiwasi kwamba mkandarasi yule yule aliyejenga barabara zile mbili za mwanzo ndio atamaliza kujenga barabara hii ya pili. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Swali la mwisho la nyongeza Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Machano Othman Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniruhusu kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, katika mpango wa serikali wa ujenzi wa barabara mradi wa barabara ya kaskazini ulikuwa unaitwa barabara Kinazini - Mjini hadi Mkokotoni kaskazini. Habari tulizonazo ni kwamba mradi ule sasa utaanza Kwanyanya kuelekea Mkokotoni.

a) Je, kama ni kweli sababu zipi zilizopelekea mradi huu kurushwa kutoka Kinazini hadi Kwanyanya wakati barabara kuanzia Maruhubi hadi Kwanyanya ni mbovu na haipitiki kwa hali yoyote.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Machano Othman Said, Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Mfenesini swali lake kama ifuatavyo:

Ni kweli barabara ile imeanzia kwa mujibu wa ule mkataba wetu kuanzia Kwanyanya pale mpaka kufikia Mkokotoni. Kwa mujibu wa *master plan* iliyokuwepo barabara kutoka mjini mpaka Bububu imekusudiwa kuwa ipite barabara mbili. Kwa hiyo, ili barabara mbili zipite zitatakiwa gharama kubwa sana. Lakini kutokana na kwamba barabara hii ina umuhimu wake sana kwa Mkoa wa Kaskazini na vile vile yapo madaraja ambayo yana gharama katika kuyajenga, kwa hiyo tumeamua tuanze kule na huku kipande kilichobakia wizara itachukua hatua kuhakikisha kwamba inafanyiwa ujenzi huo. Tumejipanga kwa hilo na hivi sasa tunatia viraka kwa ajili ya kuhakikisha kwamba ile dhiki ambayo wanaipata wananchi wakati wa kutumia barabara ile inaondoka, lakini tuko katika mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba ile barabara tunaijenga kwa kiwango cha lami na baadae kutiwa taa kama alivyosema Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango

kutokana na msaada kutoka China. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika*:* Waheshimiwa Wajumbe muda wetu wa maswali na majibu umemalizika lakini kabla ya kuendelea naomba nikutangazieni wageni wetu waliofika hapa leo ambao ni wageni wa Mhe. Hidaya Ali Makame, Mwakilishi wa Viti Maalum. Ni wageni wasanii kutoka katika kikundi cha sanaa cha ngoma ya Mchikicho kutoka Nungwi na vile vile ni wahakiki wa ngoma ya Mkurungu. Wageni wenyewe ni hawa wafuatao:

1. Ndg. Juma Haji Ame - Katibu wa Kikundi cha Mchikicho
2. Ndg. Kheri Ali Kikoti - Manju wa Kikundi
3. Ndg. Haji Ame Haji Vuai - Mpiga ngoma kubwa
4. Ndg. Hadiya Ibrahim Hakim - Mchezaji
5. Ndg. Siti Haji Haji - Mchezaji
6. Ndg. Miza Ame Nahoda - Mlezi wa Kikundi

Karibuni sana.

Wageni wetu wengine ni wageni Mhe. Shamata Shaame Khamis, Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Wageni wenyewe ni hawa wafuatao:

1. Ndg. Makame Pandu Mgana - Diwani wa Pangawe
2. Ndg. Thuwaiba Jeni Pandu - Diwani wa Kuteuliwa
3. Ndg. Amina Hassan Ameir - Diwani wa Kipungani

4. Ndg. Halima Salum Abdalla Mambosasa - Diwani wa
5. Ndg. Safia Ali Khamis Kuteuliwa - Diwani wa
6. Ndg. Iddi Salum Mwakilambe Mwembemajogoo - Diwani wa

Karibuni sana.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Mwaka 2017/2018

Mhe. Naibu Spika: Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum.

Mhe. Machano Othman Said: (Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum)

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi kama ilivyo.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa minong'ono ipungue tuelewane. Mheshimiwa anatoa ripoti minong'ono ipunguzwe, endelea mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii adhimu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi pamoja na vilivyomo ndani yake, kwa kutujaalia neema ya uhai na uzima katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku kwa hali ya amani na utulivu.

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha muhtasari wa Ripoti ya Kamati yetu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum, ripoti ambayo inaonesha shughuli zetu zote ambazo tumezitekeleza katika kipindi kilichopita.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 pamoja na kanuni ya 106 (1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, toleo la mwaka 2016. Majukumu ya Kamati yameainishwa katika jadweli la kwanza la kanuni hizo za mwaka 2016.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii muhimu kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao makubwa ambayo yameiwezesha kamati yetu kufanya kazi zake kwa ufanisi na uzoefu mkubwa. Wajumbe wenyewe ni hawa wafuatao:

Nam.	**Jina**	**Wadhifa**
1.	Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf	Mjumbe
4.	Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	Mjumbe
5.	Mhe. Ali Khamis Bakar	Mjumbe
6.	Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
7.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
8.	Ndg. Ali Alawy Ali	Katibu
9.	Ndg. Haji Jecha Salim	Katibu

Mhe. Naibu Spika, utaratibu uliowekwa katika utekelezaji wa kazi za Kamati kwa muda wote uliopita, kamati yetu ilipanga kufuatilia utekelezaji wa malengo na majukumu ya wizara zifuatazo:

(i) Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na
(ii) Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita (6) katika utaratibu iliojipangia ambapo kwa upande wa Unguja ilitumia muda wa wiki nne (4) na kisiwa cha Pemba muda wa wiki mbili (2). Muda huo ulikuwa mdogo sana kutokana na ukubwa wa idara na taasisi zilizo chini ya wizara zinazosimamiwa na kamati hii.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake za kuleta maendeleo na kuimarisha uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu imepata faraja sana kwa uamuzi wa serikali wa kuanzisha mradi maalum wa ujenzi wa mahanga ya askari wa vikosi vyetu, mradi huu ambao tayari umeshaanza kwa vikosi vya KMKM na Mafunzo huko kisiwani Pemba. Pia, tunaamini kwamba chini ya uongzi bora wa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kasi ya uendelezaji wa mradi huo itaendelea.

Mhe. Naibu Spika, aidha, kwa ujumla kamati imeridhika na uingizwaji wa fedha za matumizi mengineyo yaani *(OC)* kwa wizara zote mbili tunazozisimamia. Kwa ujumla taasisi nyingi za

wizara hizi zimepata mgao kati ya asilimia 85 – 100, hivyo kuzifanya ziweze kutekeleza vizuri majukumu yao vizuri.

Mhe. Naibu Spika, aidha, kamati inawapongeza na kuwashukuru sana viongozi wa wizara hizo wakiongozwa na Mawaziri wao, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu, Makamishna na Makamanda wa Idara Maalum za SMZ, Wakurugenzi, Maafisa Wadhamini na watumishi wote kwa ushirikiano wao mkubwa waliotupatia katika kufanikisha majukumu yetu. Mheshimiwa licha ya kuwepo kwa changamoto mbali mbali zinazowakabili na kufanyakazi katika mazingira magumu na yenye upungufu wa nyenzo lakini wameweza kutekeleza majukumu yao ya kazi kadri hali ilivyokuwa inaruhusu na hivyo kufikia malengo waliyojipangia kwa asilimia kubwa na ya kuridhisha.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa uniruhusu nieleze kwa ufupi baadhi ya mambo yaliyojitokeza katika kazi za kamati kwa wizara kama ifuatavyo:

Naanza na Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inazo idara na taasisi mbalimbali ambazo zinafanya kazi kwa mujibu wa malengo yaliyopangwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 chini ya wizara hii. Hivyo, katika kukamilisha majukumu ya kamati yetu tulifanikiwa kuzitembelea idara na taasisi kadhaa ambazo zimeundwa chini ya wizara hii na kujionea shughuli zao mbalimbali ambazo zinaleta tija na ufanisi wake umeimarika kwa misingi ya utawala bora.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum katika ziara zake imebaini kuwepo kwa changamoto kubwa ya vyombo vya usafiri katika idara na taasisi mbalimbali zilizo chini ya wizara hii, jambo ambalo linarudisha nyuma juhudi

zao katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Aidha, changamoto hii inaikabili zaidi Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa ambapo hadi sasa wana gari moja tu na kutokana na upungufu au uhaba huo wameona wanunue vespa moja, wakati Tume ya Utumishi Serikalini haina hata gari moja la kuwasaidia katika shughuli zao, hivyo huenda katika majukumu yao ya kazi kwa kutumia usafiri wa daladala jambo ambalo ni kikwazo kikubwa katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Naibu Spika, kamati katika kazi zake za kawaida ilifanikiwa kutembelea na kupokea taarifa ya Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa kwa upande wa Unguja na Pemba na kujionea utekelezaji wa majukumu yao ambapo mafanikio makubwa yamepatikana licha ya changamoto mbalimbali ambazo zinawakabili. Kamati inaishauri serikali kuchukua juhudi za makusudi katika kuboresha idara hii kwa kuwapatia vyombo vya usafiri pamoja na kuimarisha kikamilifu ujenzi wa kituo kipya cha kuhifadhia nyaraka na kumbumbu huko Koani.
Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba imejitahidi sana katika kusimamia na kutekeleza majukumu yao na kuhakikisha wanakwenda sambamba na malengo ya wizara na serikali katika utekelezaji wake wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ujumla. Kamati imebaini kuwepo kwa baadhi ya idara kisiwani Pemba ambazo utekelezaji wa majukumu yake unapaswa kuangaliwa kwa ukaribu na kwa lengo la kujenga misingi ya haki na uadilifu kwa watumishi wa umma.

Mhe. Naibu Spika, hivyo, Kamati inaagiza uongozi wa Ofisi Kuu Pemba kuhakikisha inasimamia vya kutosha watumishi wa serikali ili kujenga maadili bora ya utumishi wa umma. Vile vile inaagiza watendaji wa taasisi zinazohusika moja kwa moja katika utatuzi wa migogoro ya kijamii kuweza kufuatilia na kuchukua hatua mara tu tatizo linapotokezea na waache tabia ya kukaa ofisini kusubiri wananchi kuwasilisha matatizo yao.

Mhe. Naibu Spika, katika kufikia malengo ya serikali na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kuona kwamba idara na taasisi zake zinafanikiwa katika utekelezaji wa majukumu yao na kuleta ufanisi katika kukuza maendeleo ya nchi yetu, kamati imegundua kuwepo kwa changamoto kubwa ya uchakavu wa majengo kwa upande wa mahkama zote Unguja na Pemba, isipokuwa Mahkama ya Mwanakwerekwe ambayo imefanyiwa ukarabati mkubwa na mzuri hivi karibuni.

Mhe. Naibu Spika, hali ya Mahkama ya Wete kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba hairidhishi hata kidogo kwa watendaji na watumiaji wote wa Mahkama hii.

Mhe. Naibu Spika, vile vile wizara hii inakabiliwa na changamoto ya vitendea kazi kwa kiasi kikubwa kutokana na idadi kubwa ya idara pamoja na taasisi mbalimbali zinazotegemea ruzuku kutoka Ofisi Kuu. Tatizo hili linaonekana kushamiri zaidi katika Taasisi ya *ZAECA*, Idara ya Nyaraka, Tume ya Utumishi Serikalini, Ofisi ya Mufti na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Taasisi hizi ambazo zina jukumu zito la kulinda na kusimamia rasilimali za taifa ili zisipotee kwa watu wabadhirifu na watu wasiokuwa na imani na maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa taasisi ambazo zinapokea ruzuku kutoka ofisi kuu ni Ofisi ya Mufti Zanzibar ambayo kihistoria ofisi hii ipo kwa muda mrefu sasa na kila mmoja anafahamu umuhimu wa taasisi hii hapa Zanzibar. Aidha, katika kujiendesha kikamilifu na kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa walengwa wa taasisi hii, kamati inaishauri Ofisi ya Mufti kupatiwa fungu lake la bajeti ili liweze kuwasaidia kutatua changamoto mbali mbali zinazowakabili.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaishauri Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kufanya juhudi za makusudi katika Ofisi ya Mufti na kuhakikisha kuwa wanapatiwa jenereta

kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la nishati ya umeme katika ofisi yao. Hata hivyo, licha ya changamoto hizo kunahitaji ufumbuzi, kamati inaishauri Ofisi ya Mufti Zanzibar kufuatilia kiundani mara kwa mara utendaji wa Ofisi ya Mufti Pemba na kuhakikisha kwamba wanaboresha utendaji wao katika majukumu yao ya msingi ambayo yanaihusisha jamii ya waislam. Aidha, kamati haikuridhishwa na utendaji na uwajibikaji wa maafisa wa Ofisi ya Mufti, Kisiwani Pemba.

Mhe. Naibu Spika, ili kuboresha na kufikia katika utawala bora wa haki na sheria kwa taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kamati inaishauri serikali kuzitaka wizara au taasisi zake zote kutoa mashirikiano ya karibu pamoja na kutaka ushauri wa kisheria katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hasa wakati wizara au taasisi hizo zinapopokea indhari ya kutaka kushtakiwa na zile ambazo zimepatikana mahkamani na pale zinapotaka kuingia katika mikataba au makubaliano, kwani uzoefu unaonesha kuwa serikali hushindwa mahkamani katika hatua za awali.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kamati inaishauri serikali katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, kuandaa na kuwasilisha Baraza la Wawakilishi Zanzibar mpango maalum wa Miswada ya Sheria inayotarajiwa kuwasilishwa katika mwaka huo wa fedha ili kuweka utaratibu mzuri wa kuwasilisha Miswada ya Sheria Barazani pamoja na kuweza kuleta ufafanuzi katika matayarisho ya sheria hizo. Kuepusha uharaka ambao huisababishia serikali matumizi ya fedha ambayo yanaweza kuepukwa kwa kuchapisha upya kwa mara ya pili miswada kabla ya kujadiliwa Barazani na kuepusha kuzifanyia marekebisho sheria mara tu baada ya kutungwa na Baraza.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hayo, kamati inashauri serikali iiridhie Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kubadilisha muundo wake wa kada za utumishi kutokana na muda wote kutumia muundo wa

vitengo na badala yake itumie muundo wa idara kama zilivyo ofisi nyengine kama hizi katika nchi za Jumuiya ya Madola. Muundo huu utasaidia kupunguza changamoto ndogo ndogo zinazojitokeza na hivyo kupelekea ufanisi wa kiutendaji kwa watumishi wake.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na changamoto mbali mbali zinazoikabili Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kamati imeridhika na inaipongeza sana ofisi hii kwa utendaji wake ulio bora na kuitaka kuendelea kuwajibika zaidi hasa kwa vile Mwanasheria Mkuu na Naibu Mwanasheria Mkuu wake wamekuwa ni msaada mkubwa wa kamati hii. Pia kamati inaomba serikali ifanye juhudi ili Zanzibar iwe na akaunti yake kwa ajili ya mahujaji wake kuepuka migogoro na usumbufu unaowapata mahujaji wetu wote wanapokwenda hijja Makka, kwani hivi sasa akaunti hiyo ni moja tu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA (SMZ)

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inaundwa na kusimamiwa na idara na taasisi mbali mbali zilizogawika maeneo makuu manne katika kutimiza majukumu yake pamoja na Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba. Aidha, kamati inaipongeza sana wizara hii kwa ubunifu na uhodari wao katika kusimamia majukumu ya kazi hususan taasisi zinazoshughulikia ukusanyaji wa mapato pamoja na Idara Maalum za SMZ kwa uzalendo wao wa kulitumikia taaifa.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaunga mkono mpango wa serikali wa kuleta mfumo mpya wa Ugatuzi wa Madaraka Mikoani ambao utatumika katika taasisi hizi. Hivyo, katika kukabiliana na changamoto ambazo zitakuwa kikwazo katika utekelezaji wa majukumu yao. Kamati inaagiza Serikali za Mitaa kuwapatia

watendaji wake fursa za kimasomo katika program mbali mbali ambazo wanahitaji katika taasisi husika.

Mhe. Naibu Spika, kamati imeridhishwa na utendaji wa Mabaraza ya Miji kwa upande wa Pemba pamoja na Manispaa na Halmashauri za Unguja kutokana na kiwango kizuri cha ukusanyaji wa mapato ambayo yamekusanywa kwa vipindi tofauti. Hali ambayo imeleta faraja na kuonekana kufikiwa kwa lengo la kuanzishwa Mabaraza haya. Aidha, kamati imeona kuwepo kwa changamoto ya uhaba wa wataalam kama wahandisi, maafisa mipango na maafisa manunuzi na ugavi katika Mabaraza haya. Hivyo, kamati inashauri kwa Mabaraza hayo na yale yenye matatizo sawa na hayo kuhakikisha wameajiri wataalam wa fani mbali mbali ambao wanahitajika ili kusaidia kuleta ufanisi na kuleta tija kwa serikali.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu inapongeza sana juhudi za Baraza la Mji Chake Chake kwa kupata jengo jipya na la kisasa ambalo limepunguza kwa asilimia kubwa uhaba wa ofisi na usumbufu wa watendaji. Kamati inaomba viongozi wa Baraza hili kuitumia vizuri ofisi kwa kuitunza na kutunza samani na miundombinu mbali mbali iliyopo. Hata hivyo, kamati inaliagiza Baraza la Mji Chake Chake kulitumia jaa liliopo Vitongoji kwa kutupa taka na waache utaratibu wa kukusanya taka katika maeneo yasiyokuwa rasmi. Aidha, Baraza la Mji Chake Chake linaagizwa kuhakikisha kuwa linaweka makontena ya kukusanyia taka katika maeneo yote yenye msongomano wa watu ili kuepusha kuzagaa kwa taka kiholela katika Mji, kwani Mji huo ndio kioo cha Kisiwa cha Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaliagiza Baraza la Mji Chake Chake kusimamia vyema wafanyabiashara katika mpango wa utoaji risiti za mauzo kwa wananchi wawashajihishe na kudai risiti kwa maendeleo ya nchi yetu. Sambamba na hayo, kamati inalishauri Baraza la Mji Chake Chake kuliendeleza soko la Michakaini

(Mava Mbaruku) ambalo limeshatumia fedha nyingi za jamii lakini bado limeshindwa kukamilika na kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, kamati pia ilipata fursa ya kuangalia shughuli za Baraza la Mji wa Mkoani Pemba ambapo iliridhika na kumpongeza Mkurugenzi wa Baraza hilo kwa ubunifu wake ambao umepelekea kuweza kuwa na mpango bora wa maendeleo na kuweza kukusanya mapato kwa kuvuka lengo walilopangiwa. Kamati inaishauri wizara izidi kumpa moyo Mkurugenzi huyo na wafanyakazi wenzake kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, katika Halmashauri ya Kaskazini "B", kamati ilipata fursa ya kutembelea na kupokea taarifa ya mapato na matumizi ya Halmashauri ya Kaskazini "B" kupitia vyanzo vyake mbali mbali vya mapato. Hata hivyo, mapato hayo yameonekana kushuka sana kutokana na Serikali Kuu kuchelewa kulipa ada yao inayotokana na uuzaji wa mchanga.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaishauri serikali kufanya kikao cha pamoja kati ya Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ pamoja na Halmashauri ya Kaskazini "B" ili kufikia muafaka wa kuweka utaratibu bora wa malipo hayo, kwani hivi sasa kazi za Halmashauri hii zimezorota kutokana na ukosefu wa fedha unaowakabili.

Mhe. Naibu Spika, pia kamati yetu ilipata fursa ya kutembelea na kupata taarifa za Manispaa ya Magharibi "A" na Magharibi "B" kwa hakika kamati imeridhika na utendaji wa Manispaa hizo chini ya Wakurugenzi wao. Ingawa Manispaa hizo ni mpya zinakabiliwa na changamoto za idadi kubwa ya wakaazi na wahamiaji, miundombinu hafifu ya barabara, maji, umeme na skuli za msingi kwa kiwango kikubwa mabadiliko ya maendeleo

kwa manispaa hizo yanaonekana. Hivyo, tunaiomba serikali kuongeza nguvu na kuwapatia wataalam na vitendea kazi Manispaa hizo. Kamati yetu kwa kiasi kikubwa imeridhishwa na ukusanyaji wa mapato wa Manispaa hizo mbili ya Magharibi "A" na "B" ambazo ni mpya na tunaomba wazidi kuongeza juhudi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa miongoni mwa taasisi muhimu katika nchi yetu Ofisi za Wakuu wa Mikoa, hivyo ni wajibu wa taasisi hizo kuhakikisha wanasimamia vyema maendeleo, amani na usalama wa wananchi waliomo katika Mikoa hiyo. Kwa mukhtadha huo, kamati inaiagiza Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba kuhakikisha inachukua hatua za haraka kumaliza mgogoro wa ardhi uliopo katika Shehia ya Ndagoni, Wilaya ya Chake Chake. Vile vile kufuatilia kwa umakini baadhi ya viongozi wa Idara ya Ardhi, Serikali ya Mkoa na Wilaya au Shehia ambao wanashiriki kurudisha nyuma juhudi za kutatua mgogoro huu kwa hali yoyote ambayo itapelekea wananchi wa Ndagoni kupoteza imani kwa serikali yao kupitia mgogoro huu kwa ajili tu ya maslahi ya viongozi hawa au kwa manufaa ya mtu binafsi.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, kamati inaitaka wizara kwa kushirikiana na Mkoa pamoja na Baraza la Mji Wete kuendelea kusimamia vyanzo vya mapato bila ya kuwa na muhali na kuachana na kasumba za baadhi ya watu ambao hawataki mafanikio ya nchi yetu. Vile vile, kamati inashauri kwamba ni vizuri viongozi wa Mkoa huo wa Kaskazini Pemba kufuata utaratibu katika kushughulikia matatizo ya watumishi wa ngazi za chini ili kulinda haki zao za msingi na sio kuchukua hatua za maamuzi ambazo zitaleta athari kwa watumishi na jamii kwa ujumla bila ya kushirikisha mamlaka zenye dhamana ya kufanya maamuzi hayo kisheria.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande mwengine kamati inaupongeza uongozi wa Wilaya ya Kati Unguja kwa mafanikio mazuri

waliyofikia kiutawala na kiustawi wa jamii. Hata hivyo, wilaya hii inakabiliwa na ukosefu wa vyombo vya usafiri ambapo viongozi wake mbali mbali hulazimika kutumia vespa jambo ambalo ni changamoto kubwa katika kipindi cha mvua.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, uwepo wa bandari zisizo rasmi (bandari bubu) katika maeneo ya Uzi na Bungi kunapelekea wilaya hii kuvamiwa na wageni mara kwa mara pamoja kuingizwa kwa bidhaa za magendo na zisizokuwa na kiwango na hata madawa ya kulevya inasadikika hupitia bandari hizo. Hata hivyo, kamati imeridhika na mpango wa wilaya kujiandaa kujenga kituo kidogo cha ulinzi katika maeneo ya kuingilia Uzi ili kupambana na changamoto hizo.

Mhe. Naibu Spika, pia kamati ilifika na kutembelea Ofisi ya Wilaya ndogo Tumbatu na kujionea mambo ya msingi katika utekelezaji wa majukumu yao. Wilaya hiyo inakabiliwa na changamoto mbali mbali ambazo serikali inalazimika kuzichukulia hatua za haraka katika kusaidia maendeleo ya kisiwa hiki. Ukosefu wa wafanyakazi wa kisekta ikiwemo elimu, afya, kilimo, mazingira na kadhalika, ndio kizingiti kikubwa cha ufanisi wa maendeleo ya wakaazi wa Tumbatu pamoja na uhaba wa nyenzo za kilimo, uvuvi, usafiri na afya.

Mhe. Naibu Spika, kamati ilifanya ziara ya kuvitembelea vikosi mbali mbali vya Idara Maalum za SMZ kwa upande wa Unguja na Pemba na inapongeza sana juhudi zinazofanywa na wapiganaji wetu kwa kazi nzito wanazozifanya za kulinda, kusimamia na kudumisha amani na usalama wa raia na mali zao, pamoja na kuhakikisha kuwepo kwa amani na utulivu katika nchi yetu. Vile vile, pongezi za pekee ziende kwa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kwa kutoa huduma bora na za kisasa kabisa katika sekta ya afya kupitia vituo vyao mbali mbali Unguja na Pemba. Hata hivyo, vituo hivyo licha ya kutoa huduma za afya kwa karibu na wananchi wengi kutumia,

serikali kupitia Wizara ya Afya haivipatii dawa wala vifaa tiba kama vile vinavyopatiwa hospitali za serikali na vituo vyengine vya afya.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na changamoto hiyo kubwa, vituo hivyo hulazimika kubeba mzigo mkubwa wa kununua dawa na vifaa tiba kwa kutumia fedha za *OC* hali inayopelekea kukwama kwa utekelezaji wa baadhi ya shughuli. Hivyo, kamati inashauri kuwa ni vyema vituo vya afya vilivyo chini ya Vikosi vya Idara Maalum za SMZ vipatiwe dawa na vifaa vya kutosha kutoka Wizara ya Afya kutokana na vituo hivyo kutoa huduma kwa idadi kubwa ya wananchi walio karibu na maeneo yanayozunguka vituo hivyo.

Mhe. Naibu Spika, mbali ya hivyo, kamati inaishauri serikali kuongeza nguvu pamoja na kuzingatia hatua zinazochukuliwa na Jeshi la Kujenga Uchumi za kukifanyia maboresho makubwa kituo chake cha afya kiliopo Saateni ambapo lengo kuu la maboresho hayo ni kukifanya kituo hicho kiweze kutoa huduma za zaida kama vile kufanya operesheni za magonjwa mbali mbali. Hii itapunguza mzigo na msongamano wa wagonjwa katika hosptali kuu ya Mnazi Mmoja na kutimiza azma ya serikali kuifanya hospitali hiyo kuwa ya rufaa.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hayo, kamati inaendelea kutoa pongezi zake za dhati kutokana na hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa Mahanga ya Askari Kisiwani Pemba. Juhudi hizo za serikali zinatia moyo kuona kuwa serikali inawajali na kuwathamini vijana wetu na vile vile, serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kutekeleza kwa vitendo ahadi zake walizozitoa katika utekelezaji wa ripoti ya mwaka jana ya kamati hii na pia utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, licha ya mafanikio mazuri yaliyofikiwa katika idara zetu, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum katika ziara zake imeweza kubaini changamoto mbali mbali zinazorudisha nyuma maendeleo ya idara hii. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:

Ukosefu wa vitendea kazi ambavyo havikidhi haja ya askari wa vikosi hususan katika idara ambazo zinajihusisha moja kwa moja na uzalishaji wa kilimo na shughuli nyengine za kimaendeleo.

Mhe. Naibu Spika, uhaba wa sare *(uniform)* za askari ambapo katika baadhi ya vikosi, askari hufikia hatua ya kuazimana sare hizo.Vile vile licha ya juhudi kubwa kufanyika na kwa kiasi fulani mafanikio kuonekana lakini bado ukosefu wa hatimiliki na zaidi kwa upande wa Idara ya Mafunzo na JKU. Aidha, ukosefu wa wataalam katika vikosi hivi kwa ajili ya kuendesha shughuli mbali mbali za kitaalam. Kwa mfano, uhaba wa wataalam katika fani za *IT* (*Information System)*, wakandarasi (*Engineering*) na madaktari bingwa wa magonjwa ya binaadam.

Mhe. Naibu Spika, kutotumika kwa sheria inayohusiana na Utumishi wa Idara Maalum katika kuandaa maslahi ya wastaafu wa Idara Maalum za SMZ na kinyume chake kutumika sheria, kanuni na miongozo ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(ZSSF)* katika kuandaa maslahi ya watumishi wastaafu wa Idara Maalum za SMZ wakati wao si wanufaika wa mfuko huo. Kwa mfano, Kamishna Mstaafu wa Mafunzo hadi leo ni mwezi wa tisa bado hajalipwa mafao yake kutokana na mkanganyiko huo.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaona jambo hili ni lenye uzito katika utekelezaji wake na kwa kuzingatia mazingira ya Sheria ya Utumishi wa Idara Maalum inapaswa kutumia sheria yao katika kupanga na kulipa maslahi kwa mujibu wa inavyoelekeza na tukizingatia kwamba wao wako nje ya huduma za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Hivyo, kamati inashauri serikali kuandaa

mfumo maalum wa malipo ya askari wastaafu wa vikosi vyetu ili waweze kunufaika na utumishi wao.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, kamati inapongeza juhudi zao mbali mbali katika kuhakikisha kutoa elimu ya kujikinga na moto na uokozi katika jamii kwa njia tofauti. Aidha, kikosi kimefanikiwa kuimarisha huduma za Zimamoto na uokozi Miji na Vijiji, kuimarisha huduma za Zimamoto na uokozi katika Viwanja vya Ndege, kupatikana kwa hatimiliki katika maeneo yanayomilikiwa na KZU.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kikosi kimeendelea na ujenzi wa Kituo cha Zimamoto Marumbi ambacho kitaanza kutumika hivi karibuni, kupata msaada kwa baadhi ya vifaa vya uokozi kutoka Serikali ya Ujerumani, pia kutoa mafunzo kwa maafisa na wapiganaji katika utumiaji wa vifaa vya uokozi mjini ambapo jumla ya wapiganaji 50 waliopatiwa mafunzo hayo tayari wanatoa huduma katika bandari za Malindi na Mkoani Kisiwani Pemba.

Mhe. Naibu Spika, licha ya mafanikio hayo yaliyopatikana katika Kikosi cha KZU bado kinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa visima vya kuchukulia maji pamoja uchakavu wa miundombinu ya maji *(fire hydrant)* katika maeneo mbali mbali ya Mji wa Unguja na Pemba. Hili husababisha tatizo la ukosefu wa maji na linahitaji kushughulikiwa kwa haraka katika kukabiliana na ajali za moto.

Mhe. Naibu Spika, aidha ukosefu wa huduma za maji katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar, kutokana na ukosefu wa miundombinu ya umeme na maji katika hodhi la kuhifandhia maji lilipo katika kituo kipya cha Zimamoto uwanjani hapo linarudisha nyuma juhudi za wapiganaji hao katika kupambana na majanga ya moto katika uwanja huo ambapo kwa sasa huduma hizo zinahitajika kwa kiasi kikubwa kutokana na kuongezeka kwa

shughuli kiwanjani hapo. Pamoja na changamoto hizo pia lipo tatizo la *parking* kwa magari ya Zimamoto kwa kituo cha zamani cha Uwanja wa Ndege. Kamati inashauri ni vyema kwa taasisi zinazohusika zikubaliane ili kujenga jengo jipya la *parking* katika eneo hilo la kituo cha zamani.

Mhe. Naibu Spika, kamati inashauri KZU Uwanja wa Ndege kupatiwa mgao wa makusanyo ya kifungu cha *safety fee* ambacho Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wamepewa ruhusa ya kutumia fedha hizo. Kamati inaamini kuwa endapo mgao huo utapatikana utaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto zinazowakabili ikiwemo ufinyu wa bajeti katika uendeshaji wa kikosi hiki.

Mhe. Naibu Spika, katika ujenzi wa mahanga ya askari unaoendelea Kisiwani Pemba kwa upande wa KMKM na Idara ya Chuo cha Mafunzo, kamati imeona litakuwa ni jambo la busara baada ya kukamilika ujenzi huu, serikali kuwapatia samani (*furniture*) mpya katika nyumba zote za maafisa na pia katika mahanga ya wapiganaji ili kwenda sambamba kati ya majengo na vifaa vyake. Aidha, kamati inazidi kutoa msisitizo kwa wizara kwa kushirikiana na Idara Maalum ya SMZ kutafuta hatimiliki ya maeneo yote za kambi ambazo bado hazijapata hatimiliki hiyo.

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, katika kutimiza wajibu na majukumu yake Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum imetuma vyema Kanuni ya 106(1) ya mwaka 2016 na kutoa ushauri na mapendekezo ambayo matumaini yetu kwamba, yataleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku kwa serikali kupitia Wizara ya nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumisi wa Umma na Utawala Bora kwa pamoja na Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum.

Mhe. Naibu Spika, kamati inawashukuru sana huu ni muhtasari lakini kitabu chetu kina kurasa karibu 120 ambacho wajumbe wote wameshagaiwa. Kwa hivyo, tunaomba wavisome kwa undani wataona mambo mengi ambayo yamo. Kwa hivyo, kamati inawashukuru sana Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza la Wawakilishi pamoja na watendaji wengine wote wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi waliochangia kwa njia ama nyengine katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya kamati hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Machano Othman Said, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi. Waheshimiwa Wajumbe tuna wachangiaji watano nategemea kwamba wachangiaji wengine watakuja. Kwa hivyo, baada ya ripoti ya Mhe. Mwenyekiti tutaanza majadiliano, lakini kabla ya hapo naomba nimpishe Mwenyekiti, Mhe. Shehe Hamad Mattar ili aweze kuendelea na shughuli yetu hii ya leo.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tunaanza na kuchangia ripoti iliyoko mbele yetu ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum na mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa Mhe. Ali Suleiman Ali.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii muhimu ya kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mwenyekiti wetu wa Kamati, Makamo Mwenyekiti, Wajumbe wote wa kamati na wadau mbali mbali ambao wameshirikiana nao kutuletea taarifa hii muhimu, juu ya kuhakikisha kwamba tunayoyazungumza hapa ni maelekezo na taarifa muhimu zilizopatikana kwa maendeleo ya nchi yetu yanayopatikana kutokana na kamati zetu hizi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba ripoti hii ina wizara muhimu mbili, Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, lakini pia tuna Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Zote nazipongeza kwa dhati na nasema kwamba sitogusa mote, isipokuwa nitagusa baadhi ya maeneo. Lakini nakiri kwamba pale nitakapogusa wale niliokuwa sikuwagusa wote nimewapongeza kwamba nawaunga mkono kutokana na juhudi zetu ili twende vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza na ukurasa wa 19 - 20 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mhe. Mwenyekiti, tunaamini kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ni hazina kubwa na muhimu katika nchi, bila ya kuwa na wanasheria au bila ya kuwa na sheria nzuri hatwendi. Kwa hivyo, kwanza nimpongeze Mwanasheria Mkuu, Naibu Mwanasheria Mkuu na watendaji wao wote kwa kazi nzuri wanazokwenda nazo. Kwa sababu tunaamini kwamba hizi sheria mbali mbali tunazozitunga hapa zinapita mikononi mwao, zinatufikia sisi, halafu ndio zinakuwa sheria.

Kwa hivyo, tunawapongeza kwa kazi nzuri wanazokuja nazo na hasa niseme kwamba mimi kama Mwenyekiti wa Kamati inayohusu Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na Wizara ya Habari, Utalii na Michezo nimeridhika nazo. Ridhiko langu kubwa namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tumalize Baraza hili salama, ili Mhe. Rais apate muda wa kupitia sheria iliyopitishwa juzi ya udhalilishaji juu ya watoto wetu ambayo ni Sheria ya Jinai na Sheria ya Adhabu. Kwa hivyo,

nasema naipongeza namuomba sana Mwanasheria Mkuu atafute vijana wamsaidie zaidi ili kila penye kero tuhakikishe tunalipatia ufumbuzi liondoke katika nchi yetu.

Jengine niseme tu kwamba katika kitabu hiki nitachangia ukurasa wa 20 changamoto namba (ii) na (iii), "Ongezeko kubwa la kesi zinazohusiana na migogoro ya ardhi".

Mhe. Mwenyekiti, tatizo la ardhi ni kubwa sana katika nchi yetu na serikali imejitahidi sana na katika jitihada zake imesema moja kwa moja kwamba imeweka sheria hizi kwa manufaa ya kupunguza adha. Sheria za ardhi zimeundiwa mahkama yake na Mahkama ya Ardhi iendeleze mambo ya ardhi tu, lakini bado matatizo tunayo katika nchi yetu. Kwa hivyo, namuomba Mwanasheria Mkuu kutokana na migogoro ambayo ipo na tunaomba iondoke basi juhudi iongezwe hili suala liondoke.

La tatu katika hiyo changamoto, "Kutokuwepo kwa mashirikiano ya kutosha kutoka kwa taasisi zilizokasimiwa mamlaka ya kusimamia kesi, kwani baadhi ya wakati hata kesi hizo zinapomalizika hushindwa kutoa taarifa hiyo katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ambayo ndiyo inayokasimu mamlaka kwao". Yaani naamini kwamba kama itakwenda kesi na mambo yote huko mwanasheria anachelewa kupata muda kutokana na taratibu zake. Kwa hivyo, nasema tu kwamba vyombo vinavyohusika katika sheria kama hizi basi ni wajibu wao kufanya haraka kupeleka zile taarifa ili ile sheria ifanye kazi yake. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo napongeza sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kazi nzuri wanayoendelea nayo.

Jengine Mhe. Waziri wetu na Naibu Waziri hawa ni wasimamizi wakuu wa shughuli zote za wizara. Kwa hivyo, kwa juhudi yao kwa kipindi hiki niseme marekebisho makubwa yaliyotokea niwapongeze kwa dhati kwa kazi zao. Kusema kweli Mheshimiwa mimi nasema familia inaundwa na wana familia wenyewe. Maana

ya kusema hivyo kwamba Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni familia, Wizara ya Katiba hapewi mtoto wa pembeni wanapewa wenyewe wale wana familia. Madhumuni yangu nasema wana familia ni wale walengwa wa uchungu wa nchi hii, maana ukimpa mwengine yeyote hatari. Kwa hivyo, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa imani yake na mwenendo wake mzuri yeye na Naibu Waziri na watendaji wetu wote katika wizara hiyo.

Ukurasa wa 24 unazungumzia habari ya Mahkama. Mhe. Mwenyekiti, ili kuhakikisha kazi zinaendelea vizuri Mahkama zimegaiwa kama ifuatavyo: Kuna Mahkama ya Mwanzo, Mahkama ya Wilaya, Mahkama ya Kadhi wa Wilaya, Mahkama ya Kadhi ya Rufaa, Mahkama ya Mkoa na Mahkama Kuu. Vile vile kuna jumla ya vitengo vya Mahkama vitatu hadi sasa ambavyo ni Mahkama ya Kazi, (migogoro ya kazi), Mahkama ya Biashara (migogoro ya biashara) na Mahkama ya Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nazungumzia sana watoto, nimuombe sana Mhe. Mwanasheria Mkuu au Mhe. Waziri suala la watoto. Kwa bahati nzuri Mhe. Waziri aliifungua Mahkama ya Watoto Mahonda na Mahkama ile inaendelea vizuri, lakini namuomba sana tuwaongezee wafanyakazi au mahakimu. Kwa sababu kesi zinakwenda nyingi lakini tunayemtegemea ndugu yetu mmoja tu sijui kama hakimu au jaji sina uhakika yupo peke yake. Kwa hivyo, ni vyema tukaongeza wafanyakazi ili kesi hizi ziende haraka, malalamiko yetu tunalilia watoto wetu, malalamiko yetu vitendo vya udhalilishaji vimekuwa vingi hivyo tunaomba sana hili liangaliwe. Mahkama nyengine zote kama Mahkama za Wilaya, za Kazi, za Biashara najua hizo zina maeneo yake hazina usumbufu sana, kwa sababu watakaotumia mahkama hizo wana uwezo wa fedha lakini watoto wanataka wapate watu washauri wazuri wa kuwasaidia shughuli za kesi zao.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 32 nitazungumza kidogo, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Mhe. Mwenyekiti, ndugu yetu huyu au Mkurugenzi huyu na watendaji wake kwa kweli wana kazi nzito halafu wana kazi ya lawama. Unajua unapokuwa Askari Polisi sio Mwanajeshi, Mwanajeshi unakwenda kupigana, lakini unapokuwa Askari Polisi una kazi nzito katika nchi yako. Kwa sababu wakati mwengine inabidi umkamate mtoto wako au mtoto wa ndugu yako, panataka utaratibu mzito hata utimie, unakosa amani wakati mwengine. Mkurugenzi wa Mashtaka Mhe. Mwenyekiti, kwa dhati kabisa anafanya kazi nzito, anafanya kazi ambazo kupindukia kiwango chake. Kwa hivyo, mimi naomba tumsaidie kwa ule uhaba aliokuwanao na nitasoma changamoto ukurasa wa 32 chini kabisa.

(a) Uhaba wa vyombo vya usafiri;
(b) Kutoingiziwa fedha za matumizi kwa wakati;
(c) Kushindwa kuendelea na kesi kutokana na mashahidi kushindwa kutoa mashirikiano kikamilifu; na
(d) Kuongezeka kwa wimbi la kesi za udhalilishaji siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, tufanikiwe hili pamoja na kuifurahia sheria ambayo tumeiweka itakuja hivi karibuni. Nasema tu kwamba ili kumpunguzia au kumuongezea uwezo wa kufanya kazi zake na kupunguza hizi kesi, basi haya maombi yaliyoombwa na kamati mimi naipongeza kwa dhati kabisa, tuyaone na tumsaidie ili afanye kazi zake kwa ufanisi. Kwa sababu bila ya hayo atafanya kazi bado katika mazingira magumu lawama zitamwendea yeye kumbe yeye hana vianzio au hana pato la kutosha katika utekelezaji wa kazi zake.
Mhe. Mwenyekiti, nikimaliza Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba niingie katika Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Mhe. Mwenyekiti, huku nimpongeze sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wote

wanaohusika na wizara hii Makamanda wetu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, hasa tukiangalia kwamba wao ni roho ya sehemu zetu za wilaya, mkoa na vikosi. Vile vile ni roho katika utekelezaji wa kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa nitakuwa na mambo machache sana lakini nitazungumza mpaka utaniwashia taa. Kwanza niipongeze mikoa yote na wilaya kwa kazi zao nzuri wanazofanya, lakini naunganisha moja kwa moja nivipongeze vikosi vyetu vyote kwa kazi nzuri wanazofanya na naona tu kwamba mabadiliko yametokea tukitaka tusitake ni mazuri, wanafanya kazi katika moyo wa kujituma askari wetu. Kwa sababu mimi askari namuonea huruma sawasawa na mwanangu niliyemzaa, shida ya askari naijua ndiko tulikotokea huko huko.

Mhe. Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja kama inagaiwa kiwi shilingi 400 au 1,000, au kalamu kila askari apate kalamu hii shilingi 200 kama hukumpa ugomvi. Kwa hivyo, askari baada ya Mhe. Rais kupitia Tume ya Utumishi kuwaona kidogo waongezwe nguvu, askari wamepata imani. Mimi nampongeza sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, lakini pia nampongeza Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kusimamia vizuri haya yanayopatikana ili wayafikie. Kwa hivyo, napongeza hapo halafu naingia katika sehemu ninayotaka kuichangia.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mkoa wa Mjini Magharibi tuna manispaa tatu tumebahatika sana. Lakini bahati nzuri au mbaya Mheshimiwa mpaka leo tuna kero kubwa. Kero ya mwanzo nataka nimwambie Mhe. Waziri niliizungumza kipindi kilichopita na leo nakumbusha. Hili jengo letu la Ofisi ya Mkoa Amani mpaka leo limezungushwa mabati yanaibiwa tu, yanatoka haya watu wanaiba na kutia mengine. Hebu aieleze dunia hii na atueleze wana Mkoa wa Mjini Magharibi kuna tatizo gani? Jengo lilivunjwa ambalo lilikuwa linatusaidia *ZFA* na walikuwepo

wengi wa wilaya pale na wengine, limeondoka kwa nia njema lakini leo atueleze ile nia njema yenyewe imefikia wapi. Mheshimiwa ni jambo la aibu sana.

Ukienda Kaskazini Unguja ofisi zao kama Ulaya, ukienda Kusini Unguja kama Ulaya, ukienda zako Micheweni kuzuri, Kaskazini Pemba, hapa tumekosa nini na mkoa wetu tunasema ni mkubwa ambao una hadhi ya kila kitu na mkoa unaoingiza fedha kuliko mikoa yote. Kuna nini? Mhe. Waziri namuomba sana rafiki yangu, mwenzangu tumetoka tangu 1995 tumo sote mpaka nilitoka nimerudi tumekutana. Kwa hivyo, namuomba sana Mheshimiwa atuangalie hapa huu mkoa umekosa kitu gani hata ukakosa ofisi, yaani jengo lile pale limejibana aibu.

Mhe. Mwenyekiti, tunakwenda katika Manispaa Bara kwenda kutembea kwa wenzetu ile Manispaa unaogopa kuingia, unajisikia kama uko Ulaya. Leo ile pale ni mkoa na ofisi yake pale Vuga lakini imepitwa na wakati Mheshimiwa. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri aje katika taarifa za majibu ya baadae na Mhe. Mwenyekiti...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa malizia muda wako.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Eee, Mheshimiwa nipe dakika mbili, nakuomba sana nimalizie doh! Mheshimiwa umeshanichanganya kidogo, haya. La pili niseme kwa ufupi baada ya hilo nimuombe sana Mhe. Waziri katika changamoto katika ukurasa huu wa 70 naomba sana nije nipate jibu baadae. Ongezeko kubwa la idadi ya watu ndani ya Mkoa wa Mjini Magharibi, ukosefu wa majengo ya kudumu ya Wilaya ya Mjini Magharibi 'B', jengo nalo; uhaba wa vitendea kazi, uharibifu wa mazingira ikiwemo vyanzo vya maji na uchimbaji wa mchanga usiofuata utaratibu uliowekwa. Lakini kuongezeka kesi za udhalilishaji wanawake na watoto, uhaba wa madarasa katika skuli za msingi na sekondari, kutokuwepo kwa

kituo cha magari ya abiria ya daladala. Hii mimi hata sina habari nayo daladala hazinishughulishi.

Mhe. Mwenyekiti, moja tu hapa lililokosekana, niiombe kamati kupitia Mhe. Waziri na yeye alipate tatizo la Mkoa wetu wa Mjini ni maji. Mkoa wetu wa Mjini Magharibi nachukulia sana Wilaya zetu mbili 'A' na 'B' tatizo la maji ni usumbufu mkubwa, manispaa zetu zinakosa hadhi na zinakosa kujiendesha. Kwa sababu balaa hili limetukamata vibaya sana. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri hili liangaliwe maji bado ni tatizo na tatizo la usumbufu wa kutupa taka katika maeneo yetu.

La mwisho kwa kuokoa muda na ninaheshimu sana kiti chako, tatizo jengine ambalo limetukabili katika maeneo yetu mazingira yetu bado yanatisha siku za mvua. Kwa hivyo, narudia tena, kipindi kilichopita nilimuomba Mhe. Waziri tutembee lakini bahati mbaya hakufanikiwa, hiki nitamuomba tutembee tusikae maofisini, umefika wakati wa kutizama mitaro yetu ya maji ambayo inahatarisha amani na usalama siku za mvua kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda umekwisha sina njia nyengine niseme tu kwamba, kwanza nawapongeza tena lakini naiunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru, sasa ninamwita Mhe. Ali Khamis Bakar maarufu Dohlo akifuatiwa na Mhe. Ali Salum Haji (Mnadhimu).

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia ripoti iliyo mbele yetu ambapo pia na mimi ni Mjumbe wa Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza kamati yangu kwa kazi kubwa ambazo tumezifanya. Vile vile niwapongeze Mawaziri na Manaibu Mawaziri ambao tulikuwa nao katika kipindi chote cha kamati na walitupa mashikiriano makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niwapongeze wapiganaji wetu wa vikosi vyetu vya SMZ kwa kazi kubwa wanazozifanya kwa kutoa ushirikiano ambao waliuonesha katika kipindi chote cha kamati ambapo tulikwenda.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitakuwa na mchango mkubwa sana kwa vile ni mwana kamati isipokuwa kuna baadhi ya sehemu nitazigusia ili kukazia tu kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa Kikosi chetu cha Zimamoto na Uokozi (KZU). Kikosi hiki Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashuhuda kazi nyingi wanazozifanya miongoni mwa kazi zao mbali ya zile ambazo ni za ulinzi, lakini kuna kazi kubwa ambazo wanazifanya kwa ajili ya wananchi kwa kuokoa roho wakati mwengine inapotokezea mambo ya moto. Vile vile kuokoa mali pale ambapo kumetokezea masuala ya moto.

Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sisi tukiwa kama wana kamati tumeona juhudi kubwa wanazozifanya askari hawa juu ya utendaji wao wa kazi. Lakini cha kushangaza Mhe. Mwenyekiti, katika Uwanja wa Ndege kuna hodhi ambapo tumeliona, hodhi hili linakosa umeme jambo ambalo lingekuwa na umeme hodhi hili lingewasaidia katika upatikanaji wa maji safi ambayo yangewasaidia wao katika harakati zao za uzimaji wa moto pale ambapo imetokezea.

Lakini cha kushangaza Mhe. Mwenyekiti, jana alipokuwa akichangia Mhe. Jaku Hashim Ayoub alisema hapa kwamba tunatakiwa viongozi tumuunge mkono Mhe. Rais ili kuona zile juhudi ambazo anazifanya tusimuangushe. Mhe. Mwenyekiti,

tumekwenda pale kama wana kamati tumeambiwa kuna agizo la Mhe. Rais kwamba hodhi lile lipatiwe maji na kuna miundo mbinu mibovu ya barabara ambayo walisema kama ni agizo la Mhe. Rais ilitakiwa litekelezwe ili askari wale waweze kupata huduma ambazo zinastahiki katika kazi zao.

Lakini la kushangaza hadi leo kazi hii imekuwa ni kilio jambo hili halikutekelezeka. Vile vile kama wana kamati na sisi tulipofika pale ni mara ya pili agizo hili tumelipeleka lakini cha kushangaza Mhe. Mwenyekiti, maagizo ya kamati hayathaminiwi. Mhe. Mwenyekiti, kusema la ukweli mambo haya ndio hayo majipu yanayotakiwa yatumbuliwe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kwamba askari wetu hawa wana kazi kubwa. Ni juzi tu mimi nimeshuhudia wakati nakwenda zangu nyumbani upande wa Maungani nimeona pale kuna jaa sijui kuna mtu aliingiza moto pale kwa bahati mbaya nimeona askari wetu jinsi wanavyohangaika wanaenda kuzima moto pale karibu ya Afisi ya Mawasiliano. Mhe. Mwenyekiti, askari wetu kwa kweli wana kazi kubwa wanazozifanya kila siku, vile vile tumeona kwamba kuna baadhi ya changamoto hata sisi upande wa wananchi ujengaji holela wa maeneo ambayo pale ambapo kutatokezea masuala ya moto askari wetu hawa wanashindwa kwenda kufanya kazi zao ipasavyo.

Kwa hiyo, hapa niiombe serikali izingatie zaidi maeneo ya ukataji wa viwanja wale ambao watapewa viwanja kwa ajili ya kujenga majumba akionekana tu mtu amezidi katika eneo lile na kupelekea kuhatarisha maisha ya jamii ambapo zinaweza kutokezea wakati mwengine matatizo kama ya moto na masuala mengine. Mimi nasema kwamba serikali waliangalie jambo hili ili kuweza kuwalekeza wananchi juu ya ujengaji mzuri wa majumba, vile vile na wananchi jamani tuweni na muamko wa sasa tuache ile hali ya muhali ya kuweza kujenga majumba mpaka chini yaani ile barabara tukaifinya kiasi ambacho kama kungetokezea tatizo

askari wetu au jambo jengine lililokuwa hata kama si la askari unashidwa kuweza kutoa huduma. Mhe. Mwenyekiti, mimi niwapongeze tu askari wetu hawa na kikosi hiki kwa kazi kubwa wanazozifanya.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kwa aina ya pekee niende kwenye kikosi cha KMKM. Hiki kwa pamoja nivishirikishe na JKU. Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia kama wana kamati kwa kweli askari wetu hawa au vikosi vyetu hivi vina kazi kubwa ambazo wamezifanya kutokana na siku hadi siku ukiacha suala la ulinzi lakini wanatoa huduma nzuri kwa jamii. Mhe. Mwenyekiti, tumeona askari wetu hawa jinsi ambavyo wanahangaika wanakwenda katika sehemu za ulinzi. Vile vile kwa jamii pale ambapo pametokezea matatizo kwa mfano kama askari wa KMKM wanawezekana pengine wamekwenda kwenye doria la kulinda nchi lakini baada ya kurudi tu wanaweza wakaripotiwa kama kuna tatizo labda pengine kuna wananchi wamekwenda baharini pengine umevuma upepo wamepotea au wamepata gharika na vyombo vyao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa niwapongeze kwa kazi kubwa wanazozifanya. Naiomba wizara iwaangalie juu ya upatikanaji wa mafuta kwa sababu kero zao kubwa katika kikosi chetu hiki tulipokwenda pale tumeambiwa kuwa ni suala la mafuta. Mafuta wanayopewa ya mgawanyo wanatumia mpaka kufikia hatua ya kuwa mafuta yale hawana tena hawajui la kufanya.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, niiombe wizara kwa kushirikiana na kikosi chetu waangalie kwa jicho la huruma vikosi vyetu viwili cha JKU pamoja na KMKM kwa ajili ya mgao wa mafuta pale ambapo bajeti yao itakapokuja katika wizara.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende Chuo cha Ualimu *IPA* kule Kisiwani Pemba. Mhe. Mwenyekiti, changamoto nyingi ambazo tulikwenda tukazikuta pale licha ya ambazo tulizieleza

katika kitabu hiki ni ukosefu wa walimu ambao walikuwa wanatakiwa wawepo pale na pia ubovu wa miundo mbinu ya barabara pamoja na ukosefu wa mabweni kwa ajili ya wanafunzi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme hii ya tatu idadi ndogo ya wanafunzi ambao wanakwenda kujiunga pale. Mhe. Mwenyekiti, tumeona kwamba miongoni mwa mambo ambayo yanasaidia kwa mwanafunzi na analokwenda kufuata pale ni elimu. Lakini mwanafunzi huyu akiona kwamba anapokwenda pale kutaka kujiunga kutaka kutafuta ile elimu pana changamoto nyingi ambazo zinamfanya yeye akose elimu ile.

Basi kweli Mhe. Mwenyekiti, lazima changamoto hii ya uhaba wa wanafunzi itakuwepo kwa sababu mtu pale anakwenda kutafuta taaluma lakini akifika taaluma ile hali halisi ya kile chuo kidogo hairidhishi mwanafunzi huyo lazima atasema mimi kwa kipindi hiki siendi kujiunga au natafuta chuo kingine cha kujiunga.

Kwa hiyo, naiomba wizara kwamba kituo kile au skuli ile au chuo kile kipewe hadhi yake ya kama chuo ili wanafunzi hawa wawe na kazi kubwa ya kwenda kujiunga pale na vile vile kile ambacho kimekusudiwa kutolewa pale kiweze kupatikana ili wanafunzi hawa waweze kupata ile elimu ambayo imekusudiwa katika kiwango cha elimu ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo sina mcahango mkubwa isipokuwa niendelee kuipongeza kamati yangu kwa kazi kubwa ambazo tumezifanya na nimpongezee tu Mhe. Mwenyekiti kwa uwasilishaji wake mzuri wa ripoti yetu. Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Ali Khamis Bakar na sasa namwita Mhe. Ali Salum Haji na baadae akifuatiwa na Mhe. Bahati Khamis Kombo. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa dhati kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi.
Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wawili, Mhe. Haroun Ali Suleiman na Mhe. Haji Omar Kheri kwa namna wanavyosimamia utekelezaji wa kazi katika taasisi zao.

Lakini pia nimpongeze kaka yangu Mhe. Machano Othman Said, Mwenyekiti wa Kamati pamoja na wajumbe wake namna wanavyoweza kuratibu shughuli mbali mbali za wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakwenda katika maeneo kama matano tu na naanza na ukurasa wa 8. Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 8 sehemu ya tano hapa inazungumzia namna kamati ilivyotembelea Pemba katika taasisi mbali mbali. Ni jambo jema lakini kidogo tu Mhe. Mwenyekiti, mimi niwaombe kamati wanapotuletea taarifa basi ni vyema wakaenda ndani zaidi ili unapotizama hii ripoti unapata falsafa ya kuona lile ambalo umeliona changamoto na mahitaji au mafanikio. Hapa wameelezea tu wametembelea idara sita lakini waliloliona hawajatueleza changamoto wala mafanikio. Sasa inakuwa ni kazi kubwa na kunakuwa na mijadala mirefu katika kuchangia suala hili.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, niombe kamati basi wanapotembelea basi wajipangie yale maeneo ambayo *specific* ya *priority* katika nchi yetu. Kuna maeneo ambayo ukiyaangalia kinadharia basi haya ni vyema wangeanza mwanzo kuyatembelea, limo moja humu ukiliangalia ni sehemu ya Wizara ya Afya Pemba. Lakini ni vyema maeneo ambayo yana umuhimu ni yale ambayo yanagusa wananchi moja kwa moja wakati wote kwa mfano afya, elimu pamoja na *ZAWA.*

Humu si vibaya lakini nilishangaa kwamba kuna maeneo ambayo yalikuwa yana umuhimu kuweza kuyatembelea. Miongoni mwa waliyoanza kuyatembelea ni eneo la Baraza la Wawakilishi. Sasa naona Baraza la Wawakilishi lipo hapa hapa na watu wa idara wapo hapa hapa kila wakati, sio vibaya. Lakini ni vyema tungeanzia kule ambako kunagusa hisia za watu na watu wanakuja na malalamiko na kila siku kelele zimekuwa nyingi.

Sasa nilitaka Mhe. Mwenyekiti, basi atakapokuja kufanya majumuisho atusaidie yale ambayo wameyaona katika hizo taasisi ambazo walizitembelea. Kwa sababu tumekuwa tukipiga kelele wameeleza huku na kikubwa walichokitembelea ni kuangalia kiwango cha utendaji wa kila mtumishi wa umma kwamba anayafahamu majukumu yake ili kuongeza ufanisi wa kazi katika maeneo yao.

Sasa matatizo yamekuwa mengi, kelele zimekuwa nyingi, ufanisi hakuna wanafunzi wanafeli sana, Wizara za Elimu walimu hawasimamii kazi zao vizuri, lakini ukenda katika Sekta ya Afya tunalalamika mpaka tunaanza kuwaleta watoto wanakatwa mikono. Sasa wanapokuta yale matatizo basi angalau watueleze yale ambayo wameyakuta na ufanisi ambao umepatikana na changamoto zinazowakabili, ili tujue basi tuweze kuishauri serikali kama kuna maeneo ambayo wameyakuta yana matatizo ya vifaa namna gani ya kununua vifaa hivyo. Kama wamekuta matatizo ya ajira basi tuweze kuishauri serikali namna gani ya kuweza kuajiri watu kwa haraka.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, liko katika ukurasa wa 11 kuhusiana na Nyaraka. Mhe. Mwenyekiti, katika suala la nyaraka changamoto hapa kuna maelezo katika *column* (a) wameeleza ukusanyaji na uhifadhi mdogo wa nyaraka kutokana na kukosekana kwa eneo la kuhifadhia nyaraka katika taasisi hii kwa nafasi katika jengo lao. Ni jambo la kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, kwamba tunaanza kuzungumzia suala la ufinyu na uhaba wa eneo

katika ukusanyaji wa nyaraka. Sasa hili ni tatizo kubwa kwa sababu nyaraka ni kitu kikubwa tunahitaji kupata kumbukumbu zilizokuwa nzuri ambazo watu wasije kupoteza kumbukumbu za nchi.

Sasa mimi nishauri Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu wamesema kwamba wana eneo wanataka kulifanyia kazi, yaani idara wanataka kujenga, basi tujue hilo eneo ambalo wanatarajia Idara ya Nyaraka kujenga maana yake lipo katika hatua gani na wanategemea lini hilo jengo kuweza kulikamilisha ili kuondokana na kadhia hii.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika taasisi hiyo hiyo ambalo limenipa mashaka kwenye *paragraph* ya mwisho kabisa wameelezea kwamba taasisi imeagiza kila wizara katika taasisi iweke chumba maalum cha kuhifadhia kumbukumbu. Hapa nimeanza kupata mashaka kwamba sisi tuna sekta maalum ya kuhifadhi kumbukumbu lakini sasa hivi tunaanza kupelekea kuishauri serikali kwamba kila wizara waanze kukusanya kumbukumbu waweke eneo la kuhifadhi kumbukumbu katika taasisi zao. Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa napata mashaka kwa sababu najua umuhimu wa kumbukumbu kama kitu ambacho au idara ambayo tuliipa mamlaka ya kuhifadhi kumbukumbu ilifikia pahala kumbukumbu zikaibiwa, sasa tuanze kurejesha tena matatizo kama haya kuyarejesha katika mawizara.

Mhe. Mwenyekiti, khofu yangu kwamba huko tunakoelekea tunaweza kuja kuharibikiwa zaidi. Basi ni vyema mimi ushauri wangu kama itakuwa inaweza kwamba kwa kila taasisi kuhifadhi nyaraka zake katika hilo jengo la nyaraka ambalo litajengwa, basi ni bora wangeweka wafanyakazi wa kila taasisi ambao watapata elimu ya kutosha na eneo ambalo litakuwa na usalama wa kutosha ili kuja kuhifadhi nyaraka.

Mhe. Mwenyekiti, vyenginevyo kuanzisha maeneo au watwambie maana pia hawajatuelezea ni nyaraka gani ambazo zitahifadhiwa na Idara ya Nyaraka lakini nyaraka gani ambazo zitahifadhiwa na taasisi husika. Sasa hili kamati naona hawajatueleza ipasavyo tukaweza kufahamu Mhe. Mwenyekiti, lengo na dhamira waliyokusudia katika uhifadhi wa nyaraka katika taasisi husika.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nilitaka kulizungumzia liko katika ukurasa wa 12 Maoni na Maagizo ya Kamati. Kamati inatoa maagizo yafuatayo. Kamati inaagiza taasisi hii kufuatilia kwa karibu hatua zilizofikiwa juu ya ujenzi wa jengo hilo la Afisi za Nyaraka lilioko Koani. Basi nilitaka kujua tu jengo hilo limefikia kozi gani na bajeti yake ikoje, nini kinahitajika na nini kimekwama, kimekwama wapi na matatizo gani, nini mipango ya serikali katika kulimaliza hilo jengo ili kuweza kuhifadhi jengo letu katika hali za uhalisia uliokuwa mzuri na wa kuridhisha.

Mhe. Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo nilitaka kuyachangia ni ukurasa wa 61 kifungu cha 3.3.3 Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili wanazungumzia kwamba idara imeendelea kufuatilia na kusimamia miradi mbali mbali ya KMKM, Chuo cha Mafunzo, JKU na KVZ. Miradi hiyo ni ujenzi wa nyumba za askari, mahanga kwa upande wa Pemba, ujenzi wa Chuo cha Kurekebisha Tabia wanafunzi watoto kwa upande wa JKU, kuna ujenzi unaoendelea wa Skuli za Sekondari Mtoni na ujenzi wa Kiwanda cha Kutengenezea Viatu.

Mhe. Mwenyekiti, ni jambo jema lakini bado nasema tena kwamba kamati pia haijatuweka wazi tukapata kujua maendeleo ya hii miradi hatua zilizofikia na kama kuna maeneo ambayo wamekwama na tatizo lililowakwamisha na nini mafanikio yake. Lakini pia atwambie nini matarajio baada ya hii miradi itakapomalizika.

Lakini pia kuna mradi mmoja basi mimi kamati au serikali itakapokuja mwezi wa 9 huko ije itusaidie walipofikia ule mradi wetu wetu wa Wakala wa Ulinzi, umefikia hatua gani kama sera imeshamalizika ama jambo gani kwa sababu ni eneo ambalo liko very *sensitive.* Mhe. Mwenyekiti, katika aneo ambalo wananchi walitegemea ni eneo la ajira. Sasa na huu mradi wa uwakala umechukua muda mrefu na mara zote tunasema kwamba watu wanapoandaa vitu kama hivi basi wajipange ili mambo haya yamalizike kwa haraka.

Kwa sababu maeneo ambayo sasa hivi tunatumia yanapoteza pesa nyingi sana, vikosi vinalinda masheli, ofisi lakini hakuna utaratibu uliokuwa mzuri. Sasa jambo hili likimalizika huu mradi utawasaidia vijana wengi sana kumaliza tatizo la ajira katika nchi yetu na hasa vijana wale wazalendo.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo nataka kulizungumzia na ni la mwisho kabisa lile ambalo Mhe. Ali Suleiman Ali somo yangu alilizungumzia. Ukiangalia ukurasa wa 70 Mhe. Mwenyekiti, Mafanikio ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Kuna changamoto ambazo wamezielezea, mafanikio wamezungumza pamoja na changamoto. Changamoto namba (ii) Mhe. Mwenyekiti, wanaelezea:-

(ii) Ukosefu wa majengo ya kudumu kwa Wilaya ya Mjini na Magharibi 'B'.

Mhe. Mwenyekiti, sioni taswira ni kweli tuna changamoto ya Afisi ya Wilaya. Lakini mimi nadhani tusizungumzie wilaya sasa hivi tunakwenda na wakati, tunapotengeneza majengo ya afisi ni vyema hata taasisi zake ndogo ndogo zote ziingie katika eneo moja na lengo letu kwamba tutakapojenga jengo la mkoa maana yake na afisi za wilaya nazo ziingie katika jengo la mkoa lile. Sasa ni masikitiko na wala hatujaelezwa wala hatujui tatizo liko wapi kwa sababu khofu yangu isije kuwa tunaanza kujenga

vibanda vidogo vidogo leo Afisi ya Wilaya ya Amani, Wilaya na Magharibi, sijui Wilaya ya Mjini. Sasa hivi viwilaya wilaya na vijengo vidogo vidogo na ufinyu wa ardhi ya nchi yetu itakuwa ni tatizo.

Tuelezwe basi kamati itushauri sijui kama hawajatembelea au hawalioni lile eneo ambalo lilitengwa kwa ajili ya kujenga jengo la Mkuu wa Mkoa limefikia katika hatua gani na nini dhamira ya serikali katika kulimaliza ili kuondosha hizo changamoto ambazo tumezizowea. Kila siku tukiamka changamoto, changamoto, utekelezaji kesho tunafuatilia tuko mbioni, tunatarajia matumaini ya haraka katika kuisaidia serikali yetu na kupata maendeleo yenye ufanisi wa hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa niiombe kamati wanapotembelea hivi vikosi vya Idara Maalum vikosi vyote kwa jumla, nawaomba sana wasisahau kutembelea vikosi hivi katika maeneo ya sekta ya michezo. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo jengine ambalo linatoa ajira sasa hivi ni eneo la michezo na kwa bahati njema sana idara hii vikosi vyote vina vilabu na kwa bahati zote ziko *premier*. Lakini wakati mwengine zinakosa ufanisi wazitembelee ili tujue matatizo yao, vina mafanikio au vima changamoto. Kama vina changamoto, ni changamoto gani ili tuweze kuvidumisha na viweze kuwa endelevu sana.

Lakini jengine katika vikosi hivi ni changamoto kubwa ambayo tunaiona, vikosi hivi vilabu vyake vinashirikiana kimichezo katika hali nzuri za mashindano ya ndani. Lakini tunapotokezea katika mashindano ya nje ama ya *CAF* au *CECAFA* ama mengine imekuwa tukipata aibu siku hadi siku na tunashangaa kwamba timu ambayo inamilikiwa na serikali kupitia kikosi cha serikali lakini haifanyi vizuri katika masuala ya mchezo tujue tatizo nini. Mhe. Mwenyekiti, kama hawana bajeti basi tuandae fungu maalum kuwawekea bajeti lakini michezo iweze kudumu na iweze kutoa maendeleo na iweze kutoa ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi naunga mkono hoja ya hotuba hii, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Ali Salum Haji, Mnadhim. Sasa ninamwita Mhe. Bahati Khamis Kombo na Mhe. Jaku Hashim Ayoub ajitayarishe.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi ya Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu kwa juhudi zao kubwa walizozichukua kuisimamia ripoti hii na kutuwekea changamoto mbali mbali ambazo ziko mbele yetu na kuweza kuzichangia ili kupewa ufumbuzi wa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende moja kwa moja katika Mkoa wa Kusini Pemba. Mhe. Mwenyekiti, nipo katika ukurasa wa 74, hali halisi ya utekelezaji wa bajeti kwa Mkoa wa Kusini Pemba. Nitakwenda katika kifungu (b) jumla ya vikao 15 vya Kamati ya Usalama vimefanyika na kujadili masuala ya amani na utulivu, udhibiti wa dawa za kulevya, matayarisho ya maadhimisho ya miaka 54 ya Mapinduzi ya Zanzibar, udhalilishaji wa kijinsia na udhibiti wa magendo ya karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba kwa juhudi zake kubwa alizozifanya kupambana na udhalilishaji, kupambana na madawa ya kulevya, lakini pia na magendo ya karafuu kusimamia kwa *lillah taala* ili kuona kwamba katika Mkoa wa Kusini Pemba hayafanyiki. Mhe. Mwenyekiti, ni karibuni tu Mhe. Mkuu wa Mkoa huyu alituahidi katika vikao vyake mbali mbali kwamba atapambana na madawa

ya kulevya lakini pia na udhalilishaji kuona katika Mkoa wa Kusini Pemba haufanyiki.

Nampongeza kwa sababu juzi tu tumesikia katika vyombo vya habari tayari kuna wananchi ambao walitoka Unguja na kupeleka madawa ya kulevya Pemba na mara kufika tu wakaanza kukamatwa na juzi ndio jana wamepelekwa mahkamani. Nimwambie Mkuu wa Mkoa tuko pamoja nae na tutashirikiana nae kwa hali na mali kuona kwamba vitendo hivi ndani ya Mkoa wa Kusini Pemba vimemalizika.

Mhe. Mwenyekiti, nende katika changamoto. Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 75 kuna changamoto ambayo inahatarisha maisha ya wananchi walioko katika kijiji cha Ndagoni. Mhe. Mwenyekiti, niombe sana wizara inayohusika na suala hili basi mgogoro huu wa ardhi usemeke vizuri umalizike kwa haraka ili wananchi wasije kupata matatizo mbele yake. Bora athari iondoke kwa haraka kulikoni mara nyengine tukaja kupata tatizo hili. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika ukurasa wa 76 uchakavu wa majengo katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya. Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme tu kwamba lile jengo kamati walilitazama vibaya, lakini niiambie kamati kwamba jengo lile la Mkuu wa Mkoa linahitaji kujengwa upya liwe jengo la kisasa na lionekane kama kweli lile ni jengo la Mkuu wa Wilaya. Hivi sasa ukilitazama jengo lile ni bora jengo la Baraza la Mji Mkoani liko vizuri kulikoni jengo la Mkuu wa Wilaya ya Kusini Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana hizi changamoto ambazo tunazileta mbele yetu ziangaliwe kwa kina na ziweze kufanyiwa ufumbuzi kwa haraka sana. Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja sehemu inayosema uhaba wa walimu skuli za msingi kutokana na kundi kubwa la walimu wanaostaafu kwa kumaliza muda wao na utumishi wa kisheria. Mhe. Mwenyekiti, suala la

elimu hivi sasa tutasema tunaanguka sana lakini suala linalotuangusha moja ni ukosefu wa walimu.

Ni juzi tu katika Jimbo langu mimi binafsi la Chambani kuna walimu ambao wameshastaafu wengi, Skuli ya Chambani kuna walimu saba, kuna madarasa ishirini na sita, walimu waliokuwepo saba, tumepelekewa walimu watatu itakuwa idadi yao ni kumi. Wakianza kusomesha madarasa kumi ina maana madarasa kumi na sita hayana walimu na wanafunzi wanacheza nje.

Ni moja wapo ya kwamba tunawafanya wanafunzi wale waanze kutoroka skuli na badala yake tunawalaumu kama wanafunzi wanatoroka skuli lakini kumbe mashiko yao yalikuwa ni madogo. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, juu ya suala hili la walimu tufanyiwe juhudi za kutosha kama alivyosema Mhe. Rais wa Zanzibar kuwa walimu waajiriwe, basi tunaomba walimu waajiriwe na wale ambao wanataka kuajiriwa ajira ziwe za shehia husika.

Mhe. Mwenyekiti , nikitoka hapo niende moja kwa moja katika Ofisi ya Baraza la Mji Mkoani. Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza sana Mkurugenzi wa Baraza la Mji Mkoani kwa juhudi zake kubwa anazozichukua kuona kwamba Baraza la Mji Mkoani hivi sasa liko vizuri. Namuomba ndugu yangu huyu aendelee kuwa na mashirikiano mazuri na wafanyakazi wake.

Mhe. Mwenyekiti, pale tuna tatizo kubwa sana la wafanyakazi, hawa ndio wanaodumisha usafi, bila ya wafanyakazi mkurugenzi huyu hataweza kuusafisha mji. Suala hili sio Mkoani peke yake nimeliona hata katika Mji Mkuu wa Chake Chake kule mji ni mkubwa lakini hauna wafanyakazi. Niombe sana wizara ifanye jitihada za makusudi kuona kwamba Mabaraza haya ya Mji yamepatiwa wafanyakazi. Kama ilivyoelezwa katika Baraza la Mji wa Chake Chake kwamba hata wale wafanyakazi wa mkataba wachukuliwe, basi naomba na kule Mkoani na wao waamrishwe

kwamba hata wafanyakazi wa mkataba waweze kuchukuliwa ili mji wetu uweze kukaa safi.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika sekta ya kilimo, ukurasa 85 *marginal note* ya kwanza hapa inasema, jumla ya vikundi saba vya ufugaji wa samaki vimepatiwa majembe na mapauro kwa ajili ya uimarishaji wa mabwawa ya samaki. Mhe. Mwenyekiti, kupelekewa mapauro tu au majembe sio *solution* ya mabwawa haya, hawa wakulima wanahitaji kupewa taaluma ya nguvu jinsi gani ya ufugaji wa samaki, jinsi gani ya kutunza yale matuta ambayo wameyapiga kwa kuhifadhia yale maji. Naomba sana wapewe taaluma kama ni semina au taaluma yoyote lakini vyenginevyo kwa kupewa mapauro tu na majembe hawatoweza kufanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika uhaba wa ukosefu wa walinzi katika vituo vya afya na skuli. Mhe. Mwenyekiti, niombe kwamba ulinzi huu ndio unaofanya hata wale madaktari kukaa katika hali nzuri lakini pia na walimu kuona kwamba zile skuli zinapata ulinzi wa uhakika na wao kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikwambie tu kwamba katika Skuli ya Ukutini kulikosekana amani kutokana na kuwa skuli ile ilikuwa hawana ulinzi. Amani ile ambayo ilikosekana ilisababishwa na baadhi ya vijana, walimu na wazee kutokuwa na mashirikiano mazuri ya skuli ile. Kwa hivyo, naomba sana suala hili la kupatiwa ulinzi basi lisimamiwe kwa kina ili skuli zetu tuone kwamba zote zimepatiwa ulinzi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niendelee kwa kusema kwamba changamoto zote ambazo zimeorodheshwa katika hotuba hii basi zifanyiwe kazi tuone kwamba wizara zetu matatizo haya yamemalizika. Baada ya hayo niseme tu mwisho kwa niaba ya

wananchi wa Jimbo la Chambani naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Bahati Khamis Kombo, sasa ninamwita Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa Jimbo la Paje akifuatiwa na Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma Viti Maalum.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kuniruhusu kuchangia mjadala huu ulioko mbele ya wizara mbili hizi, lakini bila ya kusahau nisije nikafika pahala nikawa sijamfanyia haki Mhe.Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja.

Kwanza nimpongeze kwa uteuzi na kama Mhe. Rais, uteuzi wake ambao ulikuwa hauna mashaka kwa kiasi fulani kwa Mkuu wa Mkoa yule na muda mfupi tu mabadiliko ya Mkoa wa Kusini tumeyaona nimpongeze kwa dhati kabisa. Uzuri wenyewe Mwenyezi Mungu alinijaalia nilifanya nae kazi katika kamati hii niliyokuwa nayo inayoongozwa na Mwenyekiti makini Mhe. Ali Suleiman Ali na nimemuona utendaji wake. Nimpe pole tu Mhe. Waziri Maudline Cyrus Castico kwa kumtoka kijana yule kwenda kwengine nimwambie utendaji wake ndio uliompandisha daraja pale. (*Makofi*)

Lakini vile vile nitakuwa sijamfanyia haki Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Mhe. Ayoub Muhammed Mahmoud kwa kazi anayoifanya na ziara aliyoifanya kuwatembelea wananchi. Vile vile kupunguza vitendo ambavyo sio vizuri haina haja kuvitaja. Kwa hivyo, Mhe. Ayoub Muhammed Mahmoud nikupongeze kwa hilo na ukapita pale usiku unapiga kazi bila ya kujali jua wala mvua tunaona utendaji wako. Sitomfanyia haki Mkuu wangu wa Wilaya ya Kusini Mhe. Idrissa Mussa Kitwana nae nimpongeze.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu utagawika katika sehemu mbili kwa ripoti iliyokuwa kwenye kitabu hichi na mengine itakuwa labda kamati hawakuyaona au haijafika wakati wake pengine majukumu mengi.

Nianze na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Mhe. Mwenyekiti, ofisi hii kidogo ina changamoto na alianza Kitengo cha *AG*. Kitengo cha *AG* kimezungumzwa hapa yaani Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ukurasa wa 19.

"Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar pamoja na sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu (utekelezaji wa majukumu) Nam. 6 ya mwaka 2013. Afisi ina jukumu la kutoa ushauri juu ya masuala ya sheria kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, afisi imetoa ushauri wa kisheria kwa serikali na taasisi zake katika kuthibitisha miongozo na uandaaji wa mikataba na uandishi wa sheria. Miongozo miwili imekamilika ukiwemo muongozo wa mikataba na muongozo wa uandishi wa sheria".

Mhe. Mwenyekiti, nije hapa miongozo imekamilika. Mimi juzi tu sikutaka kuzungumza lakini kama pahala penye makosa Mhe. Mwenyekiti, huu mswaada mliotuletea wa juzi una mapungufu kibao sikutaka kuchafua hali muda huu. Katika mswada kama huu mkubwa uliopita mna vitu karibu 397, kitu cha mwanzo katika mswada *content* ziwemo, mswada huwezi kufungua tu bila ya *content, content* maana yake Kiswahili yaliyomo, humu hayamo.

Kitengo hiki cha Mwanasheria Mkuu na nishasema si mara ya kwanza, si mara ya pili, si mara ya tatu, miswada mikubwa kama hii muandike yaliyomo au *content*. Hii nimesema tena uzuri wenyewe imekamilika ikiwemo miongozo ya mikataba na miongozo ya uandishi wa kisheria na kitengo. Uzuri nyinyi mna kitengo sasa tuseme dharau, au vipi kitengo mnacho. Kitengo cha

uandishi nikishauri kuwa makini. Hiki nakiomba atakapokuja na mikataba mingine huko wajaribu kuandika *content* ziwemo. Nakishauri sana.

Mhe. Mwenyekiti, halafu ikaja katika hapo hapo wanasheria ikalalamika kunako kesi ongezeko la migogoro ya ardhi ukurasa wa 20. Mwanasheria Mkuu waite wizara, waite watendaji, waite Wakurugenzi, michango mingine hii inatokana na watendaji, hii migogoro ya ardhi inatokana na watendaji, waite waeleze hii nazi, hili danzi, hii shokishoki, hili pera, lakini vyenginevyo bila ya mashirikiano utakuwa unalalamika na utaendelea kulalamika. Kesi nyengine zinatatulika, kujiongezea kesi tu na mkienda mahkamani nyengine mnashindwa mnalalamika, ukisema ukapita pembeni ukalalamika.

Utashindwa ziangalie *Court of Appeal* kesi ngapi ulizokwenda nazo ngapi umepata, waite kibinaadam, hata dini yetu ya kiislamu inatuhubiria suluhu ni kitu muhimu mengine yanazungumzika Mhe. Mwanasheria Mkuu na watendaji wako. Lakini ukajiongeza mizigo hii mwisho itakuja kukuumiza fika pahala sema moja moja, mbili mbili…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub zungumza na kiti usizungumze na waziri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimezungumza wapi Mhe. Mwenyekiti, mimi nazungumza na kiti nimemtaja Mwanasheria Mkuu, utendaji wa Mwanasheria Mkuu sio maneno yangu ni kwenye kitabu hiki cha kamati yao. Mwanasheria Mkuu elimu yangu mimi ndogo nasaha zangu migogoro hii waite watendaji wanaohusika uwaambie wizara, mwite waziri mwambie kesi hii tutashinda hatushindwi utafute suluhu. Suluhu kitu muhimu, maneno mazuri ni sadaka, mengine yanazungumzika hakuna lisilozungumzika. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nije katika matatizo mengine ya Mahkama. Mhe. Mwenyekiti, mahkama zina ukosefu wa vitendea kazi vingi na kile kitengo ni muhimu sana cha mahkama ni kimbilio la mnyonge mahkamani. Kitengo cha mahkama ni kimbilio la mnyonge, maana yake mnyonge anaweza kwenda kwa waziri mwezi mzima au mitatu akafanya kazi ya kupanda ngazi na kushuka tu wala hamuoni waziri. Mwananchi yule atataka kumuona waziri wa Zanzibar hapa miezi miwili au mitatu anasikitika hamuoni mwisho hukimbilia mahkamani. Kwa hivyo, kitengo kile ni muhimu na niombe sana viongozi msiingilie, mahkama wacha itende haki yake ndio kimbilio la wanyonge wa nchi hii, ndio haya niliyosema waziri kafunga kioo chake *tinted* humuoni.

Kwa hivyo, kuna changamoto kubwa mahkama zote lakini nimpongeze sana *DPP* Sheikh Ibrahim Mzee Ibrahim kwa kazi anayoifanya kwa ukweli wake, karatasi atakwambia si penseli, penseli atakwambia penseli, *DPP* nimefanya kazi na wewe katika kamati nimekuona katika utendaji wako na mengi yaliyokukuta ustahamili ulezi kazi.

Mhe. Mwenyekiti, uhaba wa vitendea kazi ni suala la muhimu sana. Nije katika Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Hapa nasikitika na hiki kitengo kimeanzishwa si muda mrefu kinahitaji changamoto zake nyingi zitekelezwe. Kwa kweli ofisi yenyewe ndio ile pale moja na chumba chenyewe ndio kile kama kinachozungumzwa humu, uhaba wa vitendea kazi ikiwemo usafiri pamoja na rasilimali watu. Hiki ni kitengo muhimu ingawa ndio mwanzo wa hesabu inaanza moja kuendelea mbele, lakini hiki kitengo kina umuhimu wake changamoto zao zitekelezwe.

Niombe tu Kamati ya Utumishi ikae ifikirie upungufu wa madaktari hivi sasa Kisiwani Pemba. Pemba hivi sasa kuna upungufu wa madaktari wa kila sehemu, kwa hilo utumishi wafikirie sana kuajiri madaktari Pemba ingawa wakifika kule nao

madaktari hawakai Pemba nayo ni changamoto kubwa. Wakifika mtu ataolewa au atatafuta sababu nyengine arudi huku, maana yake tusifike pahala tukapigia kelele serikali tu lakini kuna changamoto hizo. Kwa hili muhimu sana ajira Pemba ya madaktari ipelekwe haraka. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ofisi inayoongozwa na Mhe. Waziri Haji Omar Kheri. Nimpongeze Mkurugenzi wa Manispaa ya Mjini, Bw. Aboud Hassan Serenge muda mfupi tu aliokuwepo pale nidhamu yake inaonekana ya hali ya juu. Kwa kusema kweli mnyonge mnyongeni sijawahi kwenda kuomba kitu kwa bwana Serenge isije ikafikiriwa labda mimi namsifu kwa sababu nimekwenda kuomba kitu kwake aa, nazungumza wazi na mwenyewe aulizwe lakini nidhamu yake mkurugenzi huyu muda mfupi tumeiona. Kwanza sifa yake hadharau simu, akienda kwenye kikao akirudi anauliza nani wala haijui namba na hii ndio sifa ya kiongozi. Ndio yale niliyosema jana Mhe. Rais anasema kiongozi asiwe na kiburi, kwa huyu jamaa mkurugenzi anastahiki lakini ana matatizo yake ndio yale ninayosema ng'ombe wa mbele hataki kwenda anapigwa ng'ombe wa nyuma. Watendaji wake hamfanyi haki.

Katika majukumu yangu nimpongeze sana Mhe. Waziri mimi nilikuwa nimeshatiwa ndani Waheshimiwa Wajumbe kama sio Mhe. Haji Omar Kheri ulikuwa mtihani mkubwa umenikuta. Nilikuwa nimeshatiwa katika lile gereza la manispaa mle ndani, hoja yangu nilikwenda kumtetea mwananchi anauza mikate ya boflo na mvua, mtu na mwanawe anapigwa pingu ni uonevu wa hali gani huo.

Mhe. Mwenyekiti, naweza kuzungumza na ushahidi kuna shati hapa naweza kukuonesha nimechaniwa ni aibu, nilipita chini kwa kumkimbia askari manispaa. Kuna shati hapa la Italy limo kwenye mfuko humu. Mtu na mwanawe anapigwa pingu kwa kuuza mikate ya boflo chini ya kipenu, askari ni aibu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tena nilikwenda na lugha nzuri. Waheshimiwa jamani hebu waachieni hawa mtu na mwanawe hali ni ngumu, wanauza mikate pahala gani, mkate wa boflo unachafua mazingira kweli. Kakaa chini ya kipenu na mvua, nikakamatwa na mimi nikatiwa ndani ya gari kufika kule nikatiwa ndani nikasukumwa huu! twende. Nikamwambia *hewallah*. Uongozi kazi, tumekula viapo kuwatumikia wananchi nikatiwa ndani mimi. Imekuwa kosa kuwatetea wananchi nikawekwa ndani, mikate ya boflo unamuweka mtu ndani tena aibu na mwenyewe kapigwa pingu. Watu wakapapatua, wakasema aa mheshimiwa. Uheshimiwa wake huko huko!

Nikamwambia hata mimi sijali hicho cheo chenyewe, cheo chenyewe nimeazima kwa muda tu hiki kesho hakipo. Wala hanijui mtu kama mimi ni mheshimiwa, mimi nina kidude changu kile cha magurudumu mawili twende tu, haya ya kupita baada uhai kuna mauti, baada ya siasa kuna maisha nje. Lakini leo mtu na mwanawe wanauza mikate ya boflo wanapigwa wanaongozwa wanapelekwa ndani na mimi nikaongozwa nikatiwa ndani, ni aibu shati langu la kileo hili hapa limechanwa. Ni unyonge wa mwisho Mhe. Mwenyekiti. Leo mkate wa boflo unachafua mazingira. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wapeni askari elimu ya kutosha, wale hawana kazi mkate wa boflo senti ishirini tu na senti hamsini ndio faida yake, anachafua nini mazingira. Kweli wengine wanakaa barabarani waondosheni, lakini sio mkate wa boflo, mkate wa boflo ni chakula cha mnyonge kwa chai kavu unachovya unakula, lakini leo tunadhalilishana kwa hili. Kwa hili nipongeze. *(Makofi)*

Mhe. Mhe. Mwenyekiti, kuna changamoto katika soko la Darajani. Nilipiga kelele sana Mhe. Mwenyekiti, pesa zinakusanywa lakini watu wanaandikishwa risiti shilingi 20,000/- wakati wanatoa shilingi 40,000/-. Leo kutokuvaa lile guo jeupe

pale kwenye samaki anaambiwa mchafu, lakini ukienda kutazama ukweli lile soko lenyewe halifai kabisa, yule samaki kwa kuwa ni mtamu tu unamla, lakini soko la Darajani samaki huwezi kumnunua, anabururwa chini hatari, soko linahitaji matengenezo makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, niliwaambia kwamba kama hamuwezi basi yuko mtu muingiane ubia angalau lile soko mlikodishe miaka mingapi, lile bati lake utafikiri *lipstick* linapigwa rangi tu kule juu, mtu anapigwa *lipstick* anaonekana kama bati jipya. Soko lile linahitaji matengenezo makubwa.

Lakini niwaonee huruma hawa watu wa Kisimamajongoo, mwakilishi wao nafikiri hayupo hapa. Hali hairidhishi hata kidogo ya miundombinu ya pale, viongozi sisi hatupiti sana kule, katika barabara ile kuna mtaro wa muda mrefu ni hatari makalbi yake yameshaoza wananchi usiku ni mtihani hakuna taa eneo la Kisimamajongoo. Tufike pahali tuangalie, michirizi ile hairidhishi hata kidogo, usalama wa watoto kucheza mle ni hatari. Najua serikali ina mambo mengi na nilishaahidiwa mara nyingi humu katika kikao itaangaliwa kuna mradi wa *ZUSP* sijui supu, hawajafika pahala. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Magharibi B. Mkurugenzi kama upo huko bwana Amour nisikilize vizuri sasa, kuna tatizo la jaa lililowekwa pale taka zote za soko zinakuja kutupwa pale. Kuna Kitengo cha Wizara ya Afya ni muhimu lile jaa liondoeni linakera watu wengi. Pia katika soko la Mombasa kuna Kitengo cha Afya, wamewekewa pembeni yao pale na kuna watu wana maghala yao ya vyakula. Mpaka leo hakuna hatua na taka zile sio kuwa mnaziondoa, mnapiga wiki au wiki mbili mnapunguza hakuna kinachoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika dogo hili kuhusu ugatuzi. Mhe. Mwenyekiti, ugatuzi bado elimu yake ni ndogo, itafika pahali

elimu muitoe ya kutosha, vyenginevyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Afya mtazitia mtihani katika ugatuzi huu, mfike pahala muwafahamishe wenzetu. Maana yake pengine mtu anaweza kuja kupoteza maisha yake utaambiwa hili ni kesi ya ugatuzi, kumbe ni kesi ya Wizara ya Afya. Mtu anakosa elimu utaambiwa ni suala la ugatuzi, bado elimu ya ugatuzi haijakaa sawa. Kuna migongano hapa kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya na halmashauri hizi, lakini hili muwaelimishe watu vyenginevyo itafika pahala majukumu. Nia ya serikali hii ni kuwatumikia wananchi wala halina mjadala, wala sina mashaka na utendaji wa mawaziri hawa wawili sina mashaka nao, ni mawaziri wazoefu. Lakini ni watendaji nyuma wanafika pahala…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, muda wako umemaliza na nimekupa muda wa ziada. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, sasa namwita Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma Viti Maalum na baadae akifuatiwa na Mhe. Mwanaasha Khamis Juma wa Jimbo la Chukwani ajitayarishe.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Ripoti ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum. Kwanza kabla ya yote naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujaalia mchana huu wa leo kuweza kuipokea na kuijadili ripoti yetu hii.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati, Makamo wake na Wajumbe wote wa kamati kwa kuweza kutuletea taarifa muhimu na nzuri iliyokamilika.

Mhe. Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuweza kumpongeza kwa dhati kabisa Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, nampongeza kwa uteuzi wake mzuri, naamini sana ataweza kutuvusha Mkoa wa

Kusini katika kipindi hiki. Nampongeza na tushirikiane kufanya kazi za Mkoa wa Kusini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye hoja. Kwa kuiangalia ripoti hii mimi naanza kuchangia kwenye Tume ya Utumishi Serikalini. Kwanza nianze kwa kuipongeza sana kwa kufanya kazi yake kubwa ya kuisaidia jamii hususan vijana wa Zanzibar kwenye masuala mazima ya kupata ajira. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya malalamiko kwa vijana hawa. Kuna vijana wamefanyiwa usaili yaani *interview* tangu mwaka jana, lakini mpaka sasa majibu yao bado hayajatolewa na hatujui tatizo hili au shida hii iko wapi. Kwa hivyo, niiombe sana wizara itakapokuja hapa ituambie na itufahamishe kwamba kuna jambo gani na kuna utata gani mpaka leo vijana wale hawajaweza kutolewa majibu ya ufasaha.

Mhe. Mwenyekiti, tume hii inakabiliwa na changamoto na miongoni mwa changamoto ambazo wametuelezea ni kukosa nafasi za uhifadhi wa nyaraka, tukijua kwamba nyaraka ni kitu muhimu sana na kwa umuhimu wake basi tuone, tupate nafasi na sehemu nzuri ya kuweza kuzihifadhi, ili tutakapotaka kuona jambo au kutafuta *reference* tupate kwa usahihi zaidi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri kwa kupitia hili nakuomba sana uangalie na utafute namna ya kuweza kupata nafasi nzuri, ili kuona nyaraka hizi zinahifadhika vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda kwenye Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, yaani *ZAECA*. Mhe. Mwenyekiti, nayo pia niishukuru kwa dhati kabisa kwa kazi ambayo wanaifanya, nikiamini kwamba wanatekeleza majukumu yao ipasavyo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika taarifa yetu hii tukiangalia tunaambiwa kwamba kuna kesi nne kutoka Pemba zinazohusiana na kesi za rushwa na uhujumu uchumi. Mimi nataka kuuliza sana kwamba tunaona na tunatambua rushwa ni

adui wa haki, lakini katika sehemu za utendaji rushwa imetawala sana, lakini kwenye ripoti hii tunaambiwa kuna kesi nne. Sasa sijui mamlaka hii inafanyakazi wakati wa kipindi cha kampeni tu na kipindi cha siasa tu, au inafanyakazi katika sekta zote. Kwa sababu tunaona sana katika kipindi ambacho kesi za rushwa zinatawala sana basi ni kipindi cha uchaguzi, hizi siku nyengine tunataka kujua. Je, taasisi hii inashughulika na nini na kitu gani ambacho wanakifanya.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naomba niende kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Niungane na Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa kusema kwamba Ofisi ya *DPP* inafanyakazi kubwa sana na kazi nzito sana, lakini kuna changamoto ambazo wanakabiliana nazo na changamoto hizi ni mbaya sana. Ofisi kama hii Mhe. Mwenyekiti, inakabiliwa na kutoingiziwa fedha kwa wakati, hili ni tatizo kubwa sana, tukiamini kwamba kitengo hiki ni kitengo nyeti sana kwetu, wanyonge wengi sana wanalilia hapa, wenye vilio wengi sana na wenye kudhulumiwa na kufanyaje wanakwenda hapa, lakini tatizo hili bado wanalo.

Kwa hivyo, tuiombe sana wizara na tuiombe sana serikali kwa umuhimu wa kitengo hiki, tuombe na tupendekeze sana kwamba fedha zitolewe kwa wakati husika, ili waweze kufanyakazi zao kwa ufanisi, vyenginevyo tutakuwa tunawazorotesha wao katika ufanyaji wao wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, watu hawa hawana vyombo vya usafiri changamoto hii nayo ni kubwa sana, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka leo hii haina usafiri hili ni tatizo na tatizo hili litawazorotesha wao kufanyakazi zao. Haiwezekani kwamba wanatakiwa wafike *site* halafu wanakosa usafiri, maana kisingizio kikubwa hapa watakuja kusema kwamba hawana usafiri. Kwa hivyo, mimi niiombe sana serikali na niiombe sana wizara iwashughulikie ili kuona Ofisi hii ya Mkurugenzi wa Mashtaka nayo inafanyakazi zake vizuri kama tunavyoona.

Mhe. Mwenyekiti, niongelee kwenye kesi ya Chuo cha Utawala wa Umma. Kwa dhati kabisa niipongeze serikali, lakini niipongeze wizara kwa kuweza kuanzisha chuo hiki ili kuwasaidia watumishi wake wa serikali. Pia niipongeze wizara kwa kuweza kuanzisha kada ya digrii katika Chuo cha Utawala wa Umma. Hii inaonesha kwamba sasa hivi tumeona umuhimu wa kwamba wafanyakazi wetu wachukue elimu ya ngazi ya juu ili kuona ufanisi unatekelezeka vizuri katika maeneo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika changamoto ambazo tumeziongelea hapa ni changamoto kutoka Pemba tu, hatujaangalia katika chuo ambacho nyinyi wenyewe mmeanzisha hii kada ya digrii iliopo Tunguu. Sasa nilitaka kujua na nataka kufahamishwa kwamba katika huu uongozi au katika hii *system* ya kuanzisha digrii hakuna changamoto yoyote ambayo mmeikuta, au tumehisi hii ndio inaumiza sana vichwa kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Idara Maalum za SMZ. Mhe. Mwenyekiti, kwa dhati kabisa nichukue nafasi hii kuishukuru serikali kwa kupitia wizara hii vikosi vyetu vinafanyakazi kubwa na nzuri inayoonekana. Mhe. Mwenyekiti, kuna changamoto nyingi sana zimeoneshwa kwa sababu wafanyakazi hawa ndio tunaoshughulika nao kwenye jamii yetu. Mimi niombe sana wizara kwa kupitia idara hii iwaangalie sana ndugu zetu, watumishi wetu na hasa hawa watumishi wa vikosi vya SMZ, ikiwemo JKU, Zimamoto na hata Askari Magereza, tuwaboreshee maslahi na tuyaangalie mazingira ambayo wanafanyia kazi. Kuna wenzetu ambao wanatoka hapa wanakwenda kufanyakazi Pemba, tuwaandalie sana mazingira rafiki ili wakitoka hapa wakienda kule waweze kuya-*tune* maisha yao kwenda sambamba na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe. Sasa namwita Mhe. Mwanaasha Khamis Juma wa Jimbo la Chukwani, akifuatiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali wa Jimbo la Ziwani Pemba.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia machache niliyonayo katika ripoti ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze kamati kwa dhati kabisa kwa kutuletea ripoti hii ambayo wao wameitayarisha na ina nia ya kujenga kwa serikali yetu ambayo inatuongoza nchini hapa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nipongeze sana wizara zote mbili zinazohusika kwa jitihada zao mbali ambali ambazo wanazifanya katika kutekeleza majukumu yao. Moja kwa moja nije katika ripoti yetu, kwanza kabisa nitaingia katika taasisi zinazojitegemea ambazo zinasimamiwa na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, napenda sana nipongeze wizara hii au taasisi hii kwa juzi tu kutuletea mswada muhimu sana wa Sheria ya Makosa ya Jinai na Sheria ya Kufuta Sheria za Adhabu ambazo sheria hizi kwa muda mrefu zilikuwa zimepitwa na wakati, na juzi kwa jitihada zao wakiungana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wametuletea miswada hii na tunawashukuru sana, nina imani sheria zile zitafanyiwa kazi kwa umakini sana.
Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nataka nije katika Idara Maalum ya Vikosi vya SMZ. Mhe. Mwenyekiti, kwa dhati kabisa nimpongeze Mhe. Waziri wa wizara hii kwa umahiri wake na kwa umakini katika utendaji wa kazi, licha ya changamoto ambazo zinaikabili wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nakuja moja kwa moja katika Mamlaka ya Serikali za Mikoa. Mhe. Mwenyekiti, pia

nichukue nafasi hii kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi hapa, kwa kazi zake za ufanisi katika kuuletea mji huu maendeleo, amani na utulivu akiwa yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Mambo mengi ambayo anayafanya tumeyaona na nadhani tayari amani, utulivu na usalama ndani ya Mkoa wa Mjini Magharibi basi upo.

Mhe. Mwenyekiti, katika majukumu ya Mkoa wa Mjini Magharibi nipongeze tu mbali ya mafanikio ambayo kamati imetuonesha, lakini kuna changamoto ambazo wameziona kama kamati na wametuletea katika ripoti, ili serikali iweze kuzipatia ufumbuzi changamoto hizi.

Mhe. Mwenyekiti, katika changamoto hizo mimi nitaigusia changamoto ya nne ambayo imesema kwamba kuna uharibifu wa mazingira, ikiwemo vyanzo vya maji na uchimbaji wa mchanga usiofuata utaratibu uliowekwa.

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza kamati, lakini niwaambie tu pamoja na wizara na Mhe. Waziri, sio hii tu ambayo ni changamoto inayokabili katika masuala mazima ya mazingira. Mhe. Mwenyekiti, kuna maeneo ambayo yalikuwa yanachimbwa vifusi katika maeneo ya jimboni kwangu Shakani, maeneo yale karibu na viwanja vya ndege. Mheshimiwa pale pana uharibifu mkubwa wa mazingira na matokeo yake sasa hivi katika eneo lile tayari litahatarisha maisha ya wananchi wale. Kwa hivyo, hii ni changamoto, nawaomba sana wizara husika wafanye ziara ya makusudi ili wakaone ule mmong'onyoko na athari iliyotokea pale, ili waipatie ufumbuzi changamoto ile ni hatari kweli kweli na sasa hivi lile shimo linakaribia kufika njiani ambapo njia ile inatumika na wananchi wa maeneo yale.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende moja kwa moja katika idara hiyo hiyo, nije katika changamoto au katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka za Serikali za Mitaa ipo

kisheria, na sheria hiyo tuliipitisha hapa nakumbuka na najua ilipitishwa katika Baraza la Wawakilishi, ni sheria namba 7 ya mwaka 2014.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii imeainisha mambo mbali mbali yanayohusu Tawala za Mikoa, Mamlaka na Serikali za Mitaa. Mhe. Mwenyekiti, niombe wizara husika watoe mafunzo kwa watendaji ili waweze kujua sheria kikamilifu na waweze kufanya kazi zao kwa umakini sana, wanafanyakazi vizuri wakiwemo Madiwani tunawashukuru sana, Wakurugenzi wa Halmashauri.

Mhe. Mwenyekiti, nitoe pongezi za dhati kabisa katika Halmashauri ya Mkoa wa Magharibi, Mkurugenzi wa Manispaa nimpongeze sana, Mkurugenzi yule kwa umahiri wake na kazi zake mimi mwenyewe shuhuda baada ya kilio cha wananchi wa Jimbo la Chukwani. Siku nyingi sana nililalamika humo kuhusiana na barabara lakini baada ya kuona vile tukaenda katika Halmashauri. Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa ile kazi inafanyika sana sasa na mimi mwenyewe nimepongeza, hivyo nipongeze katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini katika maelezo hapa tumesema katika mnasaba ili kufikia malengo ya Dira ya 2020. Mhe. Mwenyekiti, niombe serikali katika suala zima la ugatuzi na katika wizara hii ifanye kwa makusudi mazima waongeze bajeti katika wizara hii. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, baada ya ugatuzi tumeona mambo mengi yanafanyika kwa urahisi na ndio lengo lile la ugatuzi nipongeze. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, katika Kamati yangu ya Ustawi wa Jamii tumetembelea katika maeneo ya Elimu na Afya, kule tayari kuna mambo ambayo hapo kabla ya ugatuzi yalikuwa hayafanyiki, lakini sasa hivi yanafanyika na yanakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali kupitia wizara hii basi waongeze bajeti ili kurahisisha yale mambo yanayowagusa

wananchi yafanyike kwa usahihi na kwa mara moja kwa lengo tu la Dira ya 2020 kwa kuwaletea maendeleo ya haraka wananchi katika maeneo ambayo yametuzunguka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ripoti imegusa kila kitu lakini na mimi nahisi nilikuwa nichangie haya machache. Lakini pia namuomba Mhe. Waziri kupitia Mkoa au Halmashauri basi ile barabara ya Chukwani ambayo ilitolewa ahadi na Rais wa Awamu iliyopita, kwa vile sasa hivi tumeshaanza kwa kiwango cha fusi, basi ajitahidi Mhe. Waziri twende tukatimize ahadi kabla ya bajeti au baada ya bajeti. Katika mpango wake kazi katika bajeti basi na suala lile aliingize kwa vile ni ahadi ya Rais twende tukaitie barabara ile lami wananchi nao wafaidike na wajenge matumaini katika serikali yao.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niungane na wenzangu kwa kuunga mkono ripoti hii asilimi mia na naomba zile changamoto ambazo zimo katika ripoti hii, basi serikali itapofika Septemba watuletee majibu mazuri. Wanayoweza kuyafanyia kazi waanze leo kuyafanyia kazi hasa kwa lile agizo la Rais la utiaji wa lami barabara ya Chukwani. Ahsante nakushukuru Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsane sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia ripoti hii ya Kamati. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niwapongeze wizara zote hizi mbili ambazo zina changamoto kubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, nasema hilo kwa sababu ni shahidi ni Mjumbe wa Kamati hii katika wizara ambazo zina changamoto usafiri, zina changamoto ya vifaa vya kutendea kazi vyengine kama kompyuta na mambo mengine, pamoja na majengo. Ni Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumisi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Mhe. Mwenyekiti, hizi wizara

ni kubwa zina mambo mengi, kwa vile changamoto zinakuwa ni kubwa sana.

Lakini pia nimpongeze sana *DPP* kwa kazi kubwa anayoifanya, kazi ngumu lakini kwa ujasiri wake na umahiri wake kuhakikisha kwamba nchi inakwenda vizuri. Kwa sababu yeye ni kila kitu hususan kwa wanchi wanyonge ambao wanakimbilia kufuatilia masuala ya kesi zao, nampongeza sana na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atampa nguvu ili kuweza kufanya kazi zake. *(Makofi)*

Mhe. Mweyekiti, nikitoka hapo niende ukurasa wa 59 Idara Maalum. Mhe. Mwenyekiti, Idara Maalum inajumlisha vikosi vyote. Mhe. Mwenyekiti, kuna jambo la kusikitisha kwa sababu vikosi hivi vimeundwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein ndio aliyeunda vikosi hivi. Mhe. Mwenyekiti, vikosi vina wajibu wa kushirikiana na Jeshi la Polisi na vyombo vyengine vya ulinzi na usalama ili kuhakikisha kwamba amani inapatikana Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Mhe. Mwenyekiti, lakini cha kushangaza kuna polisi wanawadharau, wanawakejeli vikosi vyote vya Zanzibar, hufika baadhi ya wakati mwengine mpaka kuwatolea maneno humo mabarabarani. Kusema kweli si jambo zuri hata kidogo kufanya hivyo kwa sababu vikosi vipo kwa mujibu wa Sheria na Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, niende ukurasa wa 66 Ofisi ya Vizazi na Vifo na Kadi za Vitambulisho. Mhe. Mwenyekiti, katika maoni ya Kamati imesema kwamba inashauri ofisi kwa kijana aliyeko Pemba. Kule Pemba Mhe. Mwenyekiti, kuna kijana anajitolea huu ni mwaka wa 11, Kamati imeandika miaka 11, lakini zaidi yule kijana ameshakuwa mzoefu hadi leo hii anaendelea kujitolea katika Ofisi ya Vizazi na Vifo pale Chake Chake.

Mhe. Mwenyekiti, naishauri sana wizara kuhakikisha kwamba wamfanyie angalau ajira yule kijana nae kwa sababu ameshatumikia sana ili waweze kumuajiri na ameshakuwa mzoefu ili aweze kutoa huduma kwa jamii inayokwenda pale.

Mhe. Mwenyekiti, niingie katika Mkoa wa Kusini Pemba. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kutuchagulia Mkuu wa Mkoa jembe, mahiri, shupavu, makini, Mhe. Hemed Suleiman Abdalla. Tuna imani kwamba badala ya Mhe. Ayoub Mohammed Mahmoud hapa Unguja Mjini atakuwa Mhe. Hemed Suleiman Abdalla kwa kule Kusini Pemba yuko vizuri sana kwa kuchapa kazi na sie tupo bega kwa bega nae. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo niende katika mgogoro wa ardhi ulioko Ndagoni. Mhe. Mwenyekiti, kama ni mashahidi kwa tunaofuatilia katika vipindi vya taarifa ya habari na sehemu nyengine tunaona migogoro ya ardhi, hususan kule Tanzania Bara kama Morogoro na Dodoma watu wanauwana.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilikwenda Ndagoni ikashuhudia huu mgogoro wa ardhi lakini kuna baadhi ya viongozi walijihusisha pale kwa namna moja au nyengine. Mhe. Mwenyekiti, nina imani na kamati ilivyoshauri Mkuu wa Mkoa kwamba kulihakikisha suala lile limemalizika, nina imani kwamba suala kwa Mkuu wa Mkoa aliyeko Kusini Pemba basi litamalizika haraka sana ipasavyo. Lakini pia naishauri Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kuhakikisha yale maeneo ya serikali yote yapimwe ili kuondoa migogoro hii, kwa sababu maeneo yale yakipimwa kila mwananchi akenda pale atakuwa anakwenda tu kufanya ule ukaidi wake, lakini serikali iweze kuyatambua yale maeneo ili kuondoa hii migogoro iliyokuwa haina ulazima.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wanafika kutaka kuuwana eneo lile la serikali na maeneo mengine. Kwa hivyo, naishauri sana serikali Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, pamoja na wizara zote kuhakikisha kwamba maeneo ambayo ni ya serikali yapo wazi yapimwe ili kuondosha usumbufu huu wale wananchi wasije wakauwana. Sio kule Pemba na hata hapa Unguja kwa sababu ardhi imekuwa ni mali sana. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba sana serikali kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Kikosi cha Zimamoto na Uokozi pale *Airport.* Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba kikao kilichopita tulileta ripoti kama hii hapa. *Airport* pale Zimamoto wana tatizo kubwa la maji. Mhe. Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege uliopo hapa Unguja mzuri mkubwa na nafasi unayo lakini cha kushangaza maji hapana upande huu wa Kusini. Uwanja wa Ndege unategemea na ndege inavyokuja na upepo unavyovuma, siku nyengine ndege inarukia Kusini, siku nyengine inarukia Kaskazini.

Mhe. Mwenyekiti, ni tatizo hata ikibidi kwamba maji hapana Mwenyezi Mungu atuepushe mbali, lakini likitokezea tatizo ndege kuja kuripuka maji hamna, hata yakitoka kule yakifika watu wameshakufa na athari kubwa itapatikana. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa mara ya pili kuhakikisha kwamba kile kisima tayari kipo wawafikishie umeme kwa sababu wanawapa kazi kubwa. Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo) alisema na miundo mbinu ya barabara.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasisitiza tena kwa mara ya pili kwa sababu tulisema ndani ya kamati na sasa hivi tunasema tena. Tunaomba sana kwa vile ni agizo la Rais, masuala haya ya kupuuza puuza maagizo ya Rais yanarudisha nyuma kwamba mpaka Rais anasema lakini agizo halitekelezwi wewe Mwakilishi itakuwaje. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kila siku husema kwamba

haya yote yanatokana kuna watu hawaitaki hii Ilani ya Chama cha Mapinduzi, maana Rais ndio kila kitu anapoahidi ni kwamba kile kitu kifanywe, hata kama hakitofanywa kwa wakati ule lakini isifike mwaka kile kitu kifanywe. Eeee, basi hiyo nguzo ya umeme Mhe. Mwenyekiti, ina gharama kiasi gani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana mamlaka inayohusika kuhakikisha kwamba wamewapelekea umeme pale ili yale maji yapatikane. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia Ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niwapongeze sana Wajumbe wa Kamati hii kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ndani ya muda wote ambao waliopangiwa kufanya kazi zao katika maeneo husika.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati hii imefanyakazi usiku na mchana na kutafuta zile changamoto ambazo zipo katika Taasisi mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, pia niwapongeze sana Mawaziri wote wawili pamoja na watendaji wao wote kwa kazi ambazo wanazifanya za kila siku. Mhe. Mwenyekiti, pia nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Vuai Mwinyi kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, lakini pia niwapongeze ma-*DC* wote wa Wilaya ya Kaskazini 'A' na Kaskazini 'B' Unguja, Wakurugenzi wa Halmashauri hizi pamoja na Masheha wote. Kwani kama si wao kazi hizi haziwezi zikafanyika, lakini pia wapo na wenzao ambao ni Wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa pamoja na Wilaya. Mhe. Mwenyekiti, viongozi hawa kwa kushirikiana na Uongozi wa Chama pamoja na Serikali wanafanyakazi kubwa za kuratibu shughuli nzima za ndani ya Wilaya na Mikoa yao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kamati wametembelea katika mikoa hii na wilaya zote na wameona baadhi ya changamoto. Lakini nije moja kwa moja kwenye ukurasa wa 29 ambao unazungumzia masuala mazima ya Mahkama, mimi nije kwenye Mahkama ya Wilaya Mkokotoni. Mhe. Mwenyekiti, kamati imeona changamoato hapa mbali mbali ambazo zimo katika Mahkama ya Wilaya Mkokotoni lakini mimi nitazungumzia changamoto nne:

Moja, kuna ukosefu wa vitendea kazi na vifaa mbali mbali kama vile; magari, viti, meza, makabati na kadhalika. Mhe. Mwenyekiti, ipo haja sasa kuangalia sana na kuwatafutia nyenzo za kufanya kazi katika Mahkama hizi za Wilaya ikiwemo Mahkama ya Mkokotoni.

Mbili, Mhe. Mwenyekiti, pia nimeona changamoto ambayo inaelezewa kwamba kuchelewa kukamilika kwa ushahidi ambako kunapelekea kufutwa kwa kesi nyingi. Mhe. Mwenyekiti, changamoto hii ipo katika Mahkama nyingi za Zanzibar, Unguja na Pemba. Hii inasababisha kwamba unachelewa huu ushahidi kutokana na mambo mbali mbali. Kwa hivyo, naomba wizara husika ambao wanaoshughulikia ofisi hizi basi wakae pamoja na kuhakikisha kwamba ni sababu gani ambazo zinapelekea kuchelewa kukamilika kwa ushahidi na baadae kupatiwa ufafanuzi.

Tatu, Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo jengine ambalo linasema kwamba kukimbia kwa watuhumiwa kwenye kesi zao ambazo zinasababisha kuchelewa kukamilika kwa ushahidi. Naomba wizara husika iende kwenye mahkama husika ikatafute ni sababu gani ambazo hawa watuhumiwa wamekimbia na wako wapi, ili wanashindwa kwenye kesi zao kufuatilia mwenendo mzima wa kesi.

Nne, kupitia kwenye suala zima la mahkama kuna kuomba kuakhirishwa kwa kesi za udhalilishaji mara kwa mara kamati imeona changamoto hii. Lakini pia nilitaka kujua kwamba huyu anayeomba kuakhirishwa kwa kesi hizi za udhalilishaji mara kwa mara ni nani ambaye anafanya kazi hii, yaani kutaka kuomba kesi hizi ziakhirishwe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 73 kuna changamoto ndani ya mkoa wetu wa Kaskazini Unguja, changamoto hizi zipo 10 lakini mimi nitazungumzia baadhi ya changamoto.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeona kwamba hakuna ulinzi wa uhakika katika maeneo ya utalii. Sote tunafahamu kwamba utalii ndio unaotuletea pato kubwa hapa Zanzibar. Lakini Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja ikiongozwa na mwenyewe Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja anajitahidi sana katika kuhakikisha suala zima la ulinzi na usalama katika maeneo yote ya utalii. Lakini naomba wizara husika kupitia Vikosi vya SMZ basi ishirikiane nae kuhakikisha kwamba maeneo ya utalii yanapatiwa ulinzi wa uhakika ili watalii wetu waweze kukaa bila matatizo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala zima la maji safi Mkoa wa Kaskazini Unguja. Sote ni mashahidi tatizo la maji liko Zanzibar nzima, lakini hebu basi! Serikali kwa ujumla tukae kwa pamoja tutafute mbinu kama tulivyotafuta mbinu za kuhakikisha kutokomeza suala zima malaria Zanzibar. Sasa hivi suala la maji limekuwa tatizo kila siku kwenye Mawiyo mpaka hii leo wengine tena tumechoka. Viongozi, Wawakilishi na Wabunge pamoja na Madiwani, ukisikia tatizo la maji basi tunafuatwa sisi viongozi, kuna matatizo ambayo sisi viongozi tunaweza kuyatatua yapo ndani ya uwezo wetu, lakini kuna matatizo ambayo yapo nje ya uwezo wetu. Naomba sana Mamlaka ya Maji Zanzibar *(ZAWA)* ikae pamoja na viongozi wa mikoa yote tukishirikiana nasi ili

kuhakikisha kwamba maji safi na salama yanapatikana katika maeneo husika.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye miundo mbinu ya barabara katika Mkoa wa Kaskazini barabara ambayo inatokea Bububu mpaka Mkokotoni hali halisi mnaiona. Mhe. Mwenyekiti, kila siku ajali zinatokezea lakini pia athari zinatokea nyingi sana. Tunaomba sana serikali ichukue juhudi za kuhakikisha kwamba ule Mradi wa Barabara ya Bububu - Mkokotoni basi ianze kwa muda muafaka. Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna barabara za ndani. Katika Mkoa wa Kaskazini vijiji vingi kwa kweli tatizo ni barabara za ndani, wananchi wengi wakiwemo wanawake wanapata shida sana kuvifikia vituo vya afya kutokana na tatizo la barabara. Naomba sana Halmashauri za Wilaya za Kaskazini 'A' na 'B' kupitia wizara husika pamoja na sisi viongozi tutashirikiana kwa pamoja kuhakikisha tunafanyia kazi, tunakarabati njia hizo japo angalau kwa njia ya kifusi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna changamoto ya Mkoa wa Kaskazini kamati imeona kuongezeka na kushamiri kwa vitendo vya udhalilishaji, hili suala kweli lipo na sote mashahidi lakini naomba sana mwaka jana 2017/2018 katika bajeti Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tulipigania kifungu kiongezwe kupitia Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Kifungu kile kwa ajili ya kuhakikisha kwamba suala zima la udhalilishaji wa wanawake na watoto linapatiwa ufumbbuzi, tulipitisha fedha zile kwa ajili ya kufanyia kazi masuala haya. Ni hivi juzi tu hapa kumeanzishwa jumuiya ya kupinga vitendo vya udhalilishaji ambayo ofisi yao iko Mbuzini. Naomba sana Serikali kwa kushirikiana kupitia Wizara ya Uwezeshaji iungane nao ili kuhakikisha kwamba inawapa fedha kwa ajili ya kupita kuhamisha zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho katika changamoto kubwa katika wizara zote, katika taasisi zote kuna ukosefu wa fedha na vitendea

kazi. Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo na kila unapopagusa unakuta kwamba bajeti ni ndogo kwa hivyo hawakuweza kufikia malengo yao.

Mhe. Mwenyekiti, naamini kwamba hizi changamoto ambazo walizoziona wajumbe wa kamati hii zitafanyiwa kazi na wizara husika na baadae changamoto hizi zitaondoka. Kwa haya machache Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana naunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe. Waheshimiwa Wajumbe niwaombe kitu kimoja wakati wa kuchangia ripoti zetu tusitoke nje ya mada kama tulivyoripotiwa. Kuna mambo tunayazungumza hayamo ndani ya ripoti mama, kwa hivyo tuangalie sana katika kuchangia kwetu twende ndani ya ripoti zetu kwa yeyote yule ajichunge katika kwenda ndani ya ripoti. Baada ya hayo namwita Mhe. Masoud Abrahman Masoud na baadae atafuatiwa na Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi wa Mtopepo.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba au ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi niwapongeze Mawaziri wote wawili kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, lakini pia niwapongeze Mwenyekiti pamoja na Kamati yake kwa ufuatiliaji mzuri ambao wameuonesha katika taarifa yao hii.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mkuu wangu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, jana tulisema kwa kazi nzuri ambayo anaifanya kwa suala zima la uondoshaji wa madawa ya kulevya, lakini pia na mambo mengine ambayo katika jamii hayakubaliki.

Mhe. Mwenyekiti, leo nimpongeze sana Mhe. Mkuu wa Wilaya wangu wa Magharibi 'A' kwa kazi nzuri nae anayoifanya kwa sasa hivi, ndani ya wilaya yetu kulikuwa na matatizo ya madawa ya kulevya sasa hivi yamepungua kwa asilimia kubwa. Lakini pia kuna migogoro mikubwa ya ardhi muda wote yeye anafanya kazi kama alivyokuwa huko uaskarini, usiku na mchana anafanya kazi kwa hiyo nampongeza sana kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja na mimi niende kwenye mchango wangu kuhusu suala la miundo mbinu ya barabara zilizoko ndani ya Manispaa yetu na Halmashauri. Mhe. Mwenyekiti, ndani ya maeneo yetu au ndani ya majimbo yetu na hasa Wilaya ya Magharibi sasa hivi ni maeneo ya mji na kuna barabara nyingi za ndani na tunategemea sana viongozi wetu au Watendaji wa Halmashauri waweze kutusaidia, lakini na wao bajeti yao haiwaruhusu kujenga hizo barabara. Niombe Mfuko wa Barabara wahimizwe nao ili waweze kutusaidia hizo fedha kuingizwa ndani ya Halmashauri zetu, wapate kutekeleza angalau kutujengea barabara za ndani japo mbili tatu katika Halmashauri ya Manispaa ya Magharibi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo kuna suala zima la ajira na kuna wafanyakazi wengi sana wa muda ambao ndani ya Manispaa ya Magharibi 'B' na Magharibi 'A' hawapungui mia tatu au mia nne waliokuwa na ajira hizi za muda. Mhe. Mwenyekiti, wengine wana zaidi ya miaka kumi na tano wanafanyakazi ya muda, sasa hivi wengine uzee ushaanza kuwatembelea. Niombe sana kwa kupitia Tume ya Utumishi watu hawa waangaliwe kwa jicho la huruma waweze kuwaajiri kwa wale waliokuwa na uwezo wa kuajiriwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala hilo hilo la ajira Halmashauri zetu au Manispaa zetu zote mbili sasa hivi zimekuwa na ugatuzi kwa hiyo wana majukumu makubwa ya kufanya. Lakini kwa bahati mbaya sana Mhe. Mwenyekiti, ndani ya Manispaa ya

Magharibi 'A' hata Afisa Mipango wa ile manispaa hakuna. Niiombe serikali itutafutie Afisa Mipango wa Manispaa wa Magharibi 'A' awepo kwa sababu yeye ndio mtendaji ambaye atamsaidia mkurugenzi katika kufanya kazi za kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo kwenye Halmashauri zetu tunahimizwa suala kubwa la usafi, niwapongeze sana Wakurugenzi wangu wote wawili wa Manispaa ya Magharibi 'A' na 'B' kwa jinsi wanavyohangaika na magari mabovu kila siku kuhakikisha wanasafisha maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, ndani ya Manispaa ya Magharibi 'B' kuna ki-*carry* ambacho kinazoa taka ambacho nafasi yake ni ndogo sana ya kuweka taka lakini kila asubuhi utawakuta wafanyakazi wapo barabara ya Amani, wako barabara ya Bububu wanasafisha, niwapongeze sana kwa hilo. Mji wetu uko vizuri lakini bado niwaombee Tume ya Utumishi au Serikali Kuu Halmashauri hizi zifanyiwe fungu la huruma angalau kupatiwa gari za kuzolea taka ili mji wetu upate kukaa sawa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii nimpongeze Kamanda wa JKU kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya, kwa sababu sasa hivi katika mji wetu wa Unguja hasa mjini hata kama uwezo wako mdogo na wewe utakula tikiti lililotoka Bambi. Ni kazi nzuri ambayo wenzetu wanaifanya lakini nimuombe tu Mhe.Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi awe nao karibu sana ili kuwapa wataalam waendelee kuwasidia wafanye vizuri. Lakini pia nimuombe Mhe. Waziri anapopata miradi ambayo labda itakuwa na fedha ya kusaidia kwenye masuala ya umwagiliaji wawasaidie vijana wote wale wa JKU ili wapate kuzalisha zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, tukitoka hapo mimi bahati nzuri kwenye jimbo langu kuna hospitali mbili, hospitali ya KMKM na hospitali ya JWTZ. Niwapongeze sana madaktari wa maeneo yale lakini pia niwapongeze na wakuu wa kambi, wananchi wetu katika

maeneo yale hata ikiwa saa saba za usiku umepata tatizo la kuumwa ukienda kwenye kambi zile unapata huduma, tuwapongeze sana kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeona kama kuna changamoto za madawa, bahati nzuri au bahati mbaya wenzetu kambi zote mbili hawapati mgao wa dawa kutoka Serikali Kuu, niiombe serikali wananchi wa maeneo yale wanayozunguka ni wapiga kura wetu na wao wana haki sawa na wananchi wengine, kwa hivyo mgao wa dawa unapotoka hospitali ya KMKM wapate. Lakini pia hospitali ya JWTZ Bububu na wao wapate ili kuwasaidia wananchi wetu walio katika maeneo yale.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nilitaka niwapongeze Ofisi ya Mwendesha Mashtaka. Kwa kweli Zanzibar kulikuwa na ongezeko kubwa la mirundikano ya kesi ndani ya mahkama zetu lakini kwa sasa kidogo imepungua, kwa hiyo tuwapongeze sana kwa hilo. Lakini kuna changamoto ambayo si nzuri kwa waliokuwa hawajui sheria, kwa anayejua sheria atapambana nayo lakini aliyekuwa hajui kidogo imekuwa changamoto. Kuna wananchi wanapata tabu wanaweza wakawekwa kituo cha polisi ndani ya miezi mitatu yumo ndani ya kituo kesi haijenda hajapelekwa popote yeye yumo ndani ya kituo. Kwa wale wanaojua sheria naamini hakuna sheria ya kumuweka mtu ndani ya kituo cha polisi miezi mitatu bila ya kumfungulia mashtaka. Lakini kwa yule aliyekuwa hajui sheria watu wamekaa kwa muda wa miezi mitatu na nusu wapo ndani ya kituo cha polisi hakuna kinachoendelea.

Baada ya kikao kilichopita nilisemea hapa siku ya pili wakatolewa kituo cha polisi wakapelekwa Kiinua Miguu. Kwa hivyo, nimuombe tu Mkurugenzi wa Mashtaka watu wanapowakamata baada ya polisi kumaliza upelelezi wao basi kesi ziende ili watu wasipate usumbufu mkubwa.

Mhe. Mwenyekit, jengine ambalo nilitaka nilisemee ni suala zima la ugatuzi. Niipongeze sana serikali kwa maeneo yetu matatu ya Kilimo, Elimu pamoja na Afya kwa ugatuzi, lakini niwapongeze sana Wizara ya Afya wao wanaonekana wamekubali mwanzo kuliko Wizara nyengine zote kuukubali ugatuzi. Kwa sababu sasa hivi ukienda baadhi ya vituo wakurugenzi wanasaidia mpaka kununua dawa, kukarabati majengo ya hospitali, kununua baadhi ya vifaa ambavyo ndani ya hospitali vitu ni vipungufu. Niiombe na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi nao wakubali kuwa hili jukumu ni la kwao na sasa hivi wao ndio wanaanzisha hilo zoezi walifanye kwa vizuri ili serikali ipate kuzifanyia kazi wizara hizo kwa vizuri.

Lakini kwenye suala la ugatuzi kuna suala la elimu inaonekana. Mhe. Mwenyekiti, katika kamati yake wamegundua kama kuna tatizo la elimu baadhi ya Madiwani na sisi bahati nzuri kamati yetu ya Ustawi wa Jamii katika kuranda huko kwenye Halmashauri na maeneo mengine tumegundua kuna tatizo la elimu kwa baadhi ya Waheshimiwa Madiwani.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe sana wakurugenzi pamoja na wizara hizi husika iwape elimu zaidi Waheshimiwa Madiwani ili wanapopitisha bajeti kuna eneo moja tulikwenda Wilaya ya Kati Waheshimiwa Madiwani wanaambiwa milioni mia na hamsini wanasema imepita hiyo, lakini hawajui imetengwa kwa ajili gani. Kwa hivyo, niiombe sana serikali Waheshimiwa Madiwani wapewe elimu ya ugatuzi lakini pia kupitisha vifungu vikubwa zaidi. Tulizowea halmashauri zetu kile tunachokusanya ndio tunachotumia, lakini kwa sasa ina maana kuna ruzuku kubwa kutoka kwenye Serikali Kuu kwa hivyo tuwaelimishe ili wanapopitisha kwenye Mabaraza yao waweze kufanya vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho niunge mkono ripoti hii ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa anafuata Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na baadae ataafuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said wa Jimbo la Chake Chake.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa fursa hii adhimu ya kuchangia kwenye ripoti hii ambayo imewasilishwa sasa hivi. Kwa kweli ripoti nzuri, imeandikika vizuri na imeelezwa kwa urefu, ndio maana hata wachangiaji wengi wanaogopa kuchangia kwa sababu mambo mengi yameelezwa humu. Kwa sababu hiyo nimpongeze Mwenyekiti pamoja na Wizara zote husika zilizosaidia kutoa maelezo yaliyosababisha kupatikana kwa kitabu. Kwa mwenendo huu nadhani tutafika pahala shughuli zetu zitakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiingia kwenye maelezo yenyewe kwanza nichangie kwa jumla tu kwamba kuna maboresho ambayo ingebidi tuyafanye, mwenzangu mmoja hapa Mhe. Ali Salum Haji yeye alisema kwamba kuna baadhi za idara zimeeleza lakini hazikueleza changamoto wala maoni ya kamati. Kapendekeza kwamba tunapoeleza idara basi mtueleze na changamoto kwa sababu hakuna jambo linalofanyika lisiwe na changamoto lazima kila kitu kina changamoto zake, kwa hivyo zikielezwa vizuri changamoto na maoni basi hata wale wachangiaji watajua wachangie namna gani.

Mhe. Mwenyekiti, hayo ni maelezo ya jumla, lakini pia kuna hizi Idara mpya za Mipango, Sera na Utafiti zinafanya utafiti ndio maana yake zimepangwa kwamba zifanye Mipango, Sera na Utafiti, sasa maelezo yote yalliyomo humu ni maelezo ya sera na mipango, lakini utafiti hamna. Pia nashauri waeleze utafiti kwa sababu ni muhimu unapofanya utafiti unaboresha ile hali iliyopo sasa hivi pengine ina mapungufu ukiyafanyia utafiti utapata kuyaboresha. Pia utafiti unasaidia kuongeza kama kuna mazuri yapo, lakini kuna jambo limeonekana katika utafiti basi linaweza kutumika kuongeza ili kuboresha zaidi. Halafu pia linaweza

likatoa marekebisho kwa mipango iliyopo ikaondoka kabisa ikaletwa mingine mipya ili kupata ufanisi mkubwa zaidi.Kwa hivyo, suala la utafiti nalo tunaomba sana tukilifanyia tukiingia kwenye kamati tukienda kwenye wizara husika na zile idara husika basi zitueleze na utafiti unafanywa vipi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nimeona nilichangie ni Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa. Idara hii kwa kweli ni muhimu sana ina nyaraka za serikali ambazo ni muhimu kabisa lazima zitunzwe. Lakini wameeleza kuna changamoto hapa kuna ukosefu wa bajeti, upungufu wa bajeti kuna mambo mengi. lakini pia utekelezaji unaambiwa ni mzuri sasa imepungua vipi hiyo bajeti sijui. Lakini ninachotaka kushauri ni kwamba bajeti zote zinazofanywa najua zinafanywa na idara yenyewe halafu wizara inakaa wanazifanya tena halafu zinapelekwa huko zinakofanywa. Sasa nawashauri wafanye *Program Basic Budget* ambayo inaeleza program zao na mahitaji ya fedha zao ikipelekwa wizarani wakae wazitetee na huko Wizara ya Fedha nako wanakoweka *ceiling* nako wakazitetee ili hizo fedha zipatikane kama zinavyotakiwa.

Halafu kuna tatizo la usafiri ni jumla hiyo wapatiwe usafiri kwa kweli magari mabovu hawawezi kufanya hizo kazi zikenda vizuri zaidi. Pia sehemu zilizokuwa na majengo mabovu yarekebishwe, tupate majengo ambayo wafanyakazi watafanya kazi bila ya wasiwasi na bila kupoteza pesa kwa sababu majengo yakiwa mabovu kila siku tutatengeneza, kila siku tutapoteza pesa. Wakati mwengine utalazimisha kuhaulisha pesa ambazo hazikuingizwa kwenye bajeti lakini uhami hali ya ubovu uliokuwepo. Kwa hivyo, tunashauri sana sasa hivi haya mambo yaweze kurekebishwa ili twende vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, halafu hapo hapo kwenye Idara na Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa tunajua kwamba nimesema hapo mwanzo ni muhimu sisi hapa nadhani tunastahiki kuwa na kumbukumbu

hata enzi za kimapinduzi. Kwa mfano, tumekwenda Kigali pale Rwanda, mauaji ya Kigali pale yamewekewa kumbukumbu mpaka *mortuary* unaingia mle ndani unapata maelezo ya *audio,* ya maandishi, ya picha na kila kitu. Kwa nini na sisi tusiweke kumbukumbu kama hizo tukaonesha vishoka vilivyotumika kupindua, marungu yaliyotumiwa, kila kitu kilichotumiwa kupindua. Kwa sababu haya Mapinduzi ni muhimu tukiweka kumbukumbu hiyo ambayo itasaidia watalii wanakuja wataona,wananchi hapa wataona wasiojua mapinduzi ambao wengi kabisa hawayajui yalitokea namna gani.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani tuna haja ya kuwa na kumbukumbu zinazostahiki hata Malaysia kule nako kuna kumbukumbu zinaonesha mpaka mambo ya asili mtu anapozikwa, mtu anapohudumiwa akiwa mgonjwa, harusi zote zimewekwa pale kama *model.* Tukiwa na kumbukumbu kama hizo na sisi pia tunaweza kuongoza hata hizi huduma za kitalii na watu wetu pia wakawa na maarifa ya historia za nchi yetu. Halafu pia pameelezwa kwenye kumbukumbu wamewapitia watu wa zamani wakawahoji kupata maelezo lakini hawakueleza ni watu wangapi wamehojiwa na hizo kumbukumbu zimewekwa wapi. Mhe. Mwenyekiti, basi tuelezwe ili tupate usahihi wa maelezo yanayofaa.

Mhe. Mwenyekiti, naingia tena kwenye Mahkama nimeshtuka hapa kidogo kwamba migogoro ya ardhi bado inaongezeka, migogoro ya ardhi imeanza kushughulikiwa siku nyingi sana badala ya kwamba tuambiwe yanapungua sasa yanaongezeka, ipo hapa sentensi kwamba migogoro ya ardhi inaongezeka. Kwa hivyo, hili nalo tulishughulikie kwa maana Mhe. Rais alilitilia mkazo sana hii migogoro imalizwe sasa tuambiwe hapa tena migogoro inaongezeka kidogo inatupa mashaka.

Mhe. Mwenyekiti, niende zangu sasa moja kwa moja kwa sababu mambo mazuri humu ndani marekebisho madogo madogo haya

hayana haja sana, niende kwenye kikosi chetu kikubwa sana cha *KMKM* ambacho ni kikosi muhimu sana. Wananchi wengi wa Zanzibar kazi zao za kiuchumi ziko baharini wanalima mwani, wanavua wanafanya kila kitu. Sasa kuna mambo ya uokozi yanafanyika ambayo inaweza kutokezea dhahma huko kwenye shughuli za uvuvi basi kuwa na kitu cha uokozi. Sasa nilitaka kusema kwamba vituo vya uokozi vya baharini na nchi kavu viimarishwe na vile ambavyo havina vifaa vinavyotakiwa katika kuimarisha huko basi vipatiwe vifaa, ili mazao yetu kusafirishwa nje kwa njia ya magendo, kuingiza madawa na kadhalika, kuzama kwa watu baharini waweze kuokolewa mara moja wanapotokezewa na matatizo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sikuwa na michango mingi sana isipokuwa haya niliyoyaeleza hapa. Nawatakia kheri kamati hii iendelee kutuletea mambo ambayo tutaweza kuyachangia vizuri zaidi ili kuboresha utendaji wetu wa kazi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi safi sana na sasa namwita Mhe. Suleiman Sarahan Said na baadae akifuatiwa na Mhe. Mussa Foum Mussa na kama muda utatosha Mhe. Hidaya Ali Makame.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa hii na mimi ya kuchangia ripoti ya kudumu ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi. Awali ya yote niwapongexe kamati pamoja na eizara nzima katika jitihada zao za kuweza kuweka changamoto na kuweza kufanikisha masuala yetu ambayo tunakwenda hatua kwa hatua katika kukuza nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nizungumzie Idara za Serikali katika masuala mazima ya ajira. Katika sekta nyengine za serikali kwenye idara kuna watu wengine wanajiona ni *super* ukiwa

mfanyakazi wa *ZRB, TRA*, benki na mawizara mengine yanayofunga tai, basi wanakuwa wanawadharau sana baadhi ya wizara nyengine kuona kama wao wana renki fulani katika serikali wakati wote ni wafanyakazi wa serikali. Hili ningeliomba sana wizara ikaweza kuwapatia elimu ya kutosha wafanyakazi wote kutokudharauliana katika sekta zao wakati wote ni wafanyakazi wa serikali.

Kwa hivyo ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, hili tukalitizama kwa jicho la huruma. Najua ni taaluma tu, mfanyakazi yeyote wa serikali ni mfanyakazi lakini taaluma inaona nani bora na nani si bora katika sekta hizi lakini wote ni jamii moja. Kwa hivyo, hii ni taaluma ya kuweza kufahamishwa baadhi ya wafanyakazi wasijione bora katika sekta zao.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie suala ambalo liko katika wizara zinazotoa huduma katika kuajiri wale watu mnaowaweka pale *reception* basi waangalieni kwa macho mazuri sana waweze kujua, hata kama mtu ana ulemavu, suruali imechanika wakati anataka huduma asimdharau. Kwa sababu wanamuona hayuko *high quality* basi anaweza kuwa hamuoneshi, wala hampembejei, wala hawi katika mazingira mazuri ya kuwa anaweza kumhudumia akaweza kufanikisha lengo lake ambalo liko pale. Nikimaanisha watu ambao wana kipato cha chini hata viatu hakuvaa anamdharau hata hajafika. Ningeomba katika hoja za binaadam Mheshimiwa watu wale ambao mnawaweka *reception* kabla ya ukaguzi wa kumuweka eneo lile mkaweza kuangalia, sio mtafute mtu aliyeshinda mnamuweka pale kwa kumtia adabu kumbe mnatia watu adabu.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukulie katika sekta nyengine ni kwamba mazingira mengi sasa hivi tunayo lakini kazi ni nyingi sana zinazofanyika katika nchi hii na kila mmoja ana haki ya kufanyakazi anayoitaka, mcheza muziki nae mpe nafasi yake akiwa ni msanii aoneshe kipaji chake tusimdharau kwa sababu ni msanii, mwengine anayefanya kazi ndio hivyo. Sasa utakuta

mazingira mengine hasa mijini lazima tuangalie kuna hali halisi ya kuitwa mji na ndio maana ukasikia mjini *form six* kabla hata hujasoma. Kwa hivyo, lazima tuangalie mji unataka thamani gani ndio tuweke mji, leo tunajisifia kwamba tunataka utalii, utalii wenyewe ukifika saa mbili unalala, utalii huo utalii gani.

Ni lazima tuangalie kuna umuhimu wake katika sehemu za mjini sio shamba watu wanakwendaje kiheshima, wanakwendaje katika tamaduni, wanakwendaje katika kustarehe katika miji lazima tuangalie tutizame upande mmoja. Kama kuna kosa lirekebishwe lakini tusikatishe watu starehe zao lazima tuangalie masuala ya mji. Hata hiyo zamani yalikuwepo masinema watu walikuwa wanakwenda kustarehe, lakini sasa kosa moja tu tunachanganya mambo yote hata kama ana *interest* zake anachanganya yote. Tusiwe hivyo tutizame kosa liko wapi turekebishe mambo mengine tukisema tunayachanganya itakuwa tunaondoa hali halisi inayowezekana.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie suala la ukosefu wa wafanyakazi katika maeneo. Mimi nasema hii ni changamoto mtu tunakuwa katika daftari ambalo tunajua watu wangapi wanastaafu katika kipindi hiki, lakini wengine wamepata matatizo gani katika kipindi hiki, unaweza kukaa mwaka mzima walimu hawatoshelezi, madaktari hawatoshelezi, maeneo mengine wafanyakazi wa maidara hawatoshelezi wakati watu nje wanapiga kelele hawana kazi. Sasa mimi hili linanishangaza kidogo tunakuwaje katika takwimu zetu na hiki ni kitu muhimu ambacho watu wale wanataka huduma. Ningeomba suala hili Mhe. Mwenyekiti, likatizamwa ili lisipewe nafasi mwaka mzima bado inatafuta mtu wa kukaa ile sehemu ambayo inatakiwa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nichukue katika afisi zangu za Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya Chake Chake, ule ni mji mkuu wa Pemba, ni mji mkuu namba mbili katika Mji wa Zanzibar.

Mheshimiwa majumba yale hayaridhishi kuitwa Mkuu wa Mkoa wala kuitwa Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya ndio ana banda kabisa maana yake ukitoka mlango wa mwanzo unamkuta yeye kakaa kitako hapa. Kwa hivyo, hadhi ya Mji wa Chake Chake kutokana na ilivyo Mheshimiwa naomba sana wizara inayohusika iwajengee majengo haraka iwezekanavyo watu hawa au iwapatie majengo mengine ambayo yatakuwa yanalingana na hadhi, unatafuta mtu anakwenda kwa Mkuu wa Mkoa ofisa anayepita na wewe unamuuliza unanipitisha wapi anakwambia ndio kwa Mkuu wa Mkoa. Kwa hivyo, Afisi ya Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa wa Chake Chake kwa kweli haziridhishi kutokana na hadhi yao ningeomba sana suala hili likafanyiwa ukarabati wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni masuala ambayo barabara za ndani ambazo tunazipigia kelele kila siku katika nchi yetu ni barabara ndogo ndogo zenye nusu kilomita, robo kilomita na kilomita moja lakini kasi ya uendeshaji wa barabara zile bado ni ndogo sana. Ningeomba sana wizara inayohusika ifanye kila jitihada kwa sababu tumeshatoa maelezo mengi katika ilani zetu kwamba barabara hii itafanyika, sasa barabara za ndani za nusu kilomita, robo kilomita na kilomita moja haraka iwezekanavyo zifanyiwe ufumbuzi ili wananchi wetu wapate maendeleo katika nchi yetu.

Lakini pia usafiri katika wizara na katika maeneo mengine bado unaleta shida magari yameshapitwa na wakati au yameshakuwa mabovu yameshatumika muda mrefu, inakuwa kila siku matengenezo spana mkononi na pia pesa nyingi kuendelea kutumika katika maeneo ambayo yanakuwa pesa zile hazitii tija kwa sababu kila wakati gari inaharibika. Lakini pia mawizara nayo magari yake yatumike vizuri, magari ya serikali yanatumika vibaya jioni au usiku, kwa kweli sasa hivi serikali imeshatoa nafasi sana ya kukopesha magari watu wengi tu, wakopesheni magari wafanyakazi wetu waweze kutembelea usiku magari yao waache magari ya serikali kufanya kazi usiku. Ningeliomba sana hili serikali ikalitilia mkazo.

Mhe. Mwenyekiit, niingie tena kwenye wafanyakazi kama wa serikali katika sekta za afya, hii ni sekta muhimu ndio kwa upande mmoja wewe unakaribia kaburi au ndio nduli yupo karibu yako ukipelekwa pale maana yake ukitoka ndio unasema *alhamdulillah.* Tuangalie sana watu tunaoajiri mle ndani, tuangalie hasa watu ambao wanakuwepo katika maeneo yale ya kupokea wageni pamoja na wale wa huduma. Mheshimiwa watu wale wengine ni wajeuri kupita kiasi lazima tuangalie hizi takwimu zetu ziwe zinatupa huyu anaweza kukaa na mgonjwa hawezi, sio lazima tuangalie kwenye *qualification* zake, mengine lazima tutizame na uratibu mwengine Mheshimiwa. Ningeomba sana maeneo ya hospitali watu wanalalamika mno kutokana na ajira za watu ambao zinafanyika maeneo yale.

Mhe, Mwenyekiti, niende kwenye sehemu nyengine ya Wakfu na Mali ya Amana kule nako kunafanyika vitendo ovyo ovyo kweli kweli, haki ya mtu anapewa mtu na dhulma ndio kwenyewe. Ningeshauri sana Mheshimiwa suala lile likatizamwa sana wale wenzetu wanatupelekesha ovyo wanawadanganya mahakimu, wanakuwa wanaleta vyeti vya uongozi. Mimi ningeshauri sana Mheshimiwa eneo hili ukalitizama sana kwa sababu pahali pa mtu haki yake ni lazima umtupie haki, hawa ndio wanaofanya mpaka kesi zikaenda Mahkama ya Rufaa kwa hawa, kila mtu haamini kile kinachotendeka…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, jalada ni kubwa sana wenzangu watachangia. Naunga mkono asilimia mia moja ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana sasa ninamwita Mhe. Mussa Foum Mussa wa Jimbo la Kiwani akifuatiwa na Mhe. Hidaya Ali Makame.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa fursa ya kuchangia katika ripoti hii ya kamati.

Kwanza na mimi nipongeze Kamati hii ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi. Vile vile niwapongeze mawaziri wote wawili wanaohusika na kamati hii kwa utendaji wao mzuri wa kazi unaoridhisha vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo niende katika changamoto za Afisi ya Mufti hususan Pemba. Naomba ninukuu katika ukurasa wa 39 katika changamoto (b) inazungumza kwamba "Kushamiri kwa migogoro mbali mbali ya ndoa na misikiti". Halafu (d) inasema "Utendaji usioridhisha kwa maafisa wa Afisi hiyo kwa upande wa Pemba husababisha migogoro isiyokwisha baina ya waumini wa Dini ya Kiislam".

Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi nimepata mshtuko kidogo katika changamoto hizi kwa sababu sisi Zanzibar wengi wetu ni waislam na Afisi ya Mufti ni afisi ambayo inajihusisha sana na mambo ya kiislam, hutegemea sana sisi waislam katika afisi hii ya mufti ndio kimbilio letu. Lakini leo tunaambiwa kwamba migogoro mbali mbali ya kindoa na misikiti, misikiti ni sehemu za ibada na sisi waislam hata mtu mfano kapata matatizo basi anaweza kukimbilia msikitini kwa kuona kwamba huku nitakwenda kupata amani.

Lakini leo ndio kumekuwa na migogoro mikubwa na vile vile hii ofisi mategemeo yangu ni kwamba inaweka watu walio na ujuzi katika mambo ya kiislam. Sasa nadhani nimuombe Mhe. Waziri hili suala basi lifuatiliwe ili kuona kwamba ofisi yetu hii ya mufti inakwenda vizuri na inaisuluhisha migogoro hii wao, sio wawe ndio wenye kuchochea migogoro.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niende Tume ya Utumishi Serikalini, kwanza niipongeze hii tume kwa jitihada zake nzuri wanazozifanya katika kuajiri vijana wetu kuingia kwenye utumishi wa umma, lakini hakuna kitu kilichokuwa hakina kasoro ndogo ndogo. Mimi nitoe mfano katika hii njia ya uajiri kwa mfano niseme kwamba tuna tatiz la walimu au tuna upungufu wa walimu mfano Tumbatu, sasa imetokea ile ajira mimi hapa

nashauri kwamba ikiwa tunao vijana Tumbatu wenye kutimiza masharti ya ualimu basi ni vyema wakachukuliwa kule kule Tumbatu kuliko kuchukuliwa mjini waende wakasomeshe kule.

Kwa mfano, nitoe maelezo kwamba mimi najulikana Pemba nzima nathubutu kusema tatizo la walimu lipo Muwambe, leo kuna vijana Muwambe wanajitolea katika kusaidia wanafunzi lakini inapotokea ile ajira wale wa Muwambe hawachukuliwi. Inawezekana ikawa masharti yote wametimiza vijana kule wamemaliza cheti, tuna vijana wanamaliza diploma ya ualimu, tuna vijana wamemaliza mpaka digrii. Kwa mfano, mwaka jana tuliandikisha vijana 611, mwaka huu tumeandikisha 985, lakini tuna vijana ambao wameshamaliza cheti, digrii, diploma hawapungui kama 24 leo pale wanajenga taifa inapotokea hii ruzuku wale tena hawaangaliwi. Sasa hii hapa mimi kwa mawazo yangu basi hatufanyi vizuri waangaliwe vijana ikiwa masharti wametimiza basi ile *priority* kwanza ianze pale, haiwezekani vijana wale kwa mfano ukamtoe mtu Mkoani au Micheweni uniletee pale wale pale watajihisi vipi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba hii tume hili suala ilione ajira inakuja kwa watu kutoka popote Zanzibar lakini basi tuangalie kipaumbele cha hiyo sehemu, Muwambe tuna mikondo mitatu hivi sasa kwa sababu tuna upungufu wa walimu lazima tusomeshe, serikali imesema watoto wote wachukuliwe. Kwa mfano, mwalim umempanga asubuhi anatoka Chake Chake kuja kusomesha Muwambe hata akifika si saa saba tena anakuja kusomesha nini. Sssa nadhani hili suala tulione na kwa mara hii Mhe. Waziri nakuomba kwa kuwa ajira ya walimu karibu hicho kipaumbele ndio napiga kelele uione hiyo hali.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 84 Baraza la Mji Mkoani. Hapa nimeona kwamba Baraza la Mji Mkoani limepata sifa hususan Mkurugenzi wake kwamba wamevuka malengo. Kwa hivyo na mimi ni mtu wa Mkoani napenda nipongeze hii hali na nimpongeze Mkurugenzi kwa jitihada yake nzuri, azidishe

kufanya jitihada hii ili tuone kwamba tunakwenda vizuri, isije kugeuka kwamba leo tunamsifu kesho mambo yakenda vibaya.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nizungumzie habari za vyeti hivi vya kuzaliwa, vitambulisho vya vizazi na vifo. Hapa tumeelezwa kwamba kuna tatizo la magamba ya kupata vyeti. Hili suala limekuwa la muda mrefu. Kwa mfano, mtu amekwenda kuandikisha mtoto Wilayani ili kupata cheti, anaweza akenda miaka minne, mitano hajapata cheti. Tatizo liko wapi na tatizo hili limekuwa la muda mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba Mhe. Waziri hili suala litafutiwe ufumbuzi ili hili tatizo liondoke. Watu wetu sehemu nyengine wazito kwenda kuandikisha vizazi na vifo lakini wakati huo huo wanapata matatizo ya kuvipata vile vyeti. Nadhani iko haja ya kuona kwamba hili suala muamko wake ni mdogo na ikitokea kuna matatizo ya hapa na pale tatizo linajitokeza kuwa vyeti havipatikani. Nimuombe Mhe. Waziri hili suala alitafutie utaratibu ili hayo magamba basi yaweze kupatikana kwa umuhimu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nirudi tena kwenye changamoto zinazoikabili Kamisheni, hapa nije katika ukurasa wa 47 katika changamoto Nam.3 inasema:

> “Wananchi kuitumia vibaya sheria ya eka tatu (3) na kupinga agizo la Baraza la Mapinduzi la mwaka1993 la kuyarejesha mashamba ya wakfu/amana kwa Katibu Mtendaji Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar”.

Nadhani Mhe. Mwenyekiti, hapa kumejitokeza matatizo kidogo ya uelewa, kuna mashamba yalikuwa ni wakfu lakini hata katika kukodisha mara hii hayo mambo yalijitokeza kutokuwa na maelewano mazuri. Naomba hili suala litafutiwe ufumbuzi, yajulikane mashamba ya wakfu na mashamba ya eka ili hii

migogoro isijitokeze. Kipindi kikubwa haya mashamba inaonekana yalikuwa upande wa wakftu lakini pametokea sintofahamu hapo, kwa hivyo naomba hizi sehemu mbili zikae vizuri ionekane kwamba kuna mashamba ya wakfu yajulikane na mashamba ya eka yajulikane.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mimi naunga mkono ripoti hii mia juu ya mia, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mussa Foum Mussa na kwa sasa Mhe. Hidaya Ali Makame atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa asubuhi hii, karibu sana.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia machache juu ya ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia tukiwa wazima na bado tunaendelea kuvuta pumzi zake bila ya kuzitolea ushuru wowote au kuzilipia ada yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, pia niendelee kuwapongeza Wajumbe wa Kamati hii kuanzia Mwenyekiti, Makamo Mwenyekiti na Wajumbe wake wote anaofuatana nao katika kuhakikisha wanaitendea haki kamati yao. Lakini pia wanazitendea haki zile wizara zote ambazo zinawahusu katika kuzifanyia kazi zao na kuyaweka sawa yale ambayo yanapaswa kuwekwa sawa na kurekebishwa yale na yale ambayo yanastahiki kurekebishwa. Niwapongeze sana Wajumbe wa Kamati hii kwa kazi ngumu na kazi kubwa ambayo wanaifanya kwa kweli tunawaona jinsi wanavyopambana kutenda haki juu ya kamati yao hii.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze sana kwa nafasi ya pekee Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja akishirikiana na kusaidiana

kazi pamoja na Wakuu wa Wilaya zote mbili, lakini na Wakurugenzi wa Halmashauri zetu zote mbili. Pia wajumbe wote wanaofanya kazi Mkoa wa Kaskazini Unguja niwapongeze na niwashukuru sana kwa kazi zao wanazozifanya kwa hali na mali.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka huko kwenye shukrani na pongezi nije kwenye ripoti moja kwa moja kwenye Afisi ya Mufti. Hapa Wajumbe wa Kamati wameorodhesha mambo mbali mbali katika ripoti hii, lakini kuna changamoto na kuna mafanikio mbali mbali. Ningegusia tu kidogo kwenye changamoto ambazo wameziorodhesha.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Mufti ina changamoto kubwa ya ukosefu wa vyombo vya usafiri pale ambapo wanakuwa wanahitaji kwenda vijijini kutoa hiyo huduma inayostahiki. Ningeiomba sana Wizara wakaiangalia sana Afisi ya Mufti kwa sababu ndio kimbilio la waislam wote na bila ya afisi hii kuna mambo mengi sana yatayumba. Kuna haja ya huu uongozi kupita katika vijiji vyote na kila pale panapohusika ili kuweka sawa, kusawazisha na kuwasaidia wananchi wake juu ya hali ya nchi yetu ilivyo lakini pia hali ya kimazingira ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi tunaona uislam wetu unapelekwa na watu na kila mmoja kawa shekhe, kila mmoja kawa Ustadh, kila mmoja kawa vile anavyojua yeye, ili mradi tu aweze kumpotosha mwenziwe au ampeleke kwenye njia sizo. Tunawajua Mashekhe wengi, Wanazuoni wengi, Walimu wa Madrasa wengi, kwa hiyo hii Afisi ya Mufti kuna haja ya kupatiwa vyombo vya usafiri wakafika maeneo yanayohusika vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, kama utaniamini kuna hali ambazo sasa hivi hata kuzisikia unaona tabu utasema labda mimi nakufuru nikisema. Wanafika kusema mashekhe sasa hivi wanawaambia wananchi "tumsalie bwana Mtume" pia ni dhambi kusema, hili suala limetoka wapi. Kwa kweli kuna haja kubwa sasa hivi

viongozi wetu hawa kupitia afisi hii wakatoka nje ya maeneo na kuwafikia wanajamii na kuwaelimisha kwa kila pale panapowahusu wao, kwenye masuala ya ndoa lakini pia kwenye masuala ya utawala na dini yetu. Hali haipo vizuri, kwa kweli tunaburuzwa, tunapelekeshwa na hatujui wapi tushike kwa sababu kila Shekhe anakwambia lake. Kwa hivyo. kuna haja afisi hii kufanya kazi zake vile inavyopaswa ili mradi tukaona ile hali inatulia na ipo sawa na tunafuata ule muelekeo ambao Mwenyezi Mungu wetu katushushia na Mitume yetu ikatuelekeza tukawa tunapata hiyo mielekeo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo pia kuna changamoto ya kushamiri kwa migogoro mbali mbali ya kindoa na misikiti. Hili pia linahusiana pale pale nilipolizungumza hili suala la mwanzo. Hii afisi au hawa watendaji wangekuwa wanafika huku kwenye hivi vijiji au wanafika kwenye haya maeneo kufanya kazi ile inayopaswa, hata hii migogoro nayo pia ingepungua kwa sababu ile elimu ya mara kwa mara wangekuwa wanaipata. Lakini pia na kule kufunuka macho kwa hawa wengine ambao wamefumbwa macho wanasubiri tu kila shekhe aje awaletee wapokee, mashekhe wengine sio na walimu wengine sio na ndio wanaosababisha hii migogoro na haya mambo mbali mbali mengine ambayo hata hayastahiki katika misikiti wala katika ndoa.

Kwa kweli kuna haja kubwa Mhe. Waziri ningekuomba sana ukaingalia hiyo Afisi ya Mufti kwa macho mengi ya huruma na ya pekee ukaipatia usafiri nayo ikafanyakazi. Niiambie hii afisi kwamba endapo itapatiwa hivyo vifaa vya usafiri na kabla hapo haijapatiwa hivyo vifaa vya usafiri, basi itende hali ile ambayo wamekula kiapo kutokana na dini yao, lakini kwa imani yao wa kiislam na kwamba wameamini Mwenyezi Mungu ndie aliyewashusha na kazi hiyo. Basi waitende kihaki *lillah* ili mambo mengine yote yakae sawa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakuja ukurasa wa 73 kuhusu Mkoa wa Kaskazini Unguja, mkoa jembe, mkoa mama. Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuwapongeza sana Wakuu wa Wilaya zote mbili, lakini pia na Mkuu wa Mkoa wetu wa Kaskazini Unguja. Kwa kweli kuna changamoto hapa nazo zimeonekana wajumbe hawa wa kamati wameziorodhesha hapa nyingi na wenzangu wameshazizungumza na mimi nitazungumza baadhi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna changamoto hapa ambayo inazungumza kwamba muamko mdogo wa wananchi katika Mkoa wa Kaskazini kujihusisha na mambo ya kimaendeleo na kiujasiriamali. Mhe. Mwenyekiti, hii ni kweli changamoto, lakini haiko kihivyo labda ilivyo kichangamoto kwa sababu muamko upo na wananchi wanafanya kazi. Lakini hapa kinachokosekana ni vile vitendea kazi kwa sababu kama ni ujasiriamali, wajasiriamali ndani ya Mkoa wa Kaskazini wapo tele, dagaa kavu linaanikwa Kaskazini Unguja, tungule zinalimwa Kaskazini Unguja, manjano inalimwa Kaskazini Unguja, tangawizi, huo ndio ujasiriamali. Wavuvi wa madema na wavuvi wa kila aina wapo ndio ujasiriamali unaozungumzwa, vikundi cha *SACCOS* vipo, vikundi vya ngoma vipo, yaani vitu vingi tu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo kusema kwamba muamko mdogo mimi niseme kama sio mdogo. Muamko upo wa hali ya juu kinachokosekana niseme kama ndio labda kile kitu ambacho kinaweza kuwasaidia wakaweza kufikia yale malengo ya ule ujasiriamali wao. Lakini kwa kweli wanajitahidi ila tu wizara ijitahidi nao kuwasaidia hawa wajasiriamali wetu na wao waendeleze hizi biashara zao au waendeleze hivi vikundi na mradi hali ziendelee na wananchi wasisubiri ajira. Kwa kweli wanasubiri ajira na wanajitahidi lakini tuwaone jinsi gani na wao wanavyopambana ili tuweze kuwasidia.

Nikitoka hapo nije kwenye miundo mbinu mibovu ya barabara. Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana halmashauri yangu ya Wilaya

ya Kaskazini Unguja inajitahidi katika mambo mengi, inajitahidi kwa wananchi wake. Lakini pia inajitahidi kutekeleza yale ambayo yanapaswa kutekelezwa na mpaka sasa hivi walivyoingia huko kwenye ugatuzi tumeiona jitihada wanavyoifanya katika Wilaya ya Kaskazini. (*Makofi*)

Lakini mimi ningeiomba sana hapa wizara pamoja na serikali kwa ujumla. Mheshimiwa tunafahamu kwamba Mkoa wa Kaskazini Unguja ni mkoa ambao umetawaliwa sana na utalii na wawekezaji wengi sana wako katika Mkoa wa Kaskazini. Kwa kweli kama tutawaangalia wawekezaji wale walioko ndani ya Mkoa wa Kaskazini basi leo isingefikia hapa haja ya sisi wananchi au wanakijiji kulalamika juu ya suala la miundo mbinu mibovu ya barabara za ndani. Kwa sababu kama mwekezaji anapokuja kutaka vibali vya kuwekeza na kila kitu, kwa nini wewe wizara hujui kama kule kuna tatizo la miundo mbinu, kwa nini usiwafuate wale wananchi ukenda kuwauliza kwamba kuna tatizo gani, kuna mtu anataka kuja kuwekeza, ili na wao wakatoa yale malalamiko na changamoto zilizomo mle yule mwekezaji akaweza kusaidia. Hii miundo mbinu ya barabara na mengineyo maji na umeme isingekuwa na haja ya kuja tukalalamikia hapa kwa sababu wale wanakuja kuwekeza katika nchi yetu kutuimarishia na sisi pia miundo mbinu yetu sio kujivunia wao tu wakaendeleza na utajiri kwa upande wao.

Lakini hata wale wananchi waliomo ndani ya vijiji wana haki ya kuwasaidia. Kweli leo kuna hoteli 40 ndani ya wilaya zile mfano tuseme ndani ya kijiji kimoja tu cha Nungwi. Mnashindwa kuitengeneza barabara moja inayopokea mahoteli si chini ya saba ambayo inawafikia ndani ya hoteli yenu mnafanya kazi gani ...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa malizia muda wako kidogo sana nakupa dakika moja.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie lakini kwa kweli dakika moja hainitoshi na muda kwa kweli kwa upande wangu ulikuwa ni hafifu sana. Kwa hiyo, ningeomba hata jioni tukirudi nipate japo muda wa dakika tano ili nimalizie mchango wangu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile muda hauruhusu niseme na mimi nisimamie hapo lakini sijaiunga mkono ripoti hii kwa sababu najua baadae nitaendelea. Niseme ahsante nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe kwanza niwashukuru kwa maendeleo ya michango ya ripoti yetu iliopo mbele yetu. Lakini naomba niwaeleze Waheshimiwa Wajumbe kwamba ripoti hii inatakiwa imalize leo jioni kuchangiwa na kupitisha lakini wachangiaji bado ni wengi waliobakia nina wachangiaji kama kumi hapa.

Kwa hivyo, niwaombe sana wajitayarishe wa michango ya maandishi wengine. Muda wetu wa jioni hautatosha. Kama unajijua umeleta mwisho basi ujiandae kuchangia kwa maandishi muda hautatosha.

Baada ya hapo niseme niendelee kuwashukuru na niweze kuakhirisha kikao hiki hadi hapo saa 11:00 jioni panapo majaaliwa.

(Saa 6:58 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Mwaka 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe katika meza yangu hapa ninao wachangiaji ambao kuwa nilisema kuwa kuna baadhi ya wajumbe itabidi wachangie kwa maandishi na kuanzia kwa muda wetu ulivyo leo na hii ripoti inatakiwa imalize tutaendelea nao ikifika pahali tutamia muda uliobakia kwa ajili ya kumpa mwenyekiti naye kuweza kuweka sawa.

Kwa hivyo, kwa kuanzia tunaanzia na Mhe. Tatu Mohamed Ussi na akifuatiwa na Mhe. Saada Ramadhan Mwenda na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu. Mhe. Saada Ramadhan Mwenda endelea.

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipatia nafasi hii na nataka kuzungumza machache niliyokuwa nayo. Kwanza naanza na kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kuweza kuniwezesha kuweza kufika hapa na kuweza kusimama kuzungumza haya niliyokuwa nayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi naanza na kuzipongeza wizara zote mbili kwa kazi kubwa wanazofanya wao kuanzia mawaziri na watendaji wao kwa kulitumikia taifa hili.

Lakini pili nawapongeza kwa upande wa vikosi kwa kazi kubwa wanazoshughulikia, wanazozitenda wanazokuwa wakizisimamia katika kuongoza nchi hii, nawaombe sana kwa Mwenyezi Mungu na kazi hii ya kutulinda sisi Wazanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kubwa hasa nilokusudia kusema niseme nimpongeze Mkuu wangu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi kwa kazi kubwa anayopamba nayo ya madawa ya kulevya, nasema aendelee kazi inaoneka lakini bado hajatufanyia kazi nataka

awapate wale wanaoleta unga sio wanaotumia unga kazi amejitahidi lakini aendelee asichoke.

Mheshimiwa niendelee hapo hapo Mkoa wa Mjini/Magharibi pamoja na Manispaa yake. Mhe. Mwenyekiti Mkoa wa Mjini/Magharibi na Manispaa ya Mjini nilikuwa kuna suala moja nawaomba sana la upande wa daladala. Mhe. Mwenyekiti daladala zimekuwa na usumbufu mkubwa na usumbufu huu mkubwa huu unakuja kunatokana mtu anatoka mfano bandarini anatoka Pemba au Dar es Salaam mwanamke, ana mzigo, ana watoto, awachukuwe watoto wale mpaka afike nao Kisiwandui kwa upande wa akinamama tunaumia sana kwasababu sisi ndio walezi wa watoto.(*Makofi*).

Kwa hiyo, nilikuwa nawaomba wafanye utaratibu wenzetu Dar es Salaama tuige mitaa ya wenzetu, wenzetu Dar es Salaam wameweka mabasi yale ya mwendo wa kasi, ukitoka bandarini unapandisha juu unapandisha basi utaenda kutafuta. Lakini kwa kutoka bandarini mpaka kisiwandui kama mama hana uwezo wa kuchukua ki *carry* akakikodi akapakia mizigo na watoto ni mtihani. Kwa hiyo nilikuwa naomba wizara ifanye maarifa Mkuu wa Mkoa, Manispaa washirikiane wafanaye maarifa alau ipatikane gari usafiri wa kuweza kufika kule bandarini wa kuweze kuwachukuwa watu isikae gari lakini iende kule ichukuwe watu na iwarudishe kama inavyofanya wenzetu Dar es Salaam aua kama wanavyofanya mikoa mengine na nchi nyengine, ni usumbufu mkubwa sana na tunawaomba wana kwa upande wa wanawake wanaumia sana wanawake, imekuwa ni shida ni kero.(*Makofi*).

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo mwenyekiti upande wa Manispaa hivyo hivyo kiukweli mji wetu ni mzuri, Mkurugenzi Serenge kajitahidi kwa bustani na kwa usafi pia si haba kajitahidi Mwenyezi Mungu amzidishie lakini tatizo moja lipo. Jamani lile soko la samaki kukaa katikati ya mji mtihani,

mitaa ya wenzetu wote masoko yako nga'mbo ya mji huwezi kuweka soko la samaki pale kati kati. Sasa hivi ukipita ni hatari na ni aibu maana yake hata sijui leo kuna samaki wa aina gani. Sasa hivi sisi wenyewe tunakereka je, wageni wanaokuja pale watalii kweli panakalika Darajani. Mimi nilikuwa naiomba serikali ifanye maarifa itafute soko ng'ambo ya mji sio pale soko la samaki lile libaki soko vitu vyengine tu, lakini soko la samaki litafutiwe alau ng'ambo kidogo alau kule kokote kule liwekwe lakini pale katikati liondoshwe imekuwa ni tabu sana.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, naenda hapo hapo nimuunge mkono ndugu yangu Sele alisema hapo kuna mtendaji kule Pemba kajenga taifa miaka kumi na moja, jamani kajitolea kweli kafanya kazi jamani muoneeni huruma maana yake angekuwa mtu wasi wasi sasa hivi kishavunijka moyo miaka kumi na moja sio mchezo kwa kujenga taifa tu weye. Naomba wizara imuonee huruma imuajiri yule jamaa kajitahidi mtoto na yeye msaidieni. Miaka kumi na moja si kidogo uhai wa mtu huo, naomba sana wamsaidie ili na yeye apate kunufaika ili roho yake alau iridhike kuwa alilijengea taifa lake na taifa limemjali mwenyewe kama serikali yake.(*Makofi*).

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti nilikuwa nataka kuomba niko ukurasa wa 79 upande Mkoa wa Kaskazini Pemba. Mheshimiwa nilikuwa naomba kuna matatizo haya masuala yamezungumzwa hapa haya masuala ,nilikuwa namuomba sana Mkuu wa Mkoa Mhe. Rais alimuamini yeye ndio maana akampa Mkuu wa Mkoa, asikubali kufanyiwa kazi na watu, hili suala tumelikuta na tumeliona linaumiza huwezi akatoka mtu akamuisha akafanya anavyotaka yeye akamtangaza mtu anayemtaka akatoa bendera akaweka Sheha huyo huyo hajaapishwa kapewa bendera akaweka, sheha huyo huyo, haiwezekani mambo mengine lazima mtu ujiamini Rais anapokuamini na wewe ujiamini. Namuomba sana asipende kumuachia mtu aliyekuwa Rais alimuona Afisa Tawala lakini Mkuu wa Mkoa alimpa yeye ndiye mwenye mamlaka

kwenye Mkoa wake. Kwa hivyo nilikuwa namuomba sana ajiamini sana katika kufanya kazi zake.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sina mengi kwa hayo naunga mkono asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe tunakumbuka kuna mjumbe hapa nilibakiza dakika zake tano Mhe. Hidaya kwa hivyo ili tumpe haki yake na yeye nampa dakika tano kuendelea katika mchango wake, Mhe. Hidaya karibu sana.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunikumbuka tena na mimi ukanipa zike dakika tano ambazo niliziomba kwa kumalizia, nikupongeze sana kwa kunionea huruma.

Mhe. Mwenyekti, kwa kuendelea na mchango wangu nilikuwa katika upande wa Mkoa wa Kaskazini Unguja. Mhe. Mwenyekiti, katika changamoto ambazo zimeonekana ndani ya Mkoa wa Kaskazini Unguja nilizungumzia kuhusu miundo mbinu ya barabara za ndani.

Mhe. Mwenyekiti, nilieleza kuhusu wawekezaji ambao tunao ndani ya Mkoa wa Kaskazini na nadhani ujumbe wangu wameusikia, lakini pia wizara inayohusiana na suala hili ningeiomba sana wakaziangalia tena kwa macho mengine barabara za ndani za Mkoa mzima wa Kaskazini Unguja, kwa sababu kama Ripoti ya Kamati inavyosema kwamba katika Mkoa ambao unao miundo mbinu mibovu ya barabara, ukianzia hizo kubwa zinazopita magari kuja mjini mpaka hizi za ndani basi ni Mkoa wa Kaskazini.

Kwa hiyo, kama hili lipo linaonekana na limeshaonekana basi kuna haja ya kukaa likafanyiwa kazi ili Mkoa wa Kaskazini nasi

kwa vile ni Mkoa dume nao tukajiona kama kweli Mkoa huu una thamani yake na hadhi yake, kwa sababu najua unazalisha mambo mengi, utalii mkubwa uko kaskazini, miundo mbinu mingi inapatikana kaskazini lakini pia wawekezajim wajasiriamali, wafanya biashara na kila kitu, tumeshafunguliwa soko kubwa pale Kinyasini lipo, litatusaidia lakini hata wateja watatoka mjini waje kaskazini waje watafute mazao. Kwa hiyo hii miundo mbinu ya barabara nayo imarishwe ili tu Mkoa wa Kaskazini nao uzidi kung'ara.

Mhe. Mwenyekiti, nikimalizia hapo nije katika changamoto nyengine ambayo ni kushamiri kwa migogoro ya ardhi. Mhe. Mwenyekiti, hili nalo ni janga kubwa sana katika Mkoa wa Kaskazini kila siku iendao kwa Mwenyezi Mungu basi hakutokosa kesi ya mgogoro wa ardhi nadhania hizo Makahama zetu tangu ndani ya Wilaya kama ingekuwa kuna hizo *security* zinazomurika basi tangu ndani ya Shehia mpaka Mkoa basi kesi zishakuwa nyingi kuhusu migogoro ya ardhi, mpaka niseme kwamba hawa washughulikiaji wa hizi kesi pia nao wameshachoka. Kwa hivyo kwa kweli hili suala nalo la kukaliwa kitako chini kikaonekanwa ni kitu gani ambacho kinasababisha hii migogoro ya ardhi ndani ya Mkoa wetu wa Kaskazini.

Mhe. Mwenyekiti, ila tu niseme kwamba tatizo ukisha lijua kulipatia dawa ni rahisi. Hivyo kwa vile na hili tatizo limeshajulikana kwa Mkoa wa Kaskazini basi tuone kwamba kuna haja sasa ya kukaa na wananchi wetu na viongozi wa kati kati, wa juu wote wanaohusiana na masuala haya tukaona ni njia gani tunaweza kuimaliza haya migogoro ya ardhi, lakini pia tukaweka na mbinu mbadala ya kuweza kusawisha hii migogoro, kwa kweli inakosesha watu amani wanafika watu mpaka kuhasimiana mpaka kuuwana. Kwa hivyo mimi ningeiomba sana wizara ikalingalia na suala hili lakini pia kwa kushirikiana na halmashauri zetu, kushirkiana na madiwani na masheha wote waliomo ndani ya Shehia na wilaya wakashirikiana tukaona jinsi gani tunaweza

kuzitatua hizi changamoto ili tu Mkoa wetu au Taifa letu nalo likawa liko hali ya utulivu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nisingependa nizungumze mengi kwa vile nimeshazungumza mwanzo niseme tu kwamba niwapongeze sana wanakamati kwa kazi zao wanazozifanya juu ya ufatiliaji wa masuala ya unyanyasaji, udhalilishaji na kufatilia mambo mengi yanayohusiana na nchi yetu juu ya kuweka sawa na kurekebisha kila kitu ambacho kinahusika katika wizara zetu mbili hizi.

Mhe. Mwenyekiti, michango mingi imeshatolewa niseme nawapongeza sana tena sana Wajumbe wa Kamati kuanzia Mwenyekiti na Wajumbe wake wote niseme tu tuko nao pamoja mashirikiano tutaendelea vizuri, lakini tu niwaombe sana mawaziri Mhe. Haji Omar Kheir, waziri wetu jembe mzaliwa wa Mkoa wa Kaskazini kwa kushirikiana na halmashauri zetu na Wakuu wa Mikoa wote basi nina hakika kazi itafanyika na mambo yatakaa sawa na hizi changamoto ambazo zimeonekana na kamati hata kipindi kinachokuja cha bajeti basi Inshaallah kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu yatakuwa yameshakaa sawa na mingi yatapatiwa ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache niseme na mimi naiunga mkono ripoti hii ya kamati kwa asilimia mia moja ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hidaya sasa ninamwita Mhe. Tatu Mohamed Ussi na akifuatiwa Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) ajitayarishe.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kuipongeza kamati hii iliyotuletea ripoti hii lakini pia niwapongeze waheshimiwa mawaziri walioshiriki pamoja na watendaji wa wizara hii kwa kushirikiana na kamati ili leo wakaweza kutuletea ripoti hii na tukaweza kuijadili.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo mchango wangu naelekea kwenye ukurasa wa 56 kuhusu changamoto zilizoikabili Chuo cha Utawala wa Umma Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, katika changamoto za hapa zipo ukosefu wa walimu wa kudumu ambapo chuo kinatoa kozi tofauti za cheti na diploma, lakini chuo hiki hakina mwalimu hata mmoja aliyeajiriwa kuwa wa kudumu. Lakini ukienda changamoto (c) ukosefu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa najiuliza chuo hiki kwanza hakina walimu inaonekana walimu wake ni wa kwenda tu na kurudi, hakuna mwalimu wa kudumu katika chuo kile lakini pia hata vifaa vya vyakufundishia hakuna. Sasa sijui wanafunzi hawa watasoma vipi na watahitimu vipi na kupata hivi vyeti na diploma kutokana na kuwa hata vile vifaa hakuna ukiachia mbali walimu, nilikuwa naomba nipate ufafanuzi Mhe. Mwenyekiti.

Lakini nikitoka hapo niende kwenye Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza Mkuu wangu wa Mkoa wa Kusini Pemba lakini niwapongeze Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya ya Chake Chake na Mkoani kwa kusimamia utekeleaji wa Ilani lakini pia na kufanya shughuli za kusafisha mji yetu ya Chake Chake na Mkoani.

Mhe. Mwenyekiti, niombe tu mashirikano haya yaendelee ili tuweze kufanikiwa kufikiwa lengo lililokusidiwa, nikitoka hapo Mhe. Mwenyekiti niende kwenye ukurasa wa 97 ambao unasema ukosefu wa hati miliki katika maeneo wanayotumia vikosi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla ya kuzungumzia hati miliki niwapongeze majeshi yetu ya Zanzibar vikosi vyote vya SMZ vikomo KMKM, JKU, Magereza na vikosi vyote vya Zanzibar kwa juhudi yao waliyoifanya katika kusimamia ulinzi wa zao kubwa la uchumi wa nchi la karafuu nawapongeza sana na waendelee kuwa wazelendo wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye ukosefu wa hati miliki katika maeneo yanayotumiwa na vikosi hivi. Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukishuhudia vikosi vyetu hivi vinajitahidi pamoja na Mhe. Waziri kusimamia juhudi za wanajeshi wetu ili kupata makaazi na kupata sehemu za kufanyia kazi, lakini nasikitisha kuona kwamba katika changamoto zilizotajwa katika taarifa hii ukosefu wa hati miliki katika maeneo wanayo kaa na wanayo fanyia kazi. Mimi nilikuza naishauri wizara kutokana na wingi wa migogoro ya ardhi naishauri wizara kuliona hili na kulifanyia kazi kwa ajili ya kutafuta hati miliki ili vikosi vyetu vikae bila ya hofu na bila ya kuwa na wasiwasi mheshimiwa napongeza sana.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye ofisi ya mufti tumeona ofisi ya mufti kuna ukosefu wa vyombo vya usafiri ambapo hupekelea kushindwa kutekeleza majukumu yao vijijini. Mhe. Mwenyekiti, ofisi hii ya Mufti ni ofisi nyeti na ni ofisi muhimu miongoni mwa ofisi nyengine na waislamu wengi tuko vijijini na kwa kweli tunahitaji elimu ambayo tunaipata katika familia zetu na pengine kuna changamoto ambazo zinajitokeza sasa mimi nilikuwa niombe tu Serikali kufanya juhudi za kuwapatia usafiri ofisi hii ili kwenda kuelimisha jamii kwenye vijiji na sehemu nyengine husika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa sina mengi kwa sababu mengi wenzangu wameshayazungumza na wala sitaki nipoteze muda baada ya maelezo yangu hayo machache naunga mkono ripoti hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Tatu Mohamed Ussi sasa anayefuata ni Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) na Mhe. Shaib Said Ali ajitayarishe.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi nianze kwanza kwa kukushurkuru wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi ili niweze kutoa mchango wangu katika ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalumu ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa 2017/2018.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nichuwe nafasi hii pia kumshukuru sana na kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hotuba nzuri aliyoitoa leo katika Mahafali ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, na pia kwa ushiriki wake katika mahafali hayo pamoja na viongozi wote. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba unitumie salamu zangu kwa niaba ya Kamati yetu ya *CPA* ambayo mimi nikiwa Mwenyekiti utupelekee salamu zetu kwa Bunge letu la Afrika ya Kusini kwa kupata Rais mpya ambaye Cyril Ramaphosa amechaguliwa leo kuwa Rais mpya wa Jamhuri ya Watu wa Afrika ya Kusini ni jambo zuri sana, Afrika ya Kusini na Tanzania na vyama vyetu vya siasa tumekuwa marafiki kwa miaka mingi, *ANC* pamoja na CCM. Lakini hata katika miaka ya nyuma pia tukiangalia Kusini mwa Jangwa la Afrika tumeshiriki katika ukombozi wa nchi nyingi. Kwa hiyo, baada ya hapo naomba sasa nianze kuendelea kwenye mchango wangu.

Mhe. Mwenyekiti, moja katika eneo ninalotaka nilizungumze ni katika *devolution of powers*, kwenye Halmashauri zetu. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba sasa tunapeleka madaraka yetu katika Halmashauri ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza kupata huduma nzuri na zile ambazo zinazostahiki. Lakini bado

katika changamoto ambazo zinajitokeza ni katika maskuli yetu ambayo yapo kwenye jimbo langu la Tunguu. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa katika Jimbo la Tunguu ukienda katika Kisiwa cha Uzi tunajenga skuli ya msingi katika Ng'ambwa, ukienda Kikungwi tumekamilisha pia mabanda pale ya kujenga skuli nipo mimi pamoja na Mbunge. Ukija pia Tunguu kwenye tunajenga skuli na imeshakamilika, Kibele tumeweka msingi na Dunga Kiembeni inafuata. Kwa bahati mbaya au nzuri Mhe. Mwenyekiti, na nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri wa Elimu tumejenga skuli katika Kijiji cha Kikungwi na nawashukuru sana wananchi wamefika hapa leo wapo pale juu, baada ya ukamilishaji wa jengo hili hivi sasa wanafunzi zaidi ya 43 wanaambiwa wakasome Unguja Ukuu. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa mikakati hii ambayo tunakuwa tunaipanga baina ya serikali pamoja na Halmashauri kuhakikisha kwamba kwa upande wetu sisi Wabunge pamoja na Wawakilishi tunashiriki kupeleka maendeleo kwa wananchi wetu. Sasa inakuwaje baada ya jambo lishakamilika panakuwa pana utata na ugumu, leo imefika wazee wa Kijiji cha Kikungwi wanakataa kupeleka watoto wao Unguja Ukuu. Lakini si hapo tu na wako 43, pia katika Skuli ya Tunguu wanafunzi zaidi ya 55 na banda la skuli tayari limeshakamilika panakuwa pana kigugumizi na watoto wanaambiwa wapelekwe maeneo ya Ndijani na maeneo tofauti. Mimi ninachoomba hapa Mhe. Waziri, Mhe. Haji Omar Kheir kwa kupitia halmashauri na kwa kushirikiana pamoja anichukulie hizi salamu pia kuzipeleka kwa wizara husika ili tushirikiane kwa pamoja ili tuhakikishe kwamba wananchi wetu kwa sababu natambua lengo letu sote kwa pamoja ni kushirikiana na kuleta maendeleo. Wakati mwengine wananchi hawa wanakuwa wako tayari kujitolea kwa hali na mali.

Kwa hiyo, mimi niiombe serikali yetu ambayo ni sikivu, wana wajali wananchi wao, wana nia njema basi salamu hizi Mhe. Haji Omar Kheir zichukue ukiwa waziri. Kwanza ni *senior*, halafu

hodari, jemedari mzuri kabisa, unajiamini, nikikuangalia kila tunapokuja kwako kwa ushauri unalichukua. Kwa hiyo na hili nakuomba sana Mhe. Waziri ulibebe kifuani ili tuweze kuhakikisha kwamba wananchi wetu na hasa wale waliokuja hapa wa Kikungwi, wamekuja hapa machozi yanawatoka, moyo wao inawauma wana hamu sana ya skuli yao iweze kuendelea pale.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo pia nataka nichangie suala la taka taka katika maeneo tofauti ya mji wetu. Mhe. Mwenyekiti, suala la taka taka kwa upande wa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, ukiingia katika mitandao ya kijamii wakati mwengine tunakuwa tunaandikwa vibaya kwa sababu kutokana na mazingira ya sisi kuwa tunapokea wageni wengi. Sasa ushauri najua kuna mpango mahsusi ambao wa jaa ambalo linatayarishwa kwa upande Kibele, lakini bado ukiangalia kwa upande wa miji yetu, unakuta wakati mwengine vijana hasa wanafunzi wanapokula vitu vitamu vitamu kama malai au *ice-cream* mtu anatupa taka taka chini kwa kutegemea kwamba Manispaa itakuja kusimamia kuondoa uchafu. Tunaomba sana elimu hii izidi kupelekwa maskuli ili taka taka za chupa za *plastic* na zile nyengine zinakuwa hazipendezi kabisa hasa katika maeneo ya mjini ambapo viongozi wanapita, watu mashuhuri pamoja na viongozi wetu mbali mbali wanaopita kufanya kazi zao za kila siku. Lakini hata sisi wenyewe wananchi pia wakati inakuwa haina mvuto sambamba na hili pawe pana mkakati maalum kwa ajili ya kuhakisha hasa wakina mama wanapata maeneo ya kuweza kujisaidia.

Mhe. Mwenyekiti, leo nimemsikia Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa akilalamika sana juu ya akina mama wanapotoka bandarini, lakini hata hivyo kutoka bandarini mpaka ufike katika vituo vya daladala hakuna sehemu ya kwenda pahala mtu kujisaidia. Pia tabia mbovu ambayo hujitokeza mara nyengine hasa kwa sisi wanaume kusimama maeneo ya kando ya barabara basi faini zianze kuwekwa, kwa sababu haipendezi kabisa mtu wa

kiume anasimama kando ya barabara wakati pembeni kuna wanafunzi wanapita akionesha utupu wake huku akijisaidia inakuwa ni kibaya sana. (*Makofi*).

Kwa hiyo, mambo haya kutokana na ukosefu wa maeneo ya kujisaidia kwa ajili ya kina dada zetu, mama zetu, vijana wetu basi yapangwe maeneo maalum kwa sababu ukiangalia Mkoa wa Mjini/Magharibi nafikiri ina watu zaidi ya laki sita, lakini watu ambao wanakuja mjini kufata huduma tofauti, kutoka Darajani mpaka utafika *round about* Kariakoo hakuna *public toilet*. Binadamu unakuja kule ushapiga maembe yako na ubwabwa wako wakati mwengine tumbo linataka kukupindukia, hodi hodi kwenye nyumba, mtu mwenye nyumba kafunga mlango, unataka kwenda sehemu nyengine unaambiwa maji hakuna. Sasa tuangalie maeneo haya japo iwe ya kulipia lakini hii ni sehemu ya kufanya ajira, utaona jambo dogo lakini choo kimoja mtu akilipa mia tano kwa siku ni biashara, basi zifunguliwe ili watu waanze kupata hii huduma. Na jambo hili ni kwa ajili ya wananchi wote na mwaka jana nilisema na mwaka huu narudia tena tunahitaji *public toilets* ziwekwe kwa ajili ya wananchi au serikali iweke utaratibu huu na isimamie.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo pia nataka nizungumze suala la *duplication of license* pamoja katika halmashauri zetu na serikali kuu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nashauri najua suala la leseni serikali imejipanga, lakini bado kuna mtihani katika maeneo tofauti baina ya Manispaa, Halmashauri zetu pamoja na Serikali Kuu. Mimi siku zote ninasema *license is the regulator* ni eneo moja la kumjua ni nani na nani, Ali yupo wapi, biashara yake *Juma Enterprises* au hoteli yake ipo wapi anajua wapi tutampata. Lakini leo kila taasisi ya serikali inataka kufanya sehemu ya leseni kuwa sehemu ya mapato. Sasa kama ni hivyo mwisho wa mwezi *ZRB* asiende kuchukua hizo *tax* zilizobakia kwa sababu ikiwa kila leseni unalipa mamilioni au fedha kibao kwa mwaka. Sasa huduma hii kwa mwananchi wa kawaida tunamsaidiaje.

Tunaweza tukaangalia huko chini katika maduka madogo madogo, mjini mpaka leo kuna leseni mtu atakata leseni ya duka kwa Manispaa lakini atakata pia ya Kamisheni ya Utalii. Hebu tukaeni kwa pamoja kuangalia afueni kwa ajili ya wananchi *as licensing* iwe sehemu ya kumtambua tu mtu sio sehemu ya kutengenezea fedha. Mimi nampongeza sana Mhe. Haroun Ali Suleiman ukienda mpaka leo *work permit* yake wakati alipokuwa waziri wa *labor* iko pale pale kaiweka, kwa sababu anatumia njia ile kufanya ni *facilitation fees* sio eneo la kuongeza mapato. Ni eneo la kumtambua na kumtambua yule mfanyabiashara na mwenyewe yuko wapi. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia hizi halmashauri zetu zinapokwenda kupiga hodi hodi katika maeneo unakuta katika mahoteli huko Kaskazini wanaingia viongozi wa serikali saa saba na nusu mchana watu wanataka kutoa huduma ya chakula, Disemba, 25 ni Krismas mtu wa serikali unakwenda pale unatarajia yule mtu ataweza kukuona, anatakiwa atoe *service* kwa mgeni ambaye anayemlipa. Mimi naomba sana wale ambao watakuwa na ziara katika mahoteli wapeleke barua ili pale wanapokwenda yule mtu anayewatarajia sio wanakwenda wanapiga hodi leo watakwenda *Labor Officer*, kesho atakwenda mtu wa halmashauri, kesho mtu wa *ZSSF*, hawa wawekezaji na wafanyabiashara hawako hapo kukimbia, wako hapa kufanya biashara ili iwe ni *win-win situation* kwa serikali pamoja na wao wenyewe. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba unapotaka kwenda kupiga hizi hodi katika mahoteli na biashara yoyote hata Kiwanda cha Maji, mtu apeleke barua aseme kesho saa nne, saa tano kuna wakati wa kazi, ndio maana hata wafanyabiashara hawendi katika ofisi ya serikali saa kumi za jioni kwa sababu ofisi zinakuwa zimeshafungwa. Inakuwaje mtu anakwenda saa nane za mchana wakati yule mtu anatoa huduma, *time* za kazi kwa serikali ziwe baina ya saa nne na saa sita pengine saa tisa na kumi au apange *appointment*, itasaidia vizuri kuleta umoja baina ya

wafanyabiashara na wote kwa pamoja. Mimi naamini kule Nungwi Mhe. Mwakilishi ambaye anajua ameshapata hizi kero nyingi ambazo anazisikia na naamini atakuja kuzisema baadae.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nataka nizungumze katika ripoti ya mwaka jana juu ya kamati hii husika. Ukiangalia kwenye ukurasa wa 25 hii ripoti ya 2017 walizungumzia juu ya changamoto juu ya hatimiliki kwa ajili ya vikosi vyetu hivi. Ukiangalia kwenye ukurasa wa 25 mwaka jana inasema kwa upande wa Chuo cha Mafunzo ina jumla ya kambi kumi na hadi sasa tayari kimeshayapima maeneo yake matatu ambayo ni Hanyegwa mchana, Langoni, Kinumoshi hadi sasa utaratibu wa kuzipatia hatimiliki kambi hizo zinaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kwamba kazi iendelee na utiliwe mkazo kuhakikisha kwamba kambi zetu zote mwaka huu *inshaallah* zinamalizika zote wapate hatimiliki zao na wanakuwa tayari wao wamejipanga.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nizungumzie suala la nyaraka, limegusiwa leo asubuhi na ofisi mpya ambayo inajengwa Koani nafikiri Mnadhimu alilitaja hili. Mhe. Mwenyekiti, katika suala la nyaraka naomba sana tujipange kuhakikisha kwamba nyaraka zetu kuna sehemu ya *digital*, *electronic* na kuna *paper*. Lakini pia katika picha zetu za viongozi na kumbukumbu ambazo ni za kihistoria. Kwa hiyo, nyaraka zetu zote maeneo yatakayowekwa madawa yao tujipange vizuri sana kwa sababu kitu cha leo utakiona hakina thamani, lakini kitu ambacho baada ya miaka kadhaa kitakuwa kina historia kubwa sana. Kwa hiyo, mimi naomba sana hili suala la *electronic* tuangalie na bajeti pia ipangiwe na wapate zile zote wanastahiki ili kuhakikisha kwamba wao wanapata.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nizungumze soko la Unguja Ukuu Kaibona. Mhe. Mwenyekiti, tangu nimeingia Baraza hili

nimekuwa nauza wazo la solo la Kaibona. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi barabara imekamilika kutoka Kaibona kwenda zake mpaka Cheju, eneo lile tunafahamu kama ni la wapiganaji wetu, Mhe. Waziri mwaka jana katika bajeti alizungumza moja kwa moja hapa na nakumbuka namnukuu maneno yake. Alisema, "anawaelekeza uongozi wa Wilaya pamoja na Mkuu wa Wilaya wakae pamoja Kamati ya Ulinzi na Usalama ili kwenda kuonesha ni eneo lipi ambalo tunaliangalia *process* ianze".

Mimi naomba sana na mimi kwa upande wangu tayari nimejipanga tunae mzalendo Bi. Fatma Kara ameanza michoro. Mimi naomba sasa uongozi wa Wilaya uzidi kumfanyia atilie mkazo Mhe. Waziri na naamini anajua kwa ajili ya wananchi wa Mkoa wa Kusini pamoja na Jimbo la Tunguu na maeneo jirani kule kwa Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) pia watawaweza kuleta huduma zao katika soko la pamoja la ujirani mwema kuwaunganisha wananchi wa Mkoa wa Kusini katika maeneo ili tuweze kusogeza huduma za wananchi kutoka *cement*, samaki, vyakula, siku kuu ili nao watu wa Mkoa wa Kusini waanze kujiona na wao wako kama Ulaya na pia wako kama Mkoa wa Mjini/Magharibi.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, chengine nataka nizungumze suala la Masheikh wetu na Ofisi ya Mufti. Mimi nashauri sana Mhe. Mwenyekiti mambo ya Dini na mambo ya siasa tujaribu sana kuyatafautisha na Mhe. Waziri kwa sababu yeye ni mtaratibu, ni mtu mwenye hekma, ni mzoefu Maalim Haroun Ali Suleiman. Yeye ni mtu mmoja ambaye anaheshimika sana hapa Zanzibar na ana uwezo wa kuzungumza na mtu yeyote, popote, wakati wowote *regardless* kwamba yule mtu ana chama yuko kwenye siasa au hayupo kwenye siasa. Mimi naomba sana ili kudumisha amani na umoja wetu Mhe. Haroun Ali Suleiman azidi kutilia mkazo kwa viongozi wetu wa Dini kuleta umoja, haipendezi kabisa pale panapotokezea mtu anafunga ndoa unakuta kiongozi wa Dini anapachika maneno kidogo ya kisiasa yanakuwa hayana

mvuto. Pale mtu anapofunga ndoa ni wakati wa kumtakia na kuibariki ile ndoa watu wajenge umoja wao, waweze kuishi kwa umoja na amani, waweze kujenga upendo katika familia zao na pia kuwatakia watoto ambao wengi kwa maisha yao Mwenyezi Mungu atakaowajaalia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana na katika maeneo haya ni sehemu ambayo tunaweza tukajikuta tunakwenda pahala sipo. Kwa hiyo, umoja wetu wa Zanzibar ambao Mwenyezi Mungu ametujaalia tuachie kazi ya siasa wale wanaopenda kufanya siasa. Kuna yule ambaye anataka kufanya mambo ya siasa basi kuna vyama vya siasa ajiingize huko, viongozi wetu washike upande wao na wale ambao wamo ndani ya serikali. Kama sisi ukituangalia Mhe. Mwenyekiti, kuna mawaziri mbele ambao ni serikali na sisi huku nyuma ni Wawakilishi tunaitwa ma-*backbenchers* ni Wawakilishi wa wananchi. Kazi yetu sisi kwa mujibu wa Katiba ni kuishauri serikali. Sasa mambo kama haya na huku nje yaendelee kutolewa elimu ili umoja huu wa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba tuzidi kushikana kwa pamoja na tuwe tuna umoja wetu kwa milele na miaka inayokuja mbele.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe muda wako umemaliza.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa nafasi uliyonipa na niwashukuru Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi na Waheshimiwa Mawaziri na Kamati yote waliohusika katika kuleta hii ripoti nasema ahsanteni sana kwa kunisikiliza.(*Makofi*).

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza tumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia jioni hii kukutana hapa tukiwa katika hali ya uzima na wale wenzetu ambao sasa hivi wapo katika kitanda ni wagonjwa basi Mwenyezi

Mungu awape nafuu ili waweze kuendelea na kazi zao za ujenzi wa taifa. Na wale ambao Mwenyezi Mungu keshawachukua basi aziweke roho zao peponi, Amin.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo kwanza nimshukuru kabisa Mwenyekiti wa Kamati pamoja na watendaji wake kwa jinsi walivyoandaa ripoti yao na jinsi walivyotuletea hapa na sisi leo hii kuichangia katika maoni yetu mbali mbali.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze kwa dhati kabisa Mawaziri wa wizara hizi waliohusika, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Vikosi na wengineo ambao kwa kazi walioifanya ili kukamilisha ripoti hii. Kwa sababu kama si wao basi ripoti hii leo hapa ingekuwa haipo lakini kwa mwenendo wao waliouchukua pamoja na mwenyekiti shupavu na mahiri, leo ripoti hii hapa tunaichangia na kuona changamoto walizozitoa.

Aidha, mimi niwapongeze wizara hizi pamoja na maafisa wote wakiwemo Wakuu wa Mikoa kwa jinsi walivyoandaa ripoti hii kwa kutoa ule ukweli wenyewe, kwa sababu kama wangelificha basi ingelikuwa changamoto zao zisingeonekana.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, mimi nichangie kidogo, najua kwamba mawaziri tayari wameshaona changamoto katika ripoti na naamini kwamba watazikalia na kuzifanyia kazi na mwezi wa Septemba na sisi tutapata majibu yanayoridhisha.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna baadhi ya vifungu ambavyo nahisi kama hivi vifungu kama vitatekelezwa, yaani ninapendelea vitekelezwe kabla ya hii Septemba kufika kwa maoni yangu haya. Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa 20, kifungu cha 5 kukosekana kwa Mwanasheria kisiwani Pemba. Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli Pemba hivi sasa kuna Mahakama na hivi juzi juzi tulipitisha sheria hapa kwamba kutakuwa na baadhi ya makosa hayatakuwa na dhamana mpaka utakapomuona Jaji

Mkuu. Lakini naamini kwa sisi wa Pemba kule itabidi Jaji Mkuu uje umtafute huku.

Mhe. Mwenyekiti, lakini mpaka Mwanasheria na yeye anaomba kwamba Ofisi yake ya Mwanasheria Mkuu ifunguliwe kule ili yale masuala madogo madogo ya mtu kupata sheria zake na haki zake basi aweze kutekeleza kule kule kuliko kufatia hapa Kisiwani Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hujiuliza tutafatia mambo mangapi sisi wa Pemba hadi tufike hapa Unguja. Leo kule naamini kwamba makosa yanatendeka kwa sababu binadamu hakuna mkamilifu, makosa yanatendeka na yatataka dhamana, yanataka kuwa na mwanasheria lakini mheshimiwa bado tunaambiwa kwamba mwanasheria Pemba itakuwa hakuna, Jaji Mkuu Pemba itakuwa hakuna na ukimtafuta huyo basi lazima uje Unguja. Kwa hiyo, mimi napendekeza tu mheshimiwa ofisi yake na kule ifunguliwe ili haki za mwanasheria basi ziweze kupatikana.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nije katika ukurasa wa 41, kifungu cha 3 masuala ya maadili ya viongozi. Mhe. Mwenyekiti, karibuni tulijaza fomu hapa za kila kiongozi anatakiwa ajaze umiliki wa mali yake yeye na familia yake. Lakini mheshimiwa chakusikitisha ni kwamba mpaka wanapokwenda kamati kuna baadhi ya wahasibu na baadhi ya viongozi hawajajaza fomu hizo au hawajarejesha fomu hizi. Hii mheshimiwa au tuseme ndio ibn Kinana hawa, kwa sababu hizi fomu zina sheria zake, lakini mpaka kamati hii inakwenda na fomu wakati wake lakini bado fomu hizo hazijarejeshwa. Mheshimiwa inasikitisha sana na hususan hawa ndugu zetu baadhi ya wahasibu wanavyofahamika huku nje wanafahamika vibaya sana na leo kusikia kwamba fomu za maadili ambazo zinatakiwa zijazwe lakini mpaka leo hii hazijajazwa. Sasa mimi namuomba waziri hili suala aliangalie kila mtu anayeidharau sheria basi ahukumiwe kwa mujibu wa kosa lake analolifanya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya suala hilo nije katika ukurasa wa 75 masuala ya ugatuzi. Nafikiri sheria ya ugatuzi ilipitishwa hapa na tukasema kwamba kuna wizara tatu ambazo tutazitia katika ugatuzi. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Afya. Lakini pia masikitiko yangu Mheshimiwa wale ambao wamegatuliwa maafisa wale waliokwenda katika Halmashauri wamekwenda kama ni wafanyakazi wa Halmashauri hawakwenda kama wanaofanya kazi ya ugatuzi kutoka Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya au Wizara ya Kilimo. Kwa mfano Mheshimiwa unapokwenda katika Halmashauri anakwambia mimi nimeletewa mtu wa ugatuzi kutoka Wizara ya Elimu lakini kaja yeye tu hata kile chombo alichokuwa akikitumia Wizara ya Elimu kule kanyang'anywa kimewekwa kule kule. Sasa Mheshimiwa hebu tufikirie huu ni ugatuzi, yule kapewa adhabu au kenda kule kufanya kazi au kagatuliwa yeye pale.

Mhe. Mwenyekiti, naomba hili suala liangaliwe kama kweli tumeamua kwamba tunataka ugatuzi basi mtu anapohamishwa Wizara ya Elimu kwamba huyu ni Afisa wa Elimu kenda katika Halmashauri apewe na zana zake za kufanyia kazi. Inasikitisha Mheshimiwa, hivi sasa wale wanakwenda kama ni mayatima pale Halmashauri hata pa kukaa hawana, tumekwenda sisi tukawaona inasikitisha sana, haifanani na sheria tuliyoipitisha humu. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri hili suala alione na watu kama hawa Mheshimiwa wanapogatuliwa kule basi wende na kile ambacho wamegatuliwa kule sio wende kama hawana kazi ya kufanya pale ofisini.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika suala la madawa ya kulevya. Mimi nampongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi pamoja na Kamanda wa Polisi wa Mkoa huu, lakini vyuma vyake alivyovikaza barabara Pemba vimelegea. Natahadharisha kwamba Mheshimiwa saa hizi wauza madawa ya

kulevya wamekivamia Kisiwa cha Pemba. Kama juzi Mheshimiwa hujasikia katika kipindi cha redio cha Mawio basi watu wanne kutoka Kidongo Chekundu, Kikwajuni, Jang'ombe wamekamatwa Pemba kule wanauza madawa ya kulevya. Kwa hivyo, mimi nawatahadharisha Wakuu wa Mikoa wa Kisiwa cha Pemba kwamba tayari huku nati zimekaza Unguja na wao Pemba kule wakaze nati. Kwa sababu ndugu zetu wa Pemba waliokuwa hawajui kutumia unga huu, hivi sasa wana hatari kubwa sana, utamkuta kijana kakaa juu ya gogo la mvumo ukimuuliza uko wapi anakwambia niko Ulaya, lakini kumbe yuko Pujini au Vitongoji kakaa juu ya gogo la mvumo. Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Wakuu wa Mikoa wakaze sana ili masuala haya nayo Pemba iwe vile vile yana upungufu au yaondoke kabisa katika suala hilo.

Nikiondoka hapo nije katika suala la unyanyasaji. Mheshimiwa mimi siku zote hujiuliza hii mikoa yetu ya Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba imefikwa na maswahibu gani. Mheshimiwa huna siku utakayofungua katika Mawio usisikie mtu wa Kaskazini Pemba kabaka, mtu wa Kaskazini Unguja kabaka, hebu Mheshimiwa tuitafutieni dawa hii. Mheshimiwa mikoa hii miwili itafutiwe dawa.

Mikoa hii kihistoria ni mikoa ambayo ndimo wanamotoka Mashekhe wakubwa wa visiwa vya Unguja na Pemba. Ukija Kaskazini Pemba kule Sheikh Sharif Alawi ndiko anakotoka, Shekhe mkubwa wa Kisiwani Pemba na ukija huku Mashekhe wakubwa walikuwa tukiwasikia kwamba wanatoka Kisiwani sehemu za Tumbatu, leo kwa nini visiwa hivi, mikoa hii miwili iwe ni kikwazo kikubwa cha masuala ya unyanyasaji. Mheshimiwa tuangalie pana tatizo gani hapa lililotokezea. Mimi naomba kama ni kupungwa papungwe, kama ni uganga upigwe, kama ni dua isomwe, lakini mikoa hii ipo hatarini kwa masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu si mkubwa sana isipokuwa ni hizo sheria ambazo nimetaka zifuatiliwe. Baada ya hapo nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati hii kwa ripoti yake nzuri na naamini kwa mara nyengine nazo zitakuwa na ufanisi na mwelekeo kama wa kamati mbili zilizokwishasomwa.

Baada ya hayo naunga mkono ripoti hii asilimia mia moja ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa Shaibu. Sasa namwita Mhe. Husein Ibrahim Makungu akifuatiwa na Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kunipa nafasi hii kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Sheria ya Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu awali ya yote kufika hapa mchana huu au jioni hii tukiwa wazima wa afya. Lakini nimshukuru sana, nimpongeze, Mhe. Waziri na wizara yake yote hii na Naibu Waziri kwa kazi zao nzuri wanazofanya na kwa umakini wao mkubwa kabisa katika wizara hii. Pia nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti wa kamati hii Mhe. Machano Othman Said na makamu wake na wajumbe wote kwa kazi nzuri waliyoifanya kutuletea ripoti hii ya kamati ndani ya Baraza la Wawakilishi, kwa kweli nawapongeza sana kwa kazi yao nzuri. (*Makofi*).

Pia niwapongeze na niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mtoni kwa kunichagua kunileta hapa na kufanya yale ambayo yataleta maendeleo katika nchi yetu. Kwa hivyo nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Mtoni. Niwashukuru sana na niwapongeze Wakuu wa Mikoa wote watano katika Zanzibar yetu hii Mikoa mitatu ya Unguja na miwili ya Pemba, kwa kazi yao

nzuri kwa kujitahidi sana na mafanikio makubwa tumeyaona katika ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianzie hapa niwapongeze kwanza vikosi vyetu vyote hivi vya ulinzi hasa ukiangalia KMKM, hawa ndugu zetu wa Jeshi la Kujenga Uchumi, Chuo cha Mafunzo na Valantia. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana na tuwapongeze sana hawa ndugu zetu wa vikosi kwa kujitahidi sana kuwa usiku kucha na mchana kufanya ulinzi na shughuli mbali mbali za kiuchumi katika nchi yetu. Kwa kweli nawapongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwenye ripoto hii ya kamati ukurasa wa 97 wa kamati yetu hii ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi. Nianze kwenye changamoto kubwa ya ndugu zetu hawa wa KMKM. KMKM wanafanya kazi kubwa sana na kwa shughuli zao muhimu hasa kwenye maeneo yao, lakini angalia kwenye changamoto ya ripoti ya kamati ukosefu mkubwa wa maeneo kwa shughuli zao hatimiliki.

Mhe. Mwenyekiti, hili tatizo sio kubwa kwetu sisi, sasa mimi namuomba sana Mhe. Waziri hili suala ni letu haya maeneo yao ya ulinzi hawa ndugu zetu tuwape hatimiliki haraka iwezekanavyo. Kwa sababu maeneo wanayokaa hawajui kesho tutakuwaje. Kwa hivyo, naomba sana tuwajaalie au tuwafanyie wapate hizi hatimiliki katika maeneo yao.

Jambo jengine niseme ukosefu katika baadhi ya kambi zao maji safi na salama. Mheshimiwa hili jambo limekuwa kubwa kidogo, tangu ripoti ile suala hili linakuja kwa ndugu zetu wa KMKM. Kwa hivyo, mimi naomba tujitahidi kuwapatia maji safi na salama kwani bila ya maji hakuna maendeleo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 73 wa ripoti ya kamati katika changamoto Mkoa wa Kaskazini Unguja. Mimi nisikitike sana Mkoa wa Kaskazini Unguja kuna changamoto nyingi ripoti

imetueleza namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati kutuletea hizi changamoto. Mkoa wa Kaskazini Unguja kuna changamoto mbali mbali na nyingi na muhimu sana katika nchi yetu, tunatakiwa tuziondoshe au itakuwa hatari kubwa sana. Kutokuwepo ulinzi wa uhakika katika maeneo ya utalii hili jambo ni kubwa na kama tunavyojua sisi utalii ni uti wetu wa mgongo wa nchi yetu, leo watalii wanakuja kutoka nchi mbali mbali na wana uwezo wanakuja kutembea kwa amani na utulivu ulioko katika nchi hii.

Sasa kama hamna ulinzi hili litakuwa tatizo. Sasa naomba sana hawa vikosi vyetu tuliokuwanao tuwatumie kwenye ulinzi katika hoteli za kitalii. Kwa sababu hili eneo la kitalii tunapata kodi nyingi sana hapa Mheshimiwa, sasa mgeni mmoja akiibiwa au akipigwa na mtu yeyote hujui kila mtu na nia yake kwenye nchi hii, lakini athari yake inakuwa kubwa huko duniani. Kwa hivyo, mimi naomba sana ulinzi muhimu hasa kipindi kinachokuja hiki cha utalii mwezi wa Juni kwenda mbele, tujipange tuwasaidie hawa wawekezaji kwanza tuwape ulinzi wetu wa ndani ili hata wale watalii watapokuja watakuwa na amani na utulivu kutumia pesa zao na kustarehe kwenye kisiwa chetu hiki cha Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba niendelee kwenye changamoto nyengine katika Mkoa wa Kaskazini kuongezeka kushamiri, maana yake kushamiri kunaendelea kama kitu kinaota vile, kushamiri vitendo vya udhalilishaji wanawake na watoto. Hili ni tatizo kubwa na ukiangalia kwenye vyombo vya habari mara nyingi ukisoma udhalilishaji Kaskazini umekuwa hauchukui muda unasikia udhalilishaji watoto na wanawake. Sasa mimi naomba sana serikali yetu sikivu ipo, tunae Rais makini sana hataki mambo haya, tunae Makamu wa Rais makini sana, waziri wetu makini na serikali yote kuwa makini. Mimi naiamini sana kwa nini tusikomeshe haya mambo, kwa sababu mara nyingi tumeshaona kwenye ripoti au kwenye kesi udhalilishaji unafanyika kwa mtoto mdogo miaka minne, anayefanya

anajulikana huyu hapa lakini ushahidi unaambiwa haujakamilika.(*Makofi*)

Sasa Mheshimiwa hapa tunataka ushahidi gani tena. Jambo mtu kafanya lazima apate adhabu iwe onyo kwa wengine, leo mtoto wa miaka minne ukimharibu kweli kuna taifa gani huko mbele. Kwa hivyo mimi nasema sana Mkoa wa Kaskazini na mikoa mengine yote lakini Kaskazini naona kwenye ripoti ya kamati wameeleza kabisa, wametwambia ukweli kabisa hili jambo lipo kubwa na linakua siku hadi siku. Kwa hivyo mimi naomba tuliangalie sana hili suala la udhalilishaji katika Mkoa huu wa Kaskazini.

Jambo jengine pia katika Mkoa wa Kaskazini uhaba wa maji. Mheshimiwa katika mkoa unaoingiza fedha nyingi sana katika kodi ya nchi hii ni Mkoa wa Kaskazini. Sasa mimi naomba suala la maji safi na salama tufanye kila njia, serikali imejitahidi imeweka *tank* pale la lita 100,000 ukifika karibu ya Nungwi pale Kidoti kwa mbele. Lakini pia maji hayapatikani sijui kuna tatizo la miundombinu au vipi. Naomba Mhe. Waziri pia aliangalie Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira suala hili la maji ni muhimu kwa sababu hao watalii na wawekezaji wanaokuja kama hamna maji hata uwekezaji wao unakuwa kidogo wa kusuasua. Kwa hivyo, naomba hili tuliangalie.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine kwenye changamoto ukitizama kwenye nchi yetu hasa Kaskazini huu uhaba wa walimu hasa wa sayansi na hesabati na katika nchi yetu upo sana, lakini Kaskazini wametuelezea wazi wazi wana changamoto hii kubwa ya skuli za msingi na sekondari pamoja na utoro kwa wanafunzi wa Mkoa huo, yaani kushamiri ule utoro umekuwa mkubwa sasa. Sasa mimi naomba sana jamani hili suala la Kaskazini tuliangalie sana kuangalia katika hili suala la walimu wa sayansi ili tuweze kusaidia hawa wanafunzi wapate kusoma vizuri.

Pia niseme katika changamoto kushamiri katika migogoro ya ardhi, bado migogoro ya ardhi kwa nini iwe hivi kila siku haishi katika nchi hii. Kuna mambo mengi ya teknolojia sasa hivi ya mambo ya ardhi na mengine, lakini bado matatizo haya yapo. Sasa mimi naomba tu, changamoto hizi Mheshimiwa ripoti ya kamati ya mwakani iwe haipo tena, kila mwaka migogoro ya ardhi Kaskazini inakuwa nambari moja. Mimi naomba tuangalie sana.

Jambo jengine pia tuangalie miundombinu ya umeme, barabara pia Kaskazini bado na nasema mkoa ule unaingiza fedha nyingi kwa serikali, kodi zote za watalii hoteli kubwa ziko kule. Kwa hiyo, mimi naomba sana suala hili la barabara na maji safi na salama yapatikane kwa uhakika Mheshimiwa kwa sababu jambo muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sasa naomba niingie katika Mkoa wa Mjini/Magharibi kwa sababu nimeelezea Mkoa wa Kaskazini changamoto zake, kuna changamorto nyingi lakini ukiangalia Mkoa wa Mjini/Magharibi ni mkoa ambao ni sura ya Zanzibar. Sasa ukiangalia kwenye ripoti hii ya kamati yetu iliyoletwa na Mhe. Mwenyekiti katika mafanikio ya Mkoa wa Mjini/Magharibi tunayaona hapa kwenye ripoti. Mimi nampongeza mwenyekiti kwa ripoti yake nzuri na ya ukweli na uwazi kabisa, lakini ukisema jambo la mwanzo katika Mkoa wa Mjini/Magharibi kupungua kwa migogoro ya ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo la kupigiwa mfano, hapa ripoti ya nyuma ilipoletwa kulikuwa na migogoro mingi ya ardhi Mkoa wa Mjini/Magharibi, lakini sasa hivi kwenye ripoti hii imepungua na nimpongeze sana Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi kwa kazi yake aliyoifanya nzuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tuangalie ripoti inavyosema na ripoti imekuja ya ukweli na uwazi kwa nini tusipongeze, lakini Mkoa wa

Kaskazini mambo haya yako mengi sasa tusaidie na Mkoa wa Kaskazini mambo yapungue sasa hivi. Kwa kweli mafanikio ya Mkoa wa Mjini/Magharibi nashukuru na napongeza kwa sababu Mkoa huo ni sura ya Zanzibar. Mtalii yeyote akija hapa leo kwanza anafika Mkoa wa Mjini/Magharibi, akiona mkoa huu una mashaka au haujatulia ataondoka siku ya pili. Kwa hivyo, mimi nasema nampongeza Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi kwa kazi yake nzuri kupunguza hili suala la migogoro ya ardhi.

Jambo jengine pia Mkoa wa Mjini/Magharibi katika mafanikio makubwa yaliyoweza kufanikiwa kudhibiti ulinzi na usalama kwa raia na mali zao, hili jambo ni muhimu sana. Nimpongeze sana Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi kwa kazi zake anazozifanya. Mheshimiwa niseme mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni hii kazi kafanya nzuri, bila ya usalama nchi hii bila ya ulinzi hatuwezi kuwa na amani sisi na hawezi kuja mtalii hata mmoja hapa. Kwa hivyo, mimi nimpongeze kwa mafanikio yaliyopatikana katika Mkoa wetu wa Mjini/Magharibi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine Mkoa wa Mjini/Magharibi ukiangalia karibu asilimia 47 ya watu wa Zanzibar nzima wanaishi hapa katika Mkoa huu, yaani karibu kuna watu 593,000 karibu 600,000 katika Mkoa wa Mjini/Magharibi. Ni kazi kubwa ambayo inafanywa na Mkuu wa Mkoa wetu wa Mjini/Magharibi. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia Zanzibar nzima katika mkoa wanaoishi watu wengi ni mkoa huu. Mimi mwenyewe naishi katika mkoa huu, jimbo langu liko katika mkoa huu, lakini ukitizama hii kazi sio ndogo inayofanywa.(*Makofi*).

Mambo mengine tukisema hapa ukiangalia mimi juzi nilikuwa katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Jumatatu/Jumanne, nilikaa pale Mheshimiwa ile ofisi yake ndogo halafu anapokea wageni wengi sana kutoka Kaskazini, Kusini, kutoka sehemu mbali mbali ile ofisi ndogo. Mimi nimekaa pale mpaka saa mbili na nusu usiku mimi mwenyewe nikawa namuonea huruma Mkuu wa Mkoa, kazi

anazozifanya huyu binadamu kweli au roboti huyu? Kwa sababu anazungumza na watu wengi shida mbali mbali lakini ile ofisi ndogo imekaa pale ina makochi matatu, manne. Sasa naomba serikali iangalie lile jengo liongezwe au ofisi ipanuliwe.

Pia ukiangalia jambo jengine katika ripoti ya kamati imesema pia ukosefu wa majengo, hasa ya Wilaya ya Mjini na Magharibi. Mhe. Mkuu wa Wilaya pia hana jengo zuri, tuangalie sana jengo lake pia Wilaya ya Mjini, Mkuu wa Wilaya kidogo ana jengo zuri, lakini ukitazama Mkoa wa Mjini/Magharibi ambako natoka mimi wilaya yangu jengo la Mkuu wa Mkoa wetu hamna jengo, uhaba wa jengo. Sasa ukiangalia Mkuu wa Mkoa wetu pia jengo lake dogo, lakini Wilaya ya Magharibi jengo lenyewe yaani pia ukosefu wa jengo. Kwa hivyo, naomba sana tuangalie Mhe. Waziri awape kipaumbele sana ndugu zetu hawa waweze kufanya kazi. Kwa sababu sasa hivi kama tunavyojua haya madaraka wamepewa wenzetu Wakuu wa Mikoa kufanya kazi, lakini kama hawajapata majengo mazuri, kufanya kazi wao vizuri, wakapata vitendea kazi vizuri kama gari, lazima wawe na gari kwa sababu serikali yote imehamia pale huu ni ugatuzi kutoka Serikali Kuu. Mimi nasema hivyo kwa sababu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano pia ni Mjumbe wa TAMISEMI najua Wakuu wa Mikoa wanavyohangaika kule, kazi kubwa wanafanya na ofisi zao lakini nzuri kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, ukienda Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Paul Makonda ofisi nzuri huwezi kuamini ina kila kitu ndani. Sasa naomba na hawa Wakuu wa Mikoa wetu waangaliwe ofisi zao ziwe nzuri, wanafanya kazi kubwa kuwatumikia wananchi hasa Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi anakaa mpaka saa saba usiku ofisini anashughulikia wananchi shida zao. Hili jambo la kupigiwa mfano jamani lazima tuangalie ofisi yake pia iwe nzuri na mazingira mazuri ile hewa iliyokuwa pia ndogo haitoshi kwa binadamu, watu wanakuwa wengi sana. Kwa hivyo naomba tuangalie sana.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia niseme katika ripoti ya Mhe. Mwenyekiti wetu wa Kamati kasema pia ongezeko la kesi za udhalilishaji wanawake na watoto pia katika Mkoa wa Mjini/Magharibi ipo inazidi kuongezeka kama nilivyosema kule Kasikazini. Hii tuchukue hatua inayowezekana haraka sana, kwa sababu watoto wanaharibika tutakuwa na taifa gani watoto wakiharibika hivi na sio ubinadamu. Leo mimi nina mtoto wa miaka minne ninaye nikisikia kaharibika itakuwaje, inauma sana. Kwa hivyo, naiomba serikali ichukue hatua za ziada sasa kufungwa hao watu wanaofanya vitu kama hivyo, hata ushahidi wao ukikamilika kidogo tu basi ende zake tu afungwe miaka kumi au kumi na tano angalau ndio adhabu iwe ndogo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe muda wako umemalizika.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Mwenyekiti, japo dakika tatu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemalizika kuna wachangiaji wengine malizia.

Mhe. Ibrahim Mussa Makungu: Mhe. Mwenyekiti, mimi sijamaliza lakini naunga mkono asilimia mia kwa mia kwa ripoti hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukuwa nafasi hii kukushukuru kwa dhati kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, napenda vile vile kuiunga mkono ripoti hii ambayo iliyowasilishwa na Mhe. Machano Othman Saidi ambaye ni Mwenyekiti wa kamati wa wizara hizi mbili. Kwa kweli Mhe. Machano Othman Said katika ripoti yake alitumia sana hekma, busara na usikivu.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nizipongeze vile vile wizara zote mbili hizi kupitia mawaziri wake, wasaidizi wake watendaji wake wote wa wizara hizi kwa kazi kubwa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilisikiza sana na kuifahamu ripoti ya Mhe. Machano Othman Said kwamba changamoto zipo nyingi sana. Changamoto hizi Mhe. Mwenyekiti, kubwa ni fedha, tunakwenda tunazunguka lakini kubwa ufinyu wa bajeti, ufinyu wa mapato na fedha kwa jumla. Lakini kila tunachokipata naamini kinawafikia wananchi kupitia wizara hizi na wizara nyengine.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Machano Othaman Said katika ripoti yake amezungumza sehemu nyingi sana kaanza Afisi ya Mufti, Afisi ya Mufti Pemba suala la changamoto ya magari, kaingia kwenye suala la sheria, *DPP* mambo yote ni vitendea kazi. Na kweli Mhe. Mwenyekiti, tunaweza kuwa na watendaji wazuri lakini hawana vitendea kazi inakuwa ni ngumu na wala ile elimu yao hatuwezi kuipata. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia kupitia Afisi ya Mufti. Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar yetu tuna utamaduni wetu na kuna haja sisi Mwenyezi Mungu aliotujalia wafanyabiashara na wale ambao wenye uwezo kuona jinsi gani ya kuisaidia serikali na kuisaidia wizara kupitia Afisi ya Mufti kuweza kusaidia.

Mimi kwa kuanza naomba nitoe maoni yangu au mawazo yangu kwamba tuanze na kupata magari matano ya *double cab*in *four wheel drive* za kisasa kupitia Afisi ya Mufti kwa Mikao yote mitano Unguja na Pemba. Mhe. Mwenyekiti, nipo tayari kuchukuwa jukumu hili na kwa kushirikiana na Mhe. Mwenyekiti Machano Othman Said na wizara tunao ndugu zetu ambao wanahamu ya kuisaidia Zanzibar, ndugu zetu Saudi Arabia, UE, Dubai, Kuwait, Qatar na nchi nyengine za Kiarabu ambazo ninaamini kwa utamaduni wa Zanzibar hasa kwa jina la Zanzibar. Kwa hivyo, naomba kupitia Mwakilishi kwa kusaidiana na

serikali nipo tayari na nina hakika hilo linaweza kufanyika niandikiwe *paper* kupata magari matano *double* c*ab*in *four wheel drive* Afisi ya Mufti kwa ajili ya changamoto ya Mikoa mitano. Hili naweza nikashikirikiana na wizara yenyewe au Mhe. Machano Othman Said na nina hakika tatizo hili hata ndugu zetu za Saudia Arabia kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, sisi tuna *Public Relation* nzuri sana, kwa kihindi tunaita (*Pyara*) yaani mahusiano mazuri. (*Makofi*)

Kwa hivyo, mimi naamini tatizo hili hasa kwa ndugu zetu wa nchi wa Kiarabu wanaweza kutusaidia na hili jambo linaweza kuondoka. Lakini kuwepo na *paper* sisi tunahitaji halafu tunaweza kuwaambia wahisani hata wafanyabiashara, tuwatangazie wafanyabiashara jamani kuna Afisi ya Mufti, lete gari andika Raza si matangazo kazi ifanyike, ulimwengu huu *you scratch by your bag,* tuna *given and take* Mheshimiwa. (*Makofi*)

Kwa hivyo, Mheshimiwa sasa hivi wafanyabiashara kuna makampuni mbali mbali wanaweza kuweka *Logo* yao wameisaidia gari Afisi wa Mufti. Kwa hivyo, hilo si jambo ambalo hata ulimwenguni ndio inavyofanyika, Saudi Arabia tunawaambiwa *donated by Saudi Arabia United King* hili jambo linafanyika. Kwa hivyo Mheshimiwa peke yake hata tukitaja vifaa. Kwa hivyo, mimi nafikiri tuanze na hapa na naamini kwa sababu matatizo yote haya ni fedha Mhe. Mwenyekiti, mapungufu ya bajeti na wananchi wanategemea mambo mengi, kuna suala la barabara ya ndani, kuna suala la dawa, kuna suala la maji, kuna suala la kilimo na mengi mengineyo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naamini wizara hizi kwa kushirikiana na kiongozi wetu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Sisi si kama tunapenda haya matatizo yawepo, kwa hivyo changamoto lazima tutafute *when we the problem* lazima tutafute *solution and then you say what is next.* Kwa hivyo tatizo tutafute tatizo lenyewe vipi kulibali. Lakini

kwa kukaa kusema hatuwezi. Kwa hivyo, naomba serikali ikatumia watu maarufu watu ambao wanamvuto huko nje. Mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti, suala hili pamoja na mambo mengine yanaweza kutatulika.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nitoe wito kwa serikali na nitoe wito kwa wizara. Mheshimiwa nchi yetu haina Dini wala rangi wala kabila. Lakini kinachonisikisha sasa na naona huko tunakokwenda Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Uzini lakini mfanyabiashara, madhehebu yangu ni Shia. Mhe. Mwenyekiti, si zaidi ya Misikiti kama thalathini mpaka arubaini kwa kushirikiana na wenzangu na mimi mwenyewe kama Raza tuliojenga Unguja na Pemba. Lakini tunapojenga misikiti tuwaachie wenyewe watu wa vijijini. Lakini kumejitokeza tabia unajenga Msikiti unataka kumleta wewe Imamu, unataka kumleta wewe mnadi Adhana alaa! inakujaje. Mimi ni Shia Mheshimiwa na nimejenga Msikiti Mwangapwani, Mkokotoni. Msikiti wa kwanza sikumtafuta kiongozi wa Shia, mfanyakazi wa Shia wala mnadi wa Adhana wa Shia, nimewaachie wenyewe wahusika, *lailaha illah llah Muhamada Rasulullah*, wewe funga hapa na mimi nifunge hapa funga hapa nani bora tusubiri siku ya Kiama. (*Makofi*)

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba serikali na naomba sehemu ambayo wahisani wanataka kuja kujenga Misikiti waambiwe wazi jenga msikiti kokote, kuanzia Micheweni mpaka Nungwi ukishakumaliza basi *lailaha illah llah Muhamada Rasulullah*, ule Msikiti uendeshwe na wenyewe wanakijiji au wahusika. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ninachohofia sasa kuna tabia imejitokeza, mtu anajenga msikiti yule ambaye yuko kijijini naambiwa aah! nitakuletea mtu mimi mnadi wa Adhana, mkamata ufunguo, leo usalishe wewe, hapana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeliomba serikali na Afisi ya Mufti tusipotizama mambo haya tutakuja kugombanishwa na tutafika pahala si pazuri. Kwa hivyo, nitoe wito kwa serikali wahisani,

Waislamu sote tunapotaka kutoa *sadakatul- Jaria*, tunapotaka kutoa *Zakka* tuwaachie wahusika wenyewe, kama wana shida ya Msikiti wajengee, maliza Msikiti nenda zako.(Makofi).

Mhe. Mwenyekiti, tusipoangalia leo tuna vijana mtu anaingia kwenye ndani ya kibla humjui katoka chuo gani, kasoma wapi. Sasa hivi Mheshimiwa tusipokuwa na tahadhari na Afisi ya Mufti, Afisi ya Kadhi na Wizara yenyewe Mheshimiwa naona kutokana na umaskini tutagombanishwa, sisi watu wa aina moja tumekaa aina moja.

Kwa hivyo, ninachoomba sana kutoa msisitizo kwa wizara hii kwamba dalili ya mvua ni mawingu tuwe na thadhari sana na vitu hivi ambavyo vinaweza kuleta mgawanyiko. Kwa hivyo, nataka kusema kwa viongozi kwa watendaji lazima tuwe wakweli. Kwa hivyo, hatukatai misaada yoyote na misaada yoyote kwa Zanzibar tunaipokea lakini isiwe na masharti. Mimi niombe hivyo tu. Kwa hivyo, niombe wizara, Afisi ya Mufti pamoja na Afisi ya Kadhi na wengine ambao wanataka kuchangia Madrassa, Misikiti na mambo mengine tuwe na tahadhari tunapotoa misaada kwa ndugu zetu tusiwaekee masharti. Hawa ndugu zetu vijijini sehemu nyengine waweze kufanikisha. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hilo nilikuwa ni ombi.

Lakini upande mwengine tuna mapungufu katika Afisi ya *DPP*, Afisi ya Mwanasheria na sehemu nyengine. Mimi nafikiri na hilo linawezekana kupata vyombo. Tuzungumze na ndugu zetu kutoka Denmark, Norway, Marekani na mimi naweza nikakusaidieni nina mahusiano nao mazuri. Denmark wanaweza wakatusaidia vyombo, wanaweza kusaidia vitu vingi. Kwa hivyo, lazima tujitume na tuone misaada iko mingi lakini lazima tujitume tutoke. Kwa hivyo, mie niko tayari kushirikiana na wizara na taasisi mie niko tayari kumwambie leo kupitia wizara Afisi ya Mufti, Katibu wa Muft Shekhe Mussa Soraga ni mtu msikivu, ni mtu ambaye anafahamu, nikenda naye Dar es Salam mimi kwa ubalozi kwa

gharama zangu kupitia Jimbo la Uzini kama nikiwa Muislamu, nikawachukuwa nikenda kuonana nao wala haina tatizo wala hatutaki tena suala la mambo haya ya kupigia huku hapana. Hili letu Zanzibar, kwa hivyo *we have own autonomy*.

Kwa hivyo, tusifike pahala tuseme tuweza kupata kibali tutapata kibali wapi wakati Zanzibar haya ndio matatizo tuliokuwa nayo. Lazima tuji-*expose* kwa wenzetu. Kwa hivyo, suala hili la magari, pikipiki Afisi ya *DPP*, Afisi ya Mwanasheria na sehemu nyengine tuwaendee ndugu zetu wa Denmark, Marekani, Uingereza na mimi niko tayari kukusaidieni na niko tayari kusimamia na nina hakika tutafanikiwa, tuandike *paper* mahitaji yetu yawe vyombo sio fedha na watatusaidia na tutaletewa vitu vyote huku Zanzibar.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi naona jambo kubwa sasa hivi tulilolizungumza hapa tatizo kubwa kwenye sehemu yote hii ni fedha bajeti. Kwa hivyo, tutakuwa na majengo, mambo mengine yote tatizo ni fedha. Rais wa Zanzibar anachokifanya tunachokitapa ndio tunachokitumia. Kwa hivyo, sisi tuhimize sasa wafanyabiashara na wananchi wabadilike kulipa kodi, hilo ndilo jambo muhimu sana kwa sababu Mheshimiwa mimi nina hakika bado kuna asilimia kubwa ya kodi tuna mapungufu Zanzibar.(*Makofi*).

Kwa hivyo, tuwe na tabia ya kuweza kukusanya mapato yetu ya kodi. Lakini leo kuna wafanyabishara wenyevitu wanadaiwa kwa mfano *Zanzibar Wharfage* au sehemu mbali mbali wameshatoa huduma, mahoteli yameshatoa huduma wanadaiwa zaidi ya mamilioni halafu tunawatizama, halafu utakuta mtu anatembea na gari ya milioni mia mbili huku ana deni na huku sisi Baraza la Wawakilishi wananchi wanapiga kelele. Kwa hivyo, lazima tuwe wakweli tutizame namna gani ya kuimarisha kodi zetu na kodi zetu Mheshimiwa *is not a big deal* huo ndio ukweli. Lakini lazima tubadilike tuwe na utamaduni wa kuwahimiza wananchi wetu dhana ya kulipa kodi. Kwa hivyo tukilipa kodi hizo huduma

ndio zinatafika. Kwa hivyo, Mwenyekiti mimi niombe kwamba hili litizamwe.

Lakini ukija upande wa Mhe. Waziri wa Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ. Mimi nipongeze sana wizara hii. Wizara hii ina changamoto nyingi sana na kwa kweli mimi niwasifu wizara hii pamoja na wizara hii iliyopita kwa uzalendo wao kwa vikosi vyetu vya Mafunzo, Valantia, KMKM, JKU kwa uzalendo na uchungu wa nchi Mheshimiwa unaja maisha ni magumu. Kwa hivyo, kazi iliyokuwepo kwa vikosi hivi si jambo dogo.

Kwa hivyo, niwapongeze Wakuu wa Mikoa yote, Wakuu wa Wilaya, Makatibu, Viongozi wote wa Vikosi wa Wizara hii kwa kazi kubwa ya uvumilivu na kuona uchungu wa nchi. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi katika mtazamo huo vile vile bado tuna kazi kubwa kuziunga mkono Halmashauri zetu, tuziunge mkono sehemu zote ili. Mhe. Mwenyekiti, tuna uwezo wa kukusanya leo kuna magari yanakuwa *parking* anakuja mama wewe una gari yako ya milioni kumi, milioni mia mbili anakwambia elfu moja lazima akufukuze. Mheshimiwa ni aibu sisi tatizo lote lililotoka sasa hivi Zanzibar ni maporomoko ya maadili Mhe. Mwenyekiti, hilo ndilo ambapo lipo sasa hivi Zanzibar.

Sasa *parking* umeshawekewa ulipe shilingi elfu halafu unaweza kukimbizana halafu sisi wananchi wanasema taka ziko nyingi sijui hili halijafanywa. Sasa wewe mwenyewe hutaki kutoa huduma towa huduma halafu useme. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri bado Halmashauri zote wanafanyakazi nzuri sehemu nzuri tutafute mbinu sasa ya kuweza kupata mapato zaidi, kwa sababu mie ninaona bado tuna mapungufu ya mapato wa kuweza kutusaidia, ma-*parking* yamekuwa mengi mtu akisimama pembeni kaweka anaweka gari pale pale.

Mhe. Mwenyekiti, Dar es Salaam sasa hivi umeweka pahala tu gari hata dakika moja ameshakutolea risiti elfu thalathini, Dar es

Salaam hapo tusizungumze nje. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikata barabara nilikuwa sijaiona ikaona *red line* nikakata barabara nilipigwa faini pale pale Dirham mia sita na *passport* yangu nikanyanganywa nikenda siku ya pili kulipa polisi Dubai. Sasa lazima tubadilike tuwe wakweli, lazima suala hili la watu kuheshimiana tuheshimiane tuvumiliane, tujiadiliane.

Lakini watu wanafanya wanavyotaka mtu kaweka *parking* unapata elfu thalathini. Mimi nafikiri waziri wa vikosi vyetu na hizi *parking* uzizidishe mtu kaweka muwekee risiti yake elfu tano mpige kamera kwa hizi simu siku ya pili akalipe halipi si unaweka gari pembeni sio ndio utaratibu. Kwa sababu huko huko tunapokwenda Mheshimiwa na huko huko ndio tunatukanwa. Sasa tunapokuja lazima tusaidiane tuone mapato haya tuna suala la watalii, kuna suala la hoteli .....

Mhe. Mwenyekitui: Mheshimiwa muda wako umemalizika.

Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali: Naam Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Muda wako umemalizika Mheshimiwa.

Mhe. Mohammdraza Hassanaali Mohamdali: Mimi Mheshimiwa nakushukuru sana na naunga mkono sehemu zote mbili Mwenyezi Mungu atujaalie Zanzibar yetu njema. Ahsante (*Makofi*)

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Sheria ya Utawala Bora na Idara Maalum.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mwenyekiti wa kamati hii na kamati yake yote kwa ujumla kwa kufanyakazi nzuri

wameibua changamoto nyingi, lakini ziko mbili tatu ambazo na sisi tunazielewa tunaweza tukazisema kwa nia ya kutengeneza.

Pili Mhe. Mwenyekiti, napenda nichukuwe nafasi hii kuwapongeza mawaziri wawili kwa maana ya kufuatana na ripoti hii mzee wangu mtiifu Mhe. Haji Omar Kheir na Mzee wangu msikivu Mhe. Haroun Ali Suleiman pamoja na mawaziri wote wanaofatana na taratibu za wizara hizi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba na mimi niungane na wale wanaliotangulia nitakuwa sikutenda haki katika sura ya mashirikiano na utekelezaji wa majumu yetu kama sikumpongeza Mkuu wangu wa Wilaya ya Mjini Mhe. Marina Joel Thomas kwa namna bora anayotushirikisha sisi viongozi katika kuteleza majukumu katika maeneo yetu, mara kwa mara amekuwa akitwita mimi na wenzangu kina Mhe. Rashid Makame Shamsi wanakumbuka tunaitwa katika utelezaji wa mambo mengi tu. Kwa hivyo, na mimi nampongeza sana na namwambia asichoke kwa sababu hii ni sehemu ya wajibu wake na sisi tutaendelea kumpa mashirikiano ili nchi yetu iende.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika Idara ya Muundo wa Taasisi ya Utumishi. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili limeelezwa vizuri na mimi nimeanza kuwapongeza wana kamati kwa sababu maandiko yote mazuri. Lakini katika eneo hili pia wameeleza muundo kazi wanazozifanya lakini bado kuna sehemu kubwa ya changamoto ambazo zimo ndani ya wizara zetu na wao kama ni wamiliki wa miundo ile lakini pia na utekelezaji wa yale mambo ya astahiki hasa za wafanyakazi wanazo wao. Liko tatizo lililokuwa linazungumzwa muda mrefu Wizara ya Elimu wako walimu katika mabadiliko yale hawakukumbana na nyongeza ile mpaka sasa hivi wanaenda wanarudi hata juzi sie kuna wengine tumefatana nao kwenda katika wizara hii ili kuona haki zao za msingi wanazipata.

Kwa hivyo, katika kuhakikisha utekelezaji bora mimi ningeomba tu Mhe. Mwenyekiti wa Kamati yako maeneo kama suala hilo la Wizara ya Elimu basi mbinu na utaratibu mbadala kwa kushughulikia ili kadhia hii ikapungua utaifahamu Mhe. Mwenyekiti. Lakini naomba kwa mara nyengine ushirikiane na taasisi ile basi utayapata mengine ambayo naamini kwa uhodari wa kamati na wizara hii yatatatuliwa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba pia niipongeze kamati katika mapitio ya ukurasa huu wa eneo hili, kuna ukaguzi umefanyika katika eneo la Pemba na zikatajwa hapa moja wapo ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Wizara ya Afya, lakini eneo hili ni zuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Unguja hakuna mapitio ya ukaguzi kama huu, kama umefanywa haukuripotiwa katika ripoti iliyopita, kwa sababu nilikuwa napitia awali ya ripoti hii. Sasa jambo hili ni zuri na malalamiko makubwa hasa Wizara ya Afya, katika ukaguzi kama huu uliofanyika wa kiutumishi na uwajibikaji yapo Unguja ambayo yanalalamikiwa kwa kupitia hospitali ya Mnazi Mmoja na vituo vyengine. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ningeomba katika kazi nzuri iliyofanywa na kamati kama eneo hili lilivyo, basi na eneo hilo wenzetu wale kwa makusudi muwaambie wachukuwe juhudi za kuyafikia maeneo hayo ili ile dhamira njema ya kuwatumikia wananchi iweze kutimia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nihamie katika Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba. Kuna kazi hapa imeripotiwa. Kwanza mimi naomba niipongeze hii ripoti katika eneo hili la Afisa Mdhamini, niipongeze kamati lakini nipongeze makusudi eneo hili la Afisa Mdhamini wa Katiba na Sheria Pemba. Katika utekelezaji wa majukumu yake na nampa pongezi, kwa sababu kuna idara maalum inapongeza sana juhudi za Ofisi Kuu Pemba kwa

kufanikiwa vyema kuratibu kikao cha ukusanyaji wa maoni ya wadau kuhusu muongozo wa usalama wa afya kazini, hili ni jambo jema sana. Katika ripoti hii kwenye maeneo kama ambavyo nililiripotia mapema, suala la afya kazini halikuzungumzwa katika utaratibu wa wizara na taasisi zetu zilizokuwepo hapa nalo ni suala muhimu, wenzetu wamefanya lakini katika programu zetu huku eneo la pili la upande wa Unguja halikufanyika.

Sasa niombe Mhe. Mwenyekiti, dhamira kama hii waliyotekeleza wenzetu basi na sisi katika eneo la Unguja kwa usalama wa wafanyakazi wetu basi elimu hii ishughulikiwe nayo. Lakini kuna changamoto katika eneo la pili, katika ofisi hii tatizo moja limeripotiwa la uchakavu wa vyombo vya usafiri na kisha kuna tatizo la kufanyakazi kwa mazowea. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba hapa na maazimio ya kamati au maagizo ya kamati yanasema, kamati inaagiza uongozi wa Ofisi Kuu Pemba kuhakikisha wanasimamia vya kutosha watumishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naungana na pendekezo hili, lakini na pendekezo jengine mara nyengine lililokuwa zuri zaidi ni kwamba, kama wameshakuwa wanafanyakazi kwa mazowea, hawa tayari wanasimamiwa na sehemu za utumishi zipo hatua sasa za kisheria zichukuliwe kwa watu wa aina hii, hatuwezi kuishi na watu wanafanyakazi kwa mazowea hadi sasa. Maoni nayakubali lakini na hatua zinazostahiki zichukuliwe.

Mhe. Mwenyekiti, nihamie katika changamoto za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kuna changamoto moja kwangu haikukaa vizuri, ni nzuri katika kuripotiwa lakini haikukaa vizuri inanipa mashaka sana, kwamba changamoto hii inatoa mashirikiano madogo kutoka katika wizara na taasisi mbali mbali kupelekea Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kushindwa pale panapokuwa na kesi. Sasa kukiripotiwa kuwa taasisi za serikali zinatoa ushirikiano mdogo katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wanategemea nini, muongozo wao wa kiutumishi unawaambia nini. Niseme ile jeuri

ya kiutendaji wanaipata wapi. Kwa hivyo, nasema watumishi wa aina hii, maana ikifika pahala kama Rais amemteuwa Mwanasheria Mkuu na kumuundia ofisi, maana yake huyu ndiye mwenye dhamana ya kesi za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa leo hii tunafika pahala tunaambiwa kwamba watu wamekosa mashirikiano, hao wenzetu katika ofisi nyengine tuwaelewe vipi sisi tukiwa ndani ya chombo hiki kitukufu. Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa napata mashaka sana na kama wapo hao watu Mhe. Mwenyekiti wa Kamati mara nyengine ungeomba kuwajua. Tukifika pahala tukinong'onezana katika kutekeleza maazimio haya basi tu haina haja ya kumtaja mtu, lakini tunapokaa katika vikao vyengine haiwezekani. Mwanasheria Mkuu ameteuliwa kwa kufuata taratibu zote, kaapa vizuri na ana viapo vingi lakini kaapa vizuri. Leo hii kuna watu wanataka kuhujumu serikali, maana yake kama kuna kesi hawawezi kwenda kutoa mashirikiano kwa misingi hii, hili ni tatizo kubwa kwa upande wangu.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda katika Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuna changamoto pale. Changamoto ya kwanza imeelezwa ya wafanyakazi, lakini changamoto ya pili ya kuna wakuu wa taasisi au na mawizara kutoshiriki katika mikutano ile ya kuingia na kutokea imeripotiwa hapa. Huu ni utaratibu ambao umewekwa kisheria, *CAG* anapoingia kwenda kufanya kazi zake ana mkutano wa kuingilia na anapotoka ana mkutano wa kutokea. Lakini changamoto moja ya *CAG* aliyoiripotia kwa kamati ni kuwa wale wenye taasisi wanakataa, sasa tunapata mashaka kweli, maana wakati mwengine unapopita katika taasisi wao wanakuambia *CAG* hafanyi hivi, lakini sasa leo kuwa *CAG* yeye anaripoti wale wakuu wa taasisi wanakataa. Sasa hili Mhe. Mwenyekiti, ni changamoto yetu pamoja, kwa sababu sisi kamati yetu katika utaratibu wa kufanyakazi tunalikuta hili sana, na wanasema hasa *CAG* anapoondoka hasemi, lakini leo *CAG* karipoti kuwa watu hawampi mashirikiano. Sasa hatujui

tumkamate nani sisi tulikuwa tunataka kuwakamata hawa watendaji wakuu wa serikali ambao wanakiuka utaratibu ule wa kufanya. Lakini sasa limekuja katika sura nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, sasa eneo la pili tulikuwa tuna changamoto ya wafanyakazi. Wafanyakazi Mhe. Waziri Haroun Ali aliwahi kujibu kuwa walikuwa wana tatizo la kupata mwenyekiti wa bodi tukapitisha sheria ikamtaja huyo mwenyekiti keshapatikana. Sasa sijui hiyo changamoto hii ya kumpata wafanyakazi ndio ile ile au ina sura nyengine. Mhe. Mwenyekiti, katika kufuatilia na kamati yako katika kuona hili suala linatatuka naomba, kwa sababu ahadi ya Mhe. Waziri ilishakuwepo, sasa bado yale mashirikiano ili tatizo hili litatuke. Lakini tutakuja kuwasikiliza sana mwezi wa tisa watakapoleta yale majibu, changamoto hii wataijibu vipi. Nafikiria Mhe. Waziri Haroun Ali mara hii hutakuja na kauli ile ya 'tuta', maana tuliisoma sana ile 'tutafanya', 'tutaweza'. Sasa mara hii tunafikiri hutakuja na kauli ile utekelezaji wa eneo hili la ajira utakuwa umekwenda vizuri.

Eneo jengine ni Mahakama Kuu. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili pia napo hapa zipo changamoto niwashukuru kamati wamezieleza, lakini changamoto Mwenyekiti wa Kamati hapa tulijadili mpaka kipindi cha bajeti, lakini ripoti ya kamati iliyopita wenzetu hawa Majaji walilalamika sana, wale Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, nisiseme Majaji. Kuhusu *scheme* yao mpaka mishahara yao hii, ukiwa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo wewe hata kama una digirii ya Pili maana yake mshahara wako utakuwa ndio huo huo, kwa sababu wewe unapewa kule kwa ule Uhakimu wako wa Mahakama ya Mwanzo, ile elimu haizingatiwi. Maana yake kakaa kama mtu ana *certificate* kawa Hakimu wa Mwanzo, hata kama mtu ana diploma kawa Hakimu wa Mwanzo na mwenye digirii, hawa wote walikuwa wanapata viwango vimoja. Sasa ikawa hapa pana tatizo kubwa katika kutekeleza ule muundo wa kiutumishi kwa kuzingatia maslahi ya mfanyakazi katika elimu, sio ile nafasi yake

au kada yake anayoitumia. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hii ni changamoto ya muda mrefu Mwenyekiti wa Kamati na haijatatuliwa, lakini naomba niipe tu kamati katika mchango wangu wa kawaida waweze nayo kuichukua ili iweze kutusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ni Ofisi ya *DPP* Pemba. Ofisi ya *DPP* Pemba kuna upungufu wa mkemia na hili ni tatizo, kwa sababu wamesema hapa upungufu wa mkemia kesi zinazokwenda mahakamani katika sura ya madawa ya kulevya zinazorota sana ni tatizo kubwa. Sasa mimi naiomba serikali kwenye eneo hili basi ihakikishe inalifanikisha kwa uharaka wake, kwa sababu inahusiana na uharibifu wa vijana wetu. Kwa hivyo, kama tunawadhibiti hawa, maana yake vijana wetu tutawalinda katika eneo jengine. Sasa leo hatuna mkemia kesi haziendi hakuna mtu anayehukumiwa, maana yake watu watakuwa wanajifanyia tu kiholela kitu ambacho sio dhamira ya serikali katika eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika Tume ya Maadili. Tume ya Maadili ya Viongozi na mimi katika changamoto moja kwanza niwashukuru sana Mwenyekiti wa Kamati na kamati yake, wameibua changamoto kubwa sana. Kuna mjumbe mwenzangu mmoja ameielezea sana, kuchelewa kwa baadhi ya viongozi katika urejeshaji wa fomu wengi wao wakiwa wahasibu au watu wengine wenye dhamana ya fedha. Mimi naomba niseme kwa sauti kubwa Mhe. Mwenyekiti, kwa nini watu wa aina hii tuwaripotie kwenye eneo hili ambao hawataki kurejesha fomu. Maana yake wanatupa hata na sisi kuwafikiria katika taswira nyengine. Hawa watu wote wako ndani ya milki ya Muhasibu Mkuu wa Serikali, kwa nini tusiripotiane na Muhasibu Mkuu wa Serikali, ikiwa hataki kujaza fomu aende tu, kwa nini hataki kujaza fomu anatupa mashaka katika utaratibu huu. Wewe ukishasoma uhasibu unapewa dhamana ya fedha hutaki kujaza fomu, unatupa mazingira yepi, maana hapa wameshatupa mazingira mapya ya kuanza kuwafikiria hata kama hawana sura ya aina hiyo.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti wa Kamati nakupongeza, lakini mimi niiombe serikali katika maagizo ya utekelezaji kwenye eneo hili mutuambie tu wameshajaza hizo fomu au mmewafukuza, maana lazima ifike pahala hivyo, kama hawataki wafukuzeni tu kwani hakuna wengine, huo ndio utaratibu ambao tumeuweka kisheria kama mimi najaza na wao wajaze.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, muda wako. Malizia.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kuna eneo moja muhimu la Idara Maalum. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo la Idara Maalum kwa umuhimu wake ipo changamoto nayo, Mwenyekiti wa Kamati naomba na hii nikukabidhi. Katika promotion za kuwapandisha vyeo wapiganaji wetu. Kuna vijana ambao wamemaliza kozi toka mwaka 2013 na wana digirii na wengine wana diploma lakini kuna vikosi vyengine Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu muda umekwisha naomba nikuletee kwa maandishi eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyenyekiti, kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Subiri. Naomba ukae Mhe. Mjumbe. Kabla sijampa nafasi Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Mhe. Shamata, nampa nafasi Mhe. Nadir Abdul-latif na yeye ni mjumbe wa kamati ili aweze kuchangia, baadae Mhe. Shamata

Shaame Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ atafuatia.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bismillah Rahman Rahiym*. Mhe. Mwenyenyekiti, nilikuinukia hilo hilo, maana yake ulikuwa umeshanikatalia. Nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi kwa sababu na mimi ningeongea machache kama mjumbe wa kamati. Sisi wengine kusema ukweli kuandika kwa kalamu kwenye karatasi hatuwezi, tumeshazowea kuongea hivi hivi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, nitaomba na mimi niichangie ripoti ya kamati ikiwa na mimi ni mjumbe wa kamati kwenye wizara hizi mbili. Lakini *concern* zangu ni ndogo tu, kama tulivyoeleza kwenye ripoti hii kwamba suala la Zimamoto, Vikosi KVZ na wengineo. Bila shaka kwanza niwapongeze mawaziri wote na Manaibu Waziri wao, watendaji wao, Makatibu Wakuu wao, Wakuu wa Vikosi, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa, kwa kweli wamekuwa na mapokezi mazuri na wamekuwa wawazi zaidi, unapotaka *information* basi wanatoa *information* ambazo ni za kweli na wamekuwa hawana uwoga tofauti na zamani. Zamani tunapokwenda sisi wanakuwa kidogo wanahisi kama tunawaonea, lakini *reality* kwamba tunataka tuwasaidie na nawashukuru sasa hivi wamefahamu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana viongozi kwa ujumla hata ukiwaangalia Waheshimiwa Mawaziri wenyewe wanakupa kitu *black* and *white* unapata kufahamu mnajua mnashauriana vipi. Ndio maana unakuta sasa hivi hata yale mambo ya kuwashughulikia kwa vitendo yanapungua, kwa sababu wako wawazi kila kitu kiko safi na kusema kweli wanajitahidi. Mimi kama mnavyonijua kwenye kazi huwa napenda kuwa nasema kweli na kuwazi wanafanyakazi vizuri, kwa sababu wizara zetu sisi naweza kusema humu kweli kila wizara ina majukumu yake, lakini wizara mbili hizi nzito kweli.

Mimi mwenyewe hapa naomba hii kamati hasa nihamishwe majukumu mazito, sikuambii wao wenye wizara.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi ningemuomba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ angalau akatafuta gari jipya lile la kuzima moto la ghorofa linaloweza kuzima katika ghorofa ya tano au ya saba, Zanzibar tunalo moja lakini ni chakavu kweli kweli. Sasa hivi serikali yetu tumeona tunataka maendeleo majumba ya maghorofa mengi yanajengwa, likija kutokezea janga la moto itakuwa ni mtihani kwa gari lile moja kulitegemea. Kwa hivyo, ningeomba wizara yake ifikirie angalau kwa Mkoa wa Mjini yawepo angalau mawili au ukosefu moja, ambapo gari la zimamoto litakaloweza kufika gharofa ya saba mpaka ya nane.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi nimpe taarifa kwamba nchi ya China wametoa *fire fitter* mpya, yenye ngazi za mita 120 kwenda juu, naamini ghorofa mpaka 13 au 14 wataweza kuzima na bei zao ni *reasonable* kabisa. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri wangekwenda kufanya ziara nchini China, ili wakaona ile bei ikiwezekana hata wazungumze na serikali wakope au kama wana *cash* walipe, lakini gari la zimamoto lenye kuweza kuzima sehemu za maghorofa ya mbali liwepo.

Kwa mfano, tumeona hapa Mbweni kuna maghorofa zaidi ya kumi yanajengwa sasa hivi ya ghorofa kama saba au sita litaweza kusaidia. Vile vile zimamoto wao hawana sehemu maalum ya suala la maji *Airport*, litakapokuja kutokezea tatizo watakuja kulaumiwa. Kwa hivyo, ningeomba wizara ichukuwe hatua za jitihada kabisa ili waweze kupatiwa bwawa lao na mashine zao za maji, ili waweze kufanyakazi kwa vizuri.

Vile vile zimamoto wamelalamika sana kwamba *safety fee* hawapewi inayolipwa *Airport*, hasa wale *passengers* kwenye *set* ya *passengers*, kila *set* inalipiwa *safety fee*. *Airport* wanachukua

peke yao hawawapatii hawa zimamoto, wangekuwa wanapatiwa asilimia yao basi wangepungua matatizo kwa upande wao ya kuomba na kukaa bila ya kupata matumizi mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende kwenye KVZ. Kusema kweli tumekwenda tumetembea wanafanya kazi nzuri ya kutengeneza viatu vya majeshi na hata watu binafsi wakitaka wanauziwa viatu *high standard quality*, vizuri na bei yao *very reasonable.* Ningependa kuwapongeza sana wizara kwa kupitia uongozi wa KVZ, kuweza kumpa mzalendo kuweza kujenga kwanda kile ambacho kimejengwa sasa hivi kitakuja kuwa nafikiri cha nguo pamoja na viatu na mambo mengine. Kiwanda kile kimejengwa chini ya muda, muda aliopangiwa pia kajitahidi kajenga kabla.

Kiwanda ambacho kajenga mwenzetu ningeomba wizara wamfikirie na wazidi kumpatia kazi nyengine kutokana na kazi nzuri aliyoifanya. Kuna mambo mengine kayaongeza hata hayamo kwenye hesabu kayaongeza mwenyewe. Hata ukiangalia *tiles* alizotia hata zile za *ZRB* hazijatiwa *tiles* kama alizotia yeye kwenye kiwanda kile. Mimi nampongeza ni mwenzetu na mimi napenda wenzetu wafanikiwe sitaki kuona kila siku wanakuja watu kutoka nje kutoka Kenya, kutoka ulaya au kutoka pande nyengine wanapewa kazi. Kazi kama hizi ndogo ndogo tunaziweza Wazanzibari wapewe kama hizi, kazi kubwa za maghorofa mengi watafutwe wengine wenye uzoefu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri kwa kupitia wizara yake ningeomba wazalendo awape kipaumbele kama alivyompa huyu mzalendo ambaye aliyejenga kiwanda kile.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niende kwenye vikosi kwa ujumla. Mimi ningemshauri Mhe. Waziri kwamba kila mkoa angalau wangekuwa wale vikosi, wana *ambulance* yao, gari la kubebea wagonjwa kwa ajili yao wenyewe binafsi, kila mkoa angalau liwepo moja, kwa mikoa mitano liwekwe moja kwa ajili ya vikosi tu. Isiwe limetokea tatizo wanaanza kutafuta ya majimbo au

wanatafuta ya majeshi au kuazima ya ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo, ningeomba anunuwe kwa kuwa sio ghali na hasa akienda kununua nje hayana bei ya kutisha kwamba serikali ishindwe, huo ni ushauri wangu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ningetoa ushauri kwenye wizara hii hii kwa ujumla Masheha wote ambao wanashiriki kwa njia yoyote ile kutapeli watu viwanja, kuingia kwenye masuala ya utapeli wakati wanajua. Kwa mfano, kamati ilikwenda wapi kule, Ndagoni, Sheha anagombana na watu. Haiwezekani Sheha wewe ukawa dalali wa kiwanja, haiwezekani Sheha wewe ukawa dalali wa kiwanja, haiwezekani Masheha wa sehemu tofauti ikawa nyinyi, ndio tena mumefanya nyinyi mmefanya *master mind* wa kuwapa watu viwanja wakati wengine wanajua kabisa kwamba eneo hili ameshanunua Nadir wanamuuzia Juma, haipendezi ningeomba Wizara kesi kama hizo wakiletewa basi wale Masheha bora wawaondoshe moja kwa moja. La si hivyo itakuwa Zanzibar migogoro haishi, migogoro inaanzishwa huko huko chini mwanzo ndio inakuja juu Wizara ya Ardhi.(*Makofi*).

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi niende Mkoa wa Kusini Unguja kwanza nipongeze uongozi mzima kusema la kweli Mkoa wa Kusini nao umekuwa unaongoza kwa ukahaba na madanguro, madawa ya kulevya Paje, Bwejuu watu wanakula unga kama hawana akili vizuri. Mimi binafsi nilikwenda kutembea miezi iliyopita nilivaa shoti, maana yake na mimi nikifika kule ninakuwa mzungu, jamaa kufika kule mimi nazungumza kitu uhakika jamaa walinifuata wanauza unga wakafikiria mzungu wakataka kuniuzia unga, nikapatana nao mpaka bei, nikataka waniletee lakini nafikiri walishituliwa wale kwamba bwana huyu mtu fulani. Lakini mwanzo wamenifuata wako *very serious* wakaniambia sijui kete gani dola 250 ananambia na wenzako tunawauzia bei hizo hizo.

Mimi ningemuomba Mkuu wa Mkoa mpya na Mkuu wa Wilaya ambaye nae namuamini kwa kazi ambazo anazifanya wa Kusini, watu wa namna hii sehemu yake ya Kusini haijaharibika kama ilivyoharibika Mkoa wa Mjini/Magharibi na Kaskazini, ajitahidi aweze kuzuia mwanzo kabla mambo hayajaharibika. Haya mambo ya ardhi vile vile sasa hivi kuna watu wapo kwenye utapeli tu na viongozi humu humu baadhi yao wamo anawajua mwenyewe namuomba aendelee kufanya kazi kama anavyofahamu.(*Makofi*).

Mkoa wa Kaskazini Unguja unaongoza kwa madawa ya kulevya na ukahaba tena maarufu dunia nzima, yaani wewe ukitaja Kendwa, Nungwi dunia nzima maarufu. Mimi namuonea huruma sana Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ya kule, wana kazi nzito wanapofanya maamuzi magumu wakati mwengine tuwaachilie wafanye maamuzi magumu bila ya maamuzi magumu hawatoweza kufanya kazi kwa kule Kendwa, kuna watu kule wana pesa, kuna watu wana uenyeji wanafika hata kushindana nao. Imetajwa humu leo mambo ya madisko na nini kule kunauzwa madawa ya kulevya, watu makahaba kila sehemu *International* kutoka Tanga, kutoka Kenya, kutoka *Europe* sijui kutoka wapi wote wako pale.

Ningeomba Wizara iwape nguvu sana na mambo kama haya yasimamishwe mtu anataka aje na mkewe kama ana mchumba wake aje nae, lakini hatutaki kuona makahaba wanafukuzwa Dar es Salaam matokeo yake wanakuja kuhamia huku. Tumeona sasa

hivi na Mhe. Waziri wa Tawala za Mikoa nimwambie omba omba wanaofukuzwa Dar es Salaam sasa hivi wote wako Darajani Zanzibar. Tuangalieni watu wanaondosha wao kule kufisha miji yao tunaletewa sisi na wale machangudoa na wengine wanaokuja Nungwi wanatoka Tanga, wanatoka Dar es Salaam. Mimi ningewaomba Masheha wa kule wanaojifanya kuwapa vikaratasi vile vya kukaa na kuwatambua pengine wanapata *percent* zao na wao washughulikiwe na hili ndio lililokuwepo. Masheha wanakula *percentage* sasa hivi kwenye kila kazi, kwa wanawake wanachukua *percent*, kwenye maduka wanachukua *percent* hii ndio hali halisi iliyokuwepo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niende Mkoa wa Mjini/Magharibi……..

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir umalizie wewe ni mjumbe umeshachangia nakupa muda umalizie.

Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf Alwardy: Mheshimiwa kama ni kumalizia nakwenda Afisi ya Mufti namalizie bora nirukie hiyo Wizara nyengine maana yake naona sijaizungumzia ni Wizara ya Katba na Sheria.

Mhe. Waziri nimuombe aliwahi kututolea ahadi kwamba atahakikisha kwamba Ofisi ya Mufti itakuja kupata *vote* yake iweze kujiendesha. Ofisi ya Mufti inahitjai *vote* iweze kujiendesha, Afisi ya Mufti ina nguvu sana Zanzibar iweze kuwa

kama nchi nyengine ziwe na maamuzi yake isiamuliwe kila kitu, haiwezekane Mufti apangiwe kwa Unguja wakati kila kitu sisi tupo wenyewe kwa wenyewe, tumpe heshima yake na *standard* yake aliyokuwa nayo. Afisi ya Mufti haina hata janareta umesikia wapi wewe. Mimi nimekwenda juzi masaa mangapi hata barua kuandika hawawezi jenereta hata milioni ishirini halifiki, kweli Wizara mnashindwa kununua kwenye Afisi ya Mufti, hatutaki kusema ni dharau lakini itabidi ionekane hivyo. Ningemuomba Mhe. Waziri kwa kazi zake nzuri anazozifanya awafikirie Afisi ya Mufti kupata *vote* yao na ni muhimu sana kupata ili waweze kufanya mambo yao pamoja na jenereta.

Lakini Mheshimiwa mimi nimalizie kuwapongeza wote kwa sababu mimi ni mjumbe wa kamati kama ulivyosema na hili buku mimi nimeshiriki kutaja matatizo na nai-*support* ripoti kwa asilimia mia moja, hayo niliyoyazungumza nitaomba yafanyiwe kazi na mengine tutakuja kupelekeana kwa njia nyengine ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*).

MICHANGO YA MAANDISHI

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum

Mhe. Khadija Omar Kibano: Ukosefu wa maeneo ya kambi za vikosi kukosa hatimiliki.

Ushauri:
Kwa upande wa serikali inaweza kushitakiwa. Mfano, anaweza kutokea mtu yeyote akasema eneo hili ni langu na kumega.

Ukosefu wa huduma za afya makambini:
Katika kambi hizo zilizotajwa kwa Pemba, Tungamaa na Kangani. Hizi kambi hakuna wanafunzi tu kuna na askari wanaishi na familia zao, tujali haki za binadamu pale tatizo likitokea usiku.

Kukosa kulipwa madeni kwa taasisi husika.

Ushauri:
Wizara ya Fedha ifanye juhudi ya madeni kwa taasisi mbali mbali zinazohusiana katika kufanya kazi zao.

Kikosi cha Kuzuwia Magendo kwa upande wa lindo la baharini ni muhimu sana, hii Kambi ya Makuwe wapate boti ya doria kutokana na majukumu yao. Mfano, boti hiyo itasaidia sana hata kwa uvuvi haramu na kupata kuwafichuwa wale waliojificha.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, awali namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya njema na kuniwezesha kuwa ni mchangia wa ripoti hii ilio mbele yetu.

Kwanza mimi ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja ripoti hii ya Kamati pamoja na kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Machano Othman Said kwa uwasilishaji wake, pamoja na wajumbe wake walioandaa ripoti hii kwa pamoja na watendaji mbali mbali.

Mimi nazipongeza taasisi zote zilizomo ndani ya wizara hizi mbili kwa jinsi zinavyotekeleza majukumu yao muhimu ya nchi nzima. Lakini niende zaidi kwa vikosi vyetu vyote vya SMZ kwa kushirikiana na vyombo vyengine vya ulinzi nchini, katika kuweka nchi yetu sawa na salama na wananchi wakaweza kufanya majukumu yao ya kila siku ya kujikimu na kujiletea maendeleo.

Aidha, nivipongeze vikosi vyetu vyote vya SMZ na SMT kwa kuweza kujitahidi katika ulinzi wa zao la karafuu ambalo ni zao kuu la nchi.

Sasa niende kwa Idara ya Chuo cha Amfunzo. Kama ilivyo jina lake ninashauri sana kupeleka huduma hii ya mafunzo mbali mbali yakiwemo ushauri, ujuzi, kuchonga na kadhalika. Katika Chuo cha Mafunzo Pemba ambacho kwa sasa hivi hakuna huduma hizo, huduma ambazo zitawafanya wanapotoka kubadilika na kuanza kufaidia na mafunzo ya chuo kwa muda walio mafunzoni.

Pia wanafunzi pamoja na walioko rumande katika Chuo cha Mafunzo Wete wanaomba kufanyiwa mabadiliko ya kitoweleo cha samaki, nyama angalau baadhi ya siku badala ya harage kila siku.

Vile vile kwa zile siku za sherehe za kitaifa kama Sherehe za Mapinduzi na Iddi (Sikukuu) wajisikie kama tuliyo nje ya chuo.

Pia wanafunzi hao waliniomba niwafikishie kilio chao cha kuwa na Jji Mkaazi Pemba, ili kesi zao zipate kusikilizwa kwa haraka.

Kuhusu Idara ya JKU. Kupeleka mafunzo ya amali katika kambi zilioko Pemba kwa faida yao na taifa pia.

Idara ya Mahakama

Ninaiomba Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ikishirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kuanza kujitayarisha kufanya matengenezo makubwa katika Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini, Pemba. Hali ni mbaya ya jengo lile ambalo ni sehemu ya muhimili mkuu wa nchi ambao unatumiwa kwa wananchi kupata haki zao.

Kuhusu Kikosi cha Polisi /US. SMZ kuwa duarani hata maafisa wakuu kwa nini hii?

Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Mamlaka isimamie vyema suala zima la Manispaa za Mikoa zilizopo katika hali ya uchafu uliokithiri hapa Unguja, katika shehia ningi zinakuwa na hali mbaya ya uchafu na mvua zinakuja kila nyumba/mtaa uchafu umezagaa na ni kukaribisha magonjwa ya kipindupindu. Mamlaka bado iandae mikakati ya kuondoa uchafu na kukiondosha kipindupindu na sio kutibu kipindupindu, kukinga ni bora kuliko kutibu.

Mhe. Spika, ninawashukuru vikosi vyetu vya SMZ kwa mashirikiano mazuri yaliopo katika shughuli mbali mbali za ulinzi wa ndani baina yao na Jeshi la Polisi Tanzania. Lakini ni jambo la kushangaza Askari Polisi wa chini hawawezi kusaluti kwa Afisa wa Kikosi cha SMZ na hata kudiriki kumuelimisha kwamba yeye ni afisa anastahiki heshima kutoka kwa askari polisi. Jibu katika askari polisi amesema, mimi sitakiwi kusaluti kwa Afisa wa Kikosi cha SMZ. Je, Mhe. waziri husika na sheria na utawala bora hili ni sawa? Kama sio sawa mnaliweka vipi?

Jambo katika kuwekeana nidhamu kwa viongozi wetu ambao wanaheshimika kwa vikosi vya SMZ.

Mwisho naunga mkono ripoti hii na ninaunga mkono michango yote iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia kidogo katika ripoti hii muhimu. Naanza kwa kuwapongeza wale waliohusika katika ripoti hii pamoja na watendaji wao. Lakini pia naipongeza sana Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Sheria na waandaji wa ripoti kuanzia kiti na wajumbe wote. Ripoti inaonesha dira na kuleta

mwongozo kwa taasisi zetu, hivi nini tufanye ili kutatua changamoto zilizowakabili kwa faida ya wananchi.

Nachukua nafasi hii kumpongeza kiongozi wa serikali na chama katika Mkoa wa Kaskazini, Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya zote, vyombo vya ulinzi na usalama, viongozi wa Chama cha CCM kuanzia ngazi ya Mkoa hadi shina kwa mashirikiano yao katika kudumisha amani na utulivu katika Mkoa mzima kwa wananchi wote na bila ya ubaguzi wowote.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nigusie kuchangia katika eneo la hali ya vitendo vya udhalilishaji kuwa ni tishio. Tunasikitishwa sana na hali hiyo, lakini pia tunapongeza vyombo vinavyohusika kwa mikakati yao ya kukabiliana na vitendo hivyo.

Tunawapongeza sana wazee na familia ambazo zinapatwa na kadhia hiyo kwa kusimama kidete katika kusaidia kwa kutoa ushahidi na kukataa suluhu za kifamilia majumbani. Na mwamko huu wanao wananchi wote wa Kaskazini Pemba, kwani itokeapo familia kuonyesha dalili ya kupokea suluhu nyumbani, wananchi wako tayari kuandamana na kusindikiza muhusika afikishwe katika vyombo vya sheria ni dhahiri wanaiamini sana serikali yao huu ni mwamko mzuri kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, pili tunaipongeza sana Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Ofisi ya Baraza la Mji na taasisi zinazohusika kwa uchimbaji wa mtaro wa maji ya mvua ambao ulikuwa ni tishio kubwa kwa wananchi wakaazi wa maeneo ya Bubujiko na Vitongoji vyake na juhudi zao hususan katika kipindi cha mvua.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wete tunatoa shukurani kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein hasa alipofanya

ziara ya kuona mtaro huo, na kwa utekelezaji wake na kuondosha kero hii sugu kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sasa ninamuita Mhe. Naibu Waziri Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum karibu sana na baadae atafuatiwa na Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa fursa hii kwa kuweza kuchangia angalau machache katika ripoti hii ya kamati ambayo inahusika na Wizara hizi mbili ambayo wameiwasilisha katika Baraza letu tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba na mimi niungane na wenzangu katika kutoa maoni yangu juu ya ripoti ambayo kamati hii imeweza kuwasilisha kwetu kutokana na umahiri lakini vile vile na ufanisi wa hali ya juu katika kufuatilia na baadae katika kuandika ripiti hii. Mhe. Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba kamati hii imejituma sana na takriban nathubutu kusema kwamba ripoti hii haikuacha kitu katika yale ambayo wameyazungumzia. Mhe. Mwenyekiti, na mimi nitakuwa shuhuda tulikuwa pamoja baadhi ya maeneo lakini waliyoyasema sina shaka nayo wameelezea yale ambayo ni uhalisia.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii ni kubwa mno na sitaki nizungumze moja kwa moja katika kupitia au kuchangia katika maeneo *page* kwa *page* kwa takriban yanayogusa katika Afisi ya Rais Tawala za Mikoa yameanzia katika ukurasa wa 57 mpaka 120. Kwa hivyo wamezungumzia mambo mengi lakini kwa haraka haraka na mimi niungane tu kuungana na wachangiaji wengi ambao wameanza kutangulia kusema kwa kuipongeza Wizara, kwa maana uongozi wa Wizara, lakini vile vile wametumia fursa kubwa katika kuwapongeza Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya pamoja na Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara ya Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na idara Maalum.

Lakini vile vile pongezi zimekuja kwa vikosi vyetu na ni dhahiri kwamba haya ambayo yamepongezwa na ndio ukweli halisi ulivyo wameweza kujituma na ndio maana ikapatikana ripoti hii ambayo leo kila mmoja wetu tumeweza kuisifia. Mimi niseme tu kwamba na mimi naungana na wale ambao wamesema kwamba tunayo Sheria ya Namba 7 ya mwaka 2014 ya Serikali za Mitaa na kuonesha baadhi ya mambo ambayo Waheshimiwa Wajumbe wengine wamesema, ipo haja kwa wajumbe wa kamati kuona kwamba wafanyakazi katika taasisi hizi wanapatiwa mafunzo ili kusudi kuendana sambamba na sheria hii iweze kutambua vyema majukumu yao na katika kuendeleza uwajibikaji uliotukuka. Mhe. Mwenyekiti, na mimi niseme jambo hili ni zuri na ni imani yangu kwamba juhudi zinaendelea kufanyika na takriban kadri hali inavyoruhusu tumekuwa tukishuhudia ni namna gani wafanyakazi wamekuwa wakipatiwa mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niende katika kuangalia Manispaa za Mkoa wa Mjini/Magharibi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe kuonesha namna ambavyo wameweza kuguswa na hali ya upungufu wa magari ya kuzoa takataka, ni jambo ambalo kwa kweli halifichiki lipo na takriban katika Manispaa hizi Wakurugenzi wetu pamoja na watendaji wamekuwa wakijitahidi sana, katika kufanya kazi kubwa kutafuta namna ili kuona kwamba mji wetu unaendelea kuwa katika hali ya usafi licha ya changamoto kwamba hawawezi kusafisha kwa asilimia mia moja, lakini takriban hizo taka zinazozolewa ni juhidi kubwa ambazo wamekuwa wakizifanya. Lakini ni dhahiri kwamba juhudi zinaendelea kufanyika na tunategemea kwamba magari yataweza kupatikana na hali ikaongeza katika ufanisi na tukaepukana nayo katika kukodi magari ambayo tungeweza kupunguza gharama pengine ya kukodi magari.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niseme na mimi niungane pia kwa wale Wajumbe ambao wamesema au wamechangia na kutoa pongezi zao pamoja na ripoti ya kamati imeonesha kufurahishwa sana na namna ya ukusanywaji wa mapato hususan katika Halmashauri na Mabaraza ya miji katika mikoa ya Pemba, lakini vile vile na Unguja Kaskazini pamoja na Kusingi Unguja. Mhe. Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba hali sasa hivi kuna mabadiliko makubwa kubwa zaidi na mimi niseme niungane na wengine kwamba kuona ni namna gani tunaongeza *speed* katika kutoa taaluma kwa wananchi wetu ili kuona kwamba wanafahamu ni namna gani bora ya kuendeleza kutoa kodi ili kusudi Halmashauri hizo pamoja na Baraza yetu yaweze kukabiliana na hali

tuliyokuwa nayo ya suala zima la ugatuzi. Kwa sababu pasinakuwepo na ongezeko la makusanyo tunaweza tukafikia hali tukaja tukaona kwamba huduma zetu haziendi kwa haraka zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ambao wameweza kuonyesha hisia ni namna gani kwamba ugatuzi ambavyo umeanza kuonekana ukileta tija hususan katika sekta ya afya ambayo imepewa pongezi pia na mimi nakubaliana na hilo.

Mheshimiwa vile vile kuna wachangiaji wengine waliweza kuonyesha hisia zao kwa namna ambavyo fedha nyingi zimetumika katika ujenzi wa soko lile la Michakaeni ambalo linaendelezwa na Baraza la Mji la Chake Chake. Kwa kweli ni kwamba Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikubaliane kwamba fedha zilizotumika ni nyingi na bado zinahitajika fedha nyingi zaidi, lakini naomba tukumbuke kwamba katika eneo lile ni kwamba palikuwepo na mlima mkubwa na katika gharama kubwa vile vile palikuwepo na kulipa fidia na gharama nyingi ambazo zilihitajika eneo lile hapo awali halikuwa la serikali. Kwa hivyo ni mimi niseme fedha zilizotumika zipo katika uhalisia kutokana na hali ya jiografia ya eneo lililohusika. Hivyo niwaombe tu Waheshimiwa Wajumbe tuendelee kusaidiana katika kuona kwamba Serikali yetu inaendelea kufanya kazi vizuri lakini vile vile katika kuona pale muda utakapofika basi tusisite katika kutoa fursa ya kuona kwamba tunaongeza ufanisi katika kuitetea ili kuona tunaongezewa fedha katika kipindi cha bajeti pale kitakapofika ili kuona kwamba tunaweza tukakabiliana ile azma ya Serikali

kupunguza mrundikano katika mji wa Chake Chake basi iweze kufikia kwa kuwapeleka na kuweka mazingira mazuri pale ili kusudi wananchi wetu waweze kufaidika na matunda yao.

Lakini vile vile Mhe.Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii na mimi kuungana pia na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na kumpa pole kidogo kwa yale ambayo alisema yamemkuta, lakini naomba tu nikumbushe. Mhe. Mwenyekiti, sheria tunazopitisha ni nyingi katika Baraza letu na inafikia wakati baada ya kupitisha zile sheria nyengine kama kwamba wakati mwengine zinatupitikia. Hivyo niombe tu Waheshimiwa kwa kupitia Baraza hili tukufu tukumbuke kwamba sheria tunapozipitisha baadae tunazishusha kwenye taasisi zetu ziende zikasimamiwe na ziweze kuleta matokeo yanayokusudiwa.

Sasa isingependeza sana kwamba ikafika wakati kwamba eneo Serikali imekataza kwamba lisifanyike au lisitumike kwa matumizi fulani, hatimae sisi wananchi badala ya kuwasaidia pale ambapo wasiweze kukaidi zile amri za Serikali halali na badala yake tusubiri baada ya kufanya makosa ndio baadae tuje tujaribu kuwasaidia. Kwa kweli Serikali haina nia mbaya, ina nia ya kuwasaidia wananchi lakini vile vile tuangalie sheria zetu ambao tukizipitisha….

Hapa umeme ulikatika na baadae kurudi……

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa endelea lakini angalia na muda.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa,Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mheshimiwa Mwenyekiti naomba niendelee kwa kushauri Waheshimiwa kwamba tujitahidi sana tushirikiane katika kuwaelimisha wananchi wetu kuweza kufuata sheria ili kusudi wasikumbane na mikono ya sheria pale watakapozivunja kwa makusudi ama kwa bahati mbaya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba niende moja kwa moja moja nisitumie muda zaidi niseme kwamba ripoti ambayo Waheshimiwa Wajumbe au kamati wameiwasilisha na mimi niseme kama wenzangu ambavyo wametangulia, ushauri huu ambao umetolewa tutahakikisha kwamba tutajitahidi kwa kadri inavyowezekana kuona kwamba tunatekeleza na yale maagizo au na ushauri wa kamati ili kusudi tuone matokeo bora katika nchi yetu yanayoweza kufikia, ukweli tukubaliane kwamba mabadiliko katika taasisi zetu hizi yamekuwa makubwa siku hadi siku. Hivyo tuendelee kuwaomba wananchi lakini vile vile kuwaelimisha wananchi wetu katika kuona kwamba wanalipa kodi lakini sambamba na hilo wawe wastahamilifu pale watakapoguswa na mabadiliko pale ambapo wataona hawakufanyiwa uhalali, lakini vyema tuendelee kushirikiana na kuripoti yale matokeo ambayo hayako vizuri.

Lakini mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba baadhi ya Waheshimiwa Masheha wamepongezwa sana lakini vile vile wapo Masheha ambao wameonekana kidogo kuna shutuma ambazo zimekuwa zikonekana kujihusisha na mambo ya migogoro ya ardhi. Niseme kati ya hili hakuna hata mmoja ambaye yuko juu ya sheria lakini Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wamekuwa wakijitahidi sana katika kukabiliana na hali hiyo. Nataka nikwambie miongoni mwa mapungufu ambayo yakibainika ni kwamba Wakuu wa Mikoa tunashukuru sana kwamba wako haraka sana katika kuchukua hatua. Niwaombe sana Waheshimiwa tuendelee kushirikiana ili kusudi kuona pia na viongizi wetu hawa tunashirikiana nao kusudi ili na wao wafuate sheria. Lakini pale ambapo kwa kweli sheria zitakiukwa basi hatua zitachukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo na mimi niseme naungana na wachangiaji kuunga mikono ripoti hii ya kamati Ahsante sana Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii kuchagia machache juuu ya ripoti ya Kamati na kutoa ufafanuzi mdogo kwa baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wawakilishi. Nachukufua fursa hii kuipongeza kwa dhati kamati hii kutokana na aina ya ripoti ambayo wameandaa, hizi ndizo aina ya ripoti ambazo zitaisaidia sana Serikali kutoa maamuzi. Kwa kweli sasa tumefikia hatua kwamba tunaelewa na atunajielewa,

hizi ni ripoti muhimu sana. Kwa hivyo nawashukuru sana watu wa kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, pili napenda kuchukua fursa hii pia kuzungumzia juu ya suala la wananchi wa Kikungwi juu ya kutaka kuanzishiwa darasa la kidato cha tatu. Wizara ya Elimu katika kutoa ruhusa ya kuanzisha madarasa hayo inatumia vigezo mbali mbali. Kwanza tunajaribu kuangalia uwezo na idadi ya walimu waliopo katika skuli hiyo na kama kweli wanaweza kutosheleza kusomesha katika kiwango hicho cha elimu.

Pili tunaangalia idadi ya wanafunzi je, inakidhi kuanzisha darasa. Tatu tunaangalia nafasi je, ipo nafasi ya kusomesha. Aidha tunaangalia vifaa vya maabara, vitabu na nyenzo nyengine za usomeshaji, lakini pia huwa tunaangalia utayari kwa wananchi katika kushirikiana na skuli na mara nyengine tunaangalia masafa. Wananchi wa Kikungwi walileta maombi yao tukatafakari, tukayafanyia tafiti zote zinazokidhi. Kwanza kupitia ripoti ya Mwalimu Mkuu lakini pia tukaunda Kamati kufatilia, lakini pia tukafanya mazungumzo naye na mimi mwenyewe ndiye niliyeongoza mazungumzo hayo. Baadaye kunakamati ya kitaalamu ya Wizara ya Elimu ikakutana kulitafakari zaidi suala hili. Baada ya kutafakari Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekubali kulianzisha darasa hilo katika Skuli ya Kikungwi baada ya kutii vigezo vyote vinavyohitajika.

Muelekeo wa Wizara ya Elimu ni kuona kwamba kero za wananchi, shida za wananchi na matamanio ya wananchi

tunayafikia, pamoja ya yote, tunazingatia vigezo. Kwa hivyo Skuli ya Kikungwi imekidhi vigezo hivyo na kuanzia Jumatatu wataanza kusoma.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuomba Wawakilishi kwamba nia ya serikali kuanzisha skuli ya serikali kila pahala, lakini pia tuelewe yale mambo ya msingi yanapatikana katika maeneo hayo. Kama yanapatikana basi Wizara itaendelea kufungua skuli mara kwa mara, pale ambapo sifa zimepungua tushirikiane kwa pamoja ili ziweze kupatikana na kuweza kufungua serikali ambayo itakuwa na maana na tija, suala ni maana na tija ya elimu sio idadi ya skuli.

Aidha baada ya kutoa maelezo hayo niseme kwamba kulikuwa kuna suala la mchango juu ya masuala ya madeni ya walimu, malimbikizo ya mishahara na kadhalika. Pia nalo nilieleze kwamba suala hili Wizara ya Elimu inalielewa vizuri sana na hivi karibuni tumetakiwa kwamba tulifanyie uhakiki. Baada ya kufanyia uhakiki madeni hayo yawasilishwe katika Wizara inayohusina na Utumishi wa Umma nayo pia watafanya kazi zao halafu baadae yatapelekwa katika Wizara ya Fedha nayo pia watafanya taratibu zao. Lakini suala hili linashughulikiwa na taasisi zote zinazohusika. Napenda kuwaomba walimu waendelee kuwa na subra na hakuna mwalimu ambaye atanyimwa haki yake.

Mwisho kabisa napenda kuchukua fursa hii kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Wajumbe Wawakilishi wote ambao wametusaidia sana katika kushughulikia masuala ya elimu. Wanaotusaidia kwa kutushauri, wanaotusaidia kwa kushirikiana pamoja katika kutatua changamoto hizi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu zikiwemo madarasa, Wawakilishi wengi wamefanya kazi hiyo ikiwemo vyoo katika skuli, vikiwemo vitabu na hata wakati mwengine zikiwemo kompyuta, kwa kweli tunawapongeza sana. Sasa hivi tunachofanya ni kutaka kuziratibu shughuli hizi za Wawakilishi wanazozifanya katika sekta ya elimu ili baadae kuja

kutoa ripoti rasmi misaada yenu ambayo mmetupa. Wizara inawaomba kwa dhati waendelee kusaidia sekta hii.

Baada ya kusema nimalizie kwa kusema kwamba ripoti hii naikubali ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Naibu Waziri, sasa nampa nafasi Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na yeye aweze kutoa michango yake baadae atafuatia Waziri wa Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba nichukue nafasi hii kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu na pia kuzishukuru Wizara hizi mbili ambazo zote zinazungumzia masuala yanayohusiana na masuala mazima ya Sheria na Utawa Bora katika nchi yetu.

Pia napenda nimshukuru sana Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuendelea kupanga safu nzuri za watendaji ikiwemo Mawaziri na Viongozi mbali mbali wa vikosi vya SMZ. Pia nimpongeze watendaji wote wanaohusika katika juhudi za kufanya maisha kuwa bora katika nchi yetu yenye amani na utulivu.

Nampongeza Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Kamati yake kwa jinsi walivyoweza kuchukua muda wao wa kutosha wakakaa na kupitia mambo mengi na wameweza kutoa ushauri mwingi sana katika masuala yote yanayohusikana na Kamati ya Kudumu ya Sheria ya Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa Fedha 2017/18 kwa kazi nzuri waliyoifanya, kwani kusema changamoto na maoni waliyotoa naamini kabisa yakifanyiwa kazi mafanikio mengi yatatokea.

Mhe. Mwenyekiti, katika Idara zao nane (8) na Taasisi kumi na tatu (13) ambazo zinafanya kazi. Napenda nitoe shukurani kwa ushirikiano mkubwa ambao umekuwa ukitolewa na Wizara hii hasa Wizara yangu ilipokuwa na changamoto kubwa sana juu ya uhafifu wa Sheria zinazokinzana na masuala mazima ya wananchi kwenye masuala ya udhalilisha na mengine ambayo tumekwisha kuyafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, sheria zimetungwa na zimefanywa kwa sababu pamoja na usimamizi wa Mwenyekiti ambaye ni Waziri katika kuhakikisha katika mpango wa harakati wa kuhakikisha masuala haya yanabadilishwa, imefikia pahali ambapo sasa hivi tunaweza kuwa tunashika mpini badala ya kuchezea makali matupu. Mhe. Mwenyekiti, ushauri wa Kamati kuwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kule Pemba ili kesi ziwe zinashughulikiwa na serikali, kunakuwa na matatizo wakati wa kesi za awali. Nadhani jambo hili linafanyiwa kazi na likifanikiwa litakuwa halina tatizo.

Afisi ya Mkaguzi Mkuu kuwa na watendaji wachache washauri wa Kamati kama walivyoshauri, nadhani ipo haja ya kuongeza ili kutoa changamoto zifanyike mapema. Ni suala ambalo linafanyiwa kazi kwa hivi sasa, kwa sababu katika hali hii kama tunavyojua kwamba serikali kila inapoona kuna tatizo moja basi wanatafuta utaratibu wa haraka sana kutafuta kuyatatua masuala hala.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia kwenye suala la Mahakama kitendo cha watendaji kushiriki katika vikao vya Madola wanapopewa nafasi ya kwenda kusema Nchi za nje, nadhani ni jambo zuri sana la kuipongeza serikali yetu, kwa sababu nao wanapata nafasi na fursa ya kujifunza mambo mengine kutoka nchi za nje na kuweza kuwa na mtizamo mzuri zaidi katika kufanya masuala haya. Pia kupitisha sheria nyingi ambazo adhabu zake zinaonekana kabisa kwamba sio za kwetu bali ni za kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika adhabu mpya naamini mengine yatarekebishwa na wananchi wakorofi wataacha. Kwenye ukurasa wa 34 na 35 kuna kesi kama saba hivi ambazo zinazungumza habari za mtu wa ng'ombe, zinazungumza wanawake, zinazungumza habari za watu, kuna kesi saba ambazo zinaonyesha zingeweza kuchukua muda mrefu, lakini sasa hivi vimeorosheshwa na zimepelekwa kwenye vyombo vya sheria kufanyiwa kazi, kitu ambacho kinatia moyo. Hali ya kesi za madawa ya kulevya yanayowaathiri vijana na wanawake, kwani hili ni suala la kijamii akihusika mmoja tu katika jamii inakuwa ni mzigo wa watu wote katika jamii nzima.

Hapa naomba nitoe wito kwa akinamama kwamba nawaomba sana akinamama hata mkiwa mnamahitaji, mna tama ya kiasi gani, msikubali kutumiwa katika masuala ya madawa ya kilevya. Kwa mfano ukiangalia ile kesi iliyotokezea Pemba iliyomuhisisha mama aliyekuwa ananyonyesha, utaona akishafika katika suala la mkondo wa sheria akitiwa ndani inakuwa ni familia nzima inaumia na inakuwa kwenye mashaka mengi. Nawaomba pia na akinababa muwe na huruma msiwatumie hawa watu kuwawekea kwenye vyombo vyao hata wakafika kwenye mahali pa hatari.

Pia nishukuru Wakuu wa Mikoa na Wilaya na Afisi zao wanatutia moyo kwani wanatoa ushirikiano mkubwa katika kupiga vita kadhia mbali mbali zinazotokezea katika maeneo mbali mbali zinazotokezea katika maeneo mbali mbali. Aidha niwashukuru vikosi vyote vya SMZ kwani wanapohitajika wanatoa ushirikiano wao kwa haraka na nidhamu kubwa, wanatunza amani na kuzuia magendo ambayo hayo yanatusaidia sisi kuendelea kuwa na vipato vizuri katika nchi yetu.

Ukiangalia ukurasa wa 70 tumeshuhudia mafanikio kama vile imepunguza migogoro mbali mbali, imepunguza wanyama waliokuwa wakizurura ovyo ambao wanatishia mazingira hatari, magari yamekuwa ni mengi. Laiti kama tungeachia ile hali

kuendelea isingependa na ingeleta vitu visingekuwa na amani. Kutokana na amani tumeshuhudia wananchi wanavyohudhuria katika shughuli mbali mbali za sherehe tunapokuwa na shughuli za kuadhimisha maazimio makubwa katika nchi yetu. Inatia moyo kwamba jinsi gani yanayojitokeza na yanatunza heshima. Kwa sababu tunapokuwa katika shughuli kama zile watu wengi wanatizama Wazanzibari wanafanya nini. Nipende kupongeza jinsi wanavyofanya juhudi zao, mazoezi wanayokuwa wanafanya na hatimaye tunamaliza shughuli zetu katika hali ya amani na utulivu.

Ukiangalia katika ukurasa wa 117 juhudi kubwa inayofanywa na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein anapovijali vikosi vya SMZ na kuona umuhimu wa kujenga makaazi ya kuishi. Kwa sababu hawa watu wasipokuwa na makaazi ya kuishi itakuwa ni changamoto kwao, lakini anaona kabisa kwamba ni vyema watu wajengewe makaazi yao waweze kukaa kwa usalama zaidi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, pia suala zima la kuanzisha viwanda, tukiangalia kama tulivyosema viwanda vilivyoanzishwa na Vikosi vya SMZ zinatia moyo, kama wangeweza kuwa na viatu ambavyo vingeweza kununuliwa nje na ngozi inakuwa ni gharama na mambo mengine. Lakini viwanda hivi ndivyo vitakavyosukumia sisi kwanza kuanza kujifunza vijana wetu watakapokuwa tayari viwanda vimepanuka watakuwa tayari wameshaanza kupata mafunzo kwenye vikosi vyetu vya SMZ. Kwa hivyo itakuwa ni elimu darasa litakaloweza kutumika na serikali yetu kwa kuanza na hawa tuliokuwa nao.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kuna suala zima la ugatuzi, tunashukuru kwamba wenzetu Mawaziri ambao wanashughulikia suala la ugatuzi wameshaanza kutoa elimu ya kutosha kuhakikisha kwamba suala hili litakapokuwa limegatuliwa basi kusiwe na matatizo watu waendelee kuelewa, lakini pia na elimu itolewe.

Naamini kabisa tutashirikiana katika kuhakikisha kwamba yatakapokwenda huko yawe ni katika mazingira mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho napenda kusema kuwa napenda kuunga mkono ripoti hii moja kwa moja na ushauri wote uliotolewa na Wajumbe wa Kamati katika utekelezaji huu kwa asilimia mia moja. Ahsante kwa kunisikiliza.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sasa namwita Mhe. Waziri, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ na baadae Waziri wa Katiba na Sheria akifuatia.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, jioni hii ya leo na mimi kupata nafasi ya kuchangi ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum za SMZ.

Pili nikupongeze wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii. Tatu nichukue nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati hii ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum za SMZ pamoja na Wajumbe wake wote wa Kamati kwa mashirikiano mazuri sana ambayo walitupa wakati wakifanya kazi yakupitia utekelezaji wa majukumu ya Afisi yetu, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum.

Kwanza nataka nikubali kuipokea ripoti hii ambayo imewasilishwa na Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 106 cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, tumeipokea sisi kama Ofisi ya Rais na kama ilivyokawaida kwa mujibu wa kifungu cha 108 sisi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum, tutawasilisha rasmi utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati ifikapo mwezi wa Septemba au Oktoba mwaka huu

tukiwa tumeyazingatia au tutayazingatia yote yale ambayo tumeshauriwa na Kamati hii.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile nataka nichukue nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza wale wajumbe ambao wameelekeza michango yao kwenye Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum, na wengi wao wametupongeza *style* yao ya leo Wajumbe wengi kila mmoja alikuwa akipongeza Mkoa wake. Lakini kwa sababu mimi ndiye msimamizi wa Mikao hiyo yote, naomba nizipokee shukurani hizo na baadhi ya Wakuu wa Mikoa pale wapo na Wakuu wa Wilaya na wao watakuwa wamezipokea pongezi hizo.

Nataka nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa miongozo na maelekezo yake ambaye amekuwa akitupa siku hadi siku na yale yote mafanikio ambayo yamepatikana ambayo Wajumbe leo wameweza kuyazungumza, sababu yenyewe ni kwa sababu ya Dkt. Ali Mohamed Shein akiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo unazipokea pongezi hizo, tunazipokea pia pongezi walizopewa wapingaji wetu wa Idara maalum.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nimeshasema majibu yote tutayatoa katika kipindi hicho, leo kwa ruhusa yako nataka niseme moja tu. Baadhi ya Wajumbe wameonyesha wasi wasi kuhusu suala zima la ugatuzi. Mimi nataka niendelee kuwambia kwamba wasiwe na wasi wasi juu ya suala hilo. Katika kipindi kifupi tokea Julai mosi, tokea umeanza ugatuzi katika sekta tatu kuna mafanikio makubwa ambayo yamepatikana na sisi tutakapokuja mwezi wa Septemba na mwezi wa Oktoba tutayabainisha hayo mafanikio ambayo yamepatikana.

Mhe. Mwenyekiti, siku zote unapotaka kufanya jambo kwanza unatakiwa uwe na uhakika wa lile jambo unalolifanya. Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum tuna uhakika na tunachokifanya na kama tunauhakika tunakiamini tunachokifanya, na kwa sababu tunakiamini tunachokifanya, niwaondoshee hofu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wategemee mafanikio makubwa katika eneo hili la ugatuzi, wako waliotushauri tuendelee kutoa elimu, tunafanya hivyo na tutaendelea kutoa taaluma hii na wao wenyewe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu ni wahusika wengine katika maeneo yao. Ni imani yangu tutakapokuja kwenye Mkutano wa Bajeti watakuja kuunga mkono kama leo vile baadhi ya Wajumbe wengi ambao wametuombea shufaa kwa baadhi ya taasisi zite kupata unafuu zaidi wa kupata fedha kwa ajili ya kufanikisha shughuli zetu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Mwenyekiti, na ripoti hii ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa asilimia mia moja, ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Subuhana Wataala Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sasa hivi kuweza kufanya shughuli hii ambayo tumeweza kuifanya sasa hivi kwa usalama kabisa na Inshallah Mungu atujaalie tumalize Kikao chetu hichi kwa salama.

Mhe. Mwenyekiti, la pili naomba nichukue nafasi hii maalum kwa dhati kabisa nimshukuru sana Rais wetu wa Zanzibar Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa miongozo na ushauri, na maelekezo mbali mbali ambayo anatupa na haya mafanikio ambayo Waheshimiwa wameyazungumza kama walivyozungumza Waziri mwenzangu wa Tawala za Mikoa kutokana na miongozo hiyo anayotupa na tunamuahisi sisi tutaendelea Inshallah kuhakikisha kwamba tunatekeleza majukumu yetu na wajubu wetu kama tulivyotakiwa na maelekezo tunayopewa.(*Makofi*).

Pili nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya na mashirikiano mazuri waliyotuonyesha na sisi tunawaahidi tutaendelea kutoa mashirikiano yetu hadi hapa ambapo Inshalla Kamati hii itakapokuwa inamaliza muda wake. Ni imani yangu kwamba wataendelea na kamati hii kwa sababu ni moja katika kamati ambayo inatoa mafunzo mengi sana, safari hii wamepata taaluma sana juu ya mambo ya kisheria. Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na wewe pamoja na viongozi wote ambao wanakalia kiti hicho kwa mashirikiano yenu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nizungumzie mambo mawili tu au matatu. Moja nataka niwatoe wasi wasi. Hivi sasa tupo katika hatua za mwisho za kumaliza utaratibu wa kuunda Bodi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Mahesabu. Kwa hivyo tuondoshe mashaka mambo yatakaa sawa tukijaaliwa hayana muda mrefu.

La pili Waheshimiwa wengi waliuliza suala la Afisi ya Mufti, usafiri na mambo mengine. Kwanza kupatiwa *vote* yao sasa hivi taratibu zinakwenda Wizara ya Fedha ili kuhakikisha kwamba jambo hili linamalizika, ingawa ni jambo la siku nyingi ni kweli na tunaahidi kwamba kutokana mashirikiano mazuri tuliyokuwa nayo na wenzetu wa Wizara ya Fedha litamalizika haraka iwezekanavyo. Moja ambalo linatendeka sasa hivi kwa mujibu wa bajeti ya Afisi ya Mufti wanapata asilimia mia moja yote bila ya matatizo yoyote. Tunawapa hivyo kutokana na umuhimu wa Afisi yenu wenyewe. (*Makofi*).

Jengine ninalotaka nilizungumze mheshimiwa mmoja alizungumzia fomu za maadili kwamba hazijarejeshwa nilishangaa kidogo kwa sababu fomu hizi ni siri sasa yeye mheshimiwa kama alikusudiwa ile taarifa iliyoandikwa humu haikuandikwa kama haikurejeshwa isipokuwa zimechelewa kurejeshwa, sasa huu ni utaratibu umeripotiwa humu umechelewa

sio kama hazijarejeshwa kwa sababu huwezi kujua sasa hivi kamati ile au tume ile ina mambo ya siri kabisa wao wenyewe kwa utaratibu kwa ambao wanaujua wenyewe namna wanavyopeleka. Sasa si vyema baadhi ya masuala tukayazungumza hapa kwanza hayakuwa sahihi sio kwamba hazikurejeshwa isipokuwa wamechelewa na ndio kilichoripotiwa kwenye fomu hii.

Baada ya hayo mheshimiwa mimi naipokea ripoti hii rasmi na Insha'Allah tukijaliwa naahidi mwezi wa Septemba kama kanuni ya 108 inavyoelekeza watapata majawabu mazuri sana na mengine hatutosubiri Septemba tutayatekeleza tutamaliza kila kitu kabla Septemba tutaripoti tu yale ambayo tumeyafanya, ahsante mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri nikushukuru sana sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ili na yeye aweze kuja kumalizia, mheshimiwa karibu sana.

Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kutupa jioni njema hii ingawa mimi na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) sio nzuri sana, lakini kwa ujumla tumekwenda vizuri na nawashukuru waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi waliochangia na wale ambao walisikiliza.

Mheshimiwa kitabu chetu cha ripoti ya kamati yetu kilikuwa na *page* kama mia moja na ishirini na hizi *page* mia moja na ishirini ni kutokana na kubana sana na taratibu za baraza, lakini kwa wizara zetu zilivyo hivi mbili ningeliweze kwenda mpaka *page* mia tatu mpaka mia nne.

Kwa leo hapa jumla ya waheshimiwa wajumbe arubaini wamechangia wajumbe ishirini na saba wamechangia kwa

kuzungumza na wajumbe kumi na tatu kwa maandishi sasa tutaona jinsi gani hizi wizara zinawagusa wananchi kwasababu ni wizara za watu zinashughulika na mambo ya watu na zinafanya kazi mtambuka na wizara nyengine kwa hivyo, mchango wa hapa inawezekana pia ukagusa ripoti za kamati zengine na kwa wajumbe arubaini nafikiri ukitaka kujibu mmoja mmoja unaweza kufika hata kesho itakuwa kuliko bajeti.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba tu kwanza niwatambue waliochangia halafu baadaye kwa umoja wao nieleze yale ya msingi kwa sababu kwa ujumla kazi kubwa iliyofanywa na kamati kuangalia, kubaini na baadaye kuziarifu taarifa hizi barazani na wizara sasa watapata muda wa kuja kujibu hoja, kueleza juu ya ushauri wetu na changamoto ambazo zinatukabili wizara hii.

Kwa hivyo, nafikiri wajumbe mnajua taratibu zetu za baraza kwamba ikifika mwezi wa tisa watakuja kuwasilisha wizara, lakini tuzishukuru wizara kabla ya kuwataja wajumbe kwamba changamoto za mwaka jana zimeanza kutekelezwa tulikuwa na tatizo kubwa la askari kutokuwa na mahanga tayari yameanza kujengwa, mradi wa serikali tunaishukuru wizara hii, tunaishukuru Wizara ya Fedha na waziri wao na wengine ambao wameshughulika na kwa mfano mambo mengine ambayo wajumbe wamesema hamkwenda kwa ndani sana lakini niwahakikishe tumeaangalia kwa undani sana lakini hatukuweza kuyaandika yote kwa undani kwa sababu pia taratibu za baraza hazikubali.

Sasa waheshimiwa waliochangiwa leo kwa kuchangia barazani ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Ali Suleiman Ali
2. Mhe. Ali Khamis Bakari (Doholo)
3. Mhe. Ali Salum Haji
4. Mhe. Bahati Khamis Kombo

5. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
6. Mhe. Salha Mohamed Mwinyijuma
7. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na yeye zaidi alizungumzia barabara yake iwekwe lami nasikia Mhe. Waziri kamsikia vizuri.
8. Mhe. Suleiman Makame Ali
9. Mhe. Asha Abdlla Mussa
10. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
11. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
12. Mhe. Suleiman Sarahan Said
13. Mhe. Mussa Foum Mussa
14. Mhe. Hidaya Ali Makame
15. Mhe. Saada Ramadhan Mwenda *(Makofi)*
16. Mhe. Tatu Mohamed Ussi
17. Mhe. Simai Mohammed Said
18. Mhe. Shaibu Said Ali
19. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)
20. Mhe. Mohammedraza Hassanaali
21. Mhe. Miraji Khamis Mussa (kwanza)
22. Mhe. Narid Abdul-latif Yussuf

Waheshimiwa Naibu waziri

23. Mhe. Shamata Shaame Khamis
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri
25. Mhe. Maudline Cyrus Castico
26. Mhe. Haji Omar Kheir
27. Mhe. Haroun Ali Suleiman

Hawa ndio wamechangia kwa maneno lakini kwa maandishi waheshimiwa kumi na tatu ambao wamechangia ni:

1. Mhe. Choum Kombo Khamis
2. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha
3. Mhe. Khamis Juma Mwalim
4. Mhe. Ussi Yahya Haji

5. Mhe. Salama Aboud Talib
6. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
7. Mhe. Shehe Hamad Mattar
8. Mhe. Khadija Omar Kibano
9. Mhe. Harusi Said Suleiman
10. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
11. Mhe. Juma Ali Khatib
12. Mhe. Said Soud Said
13. Mhe. Salma Mussa Bilali

Sasa waheshimiwa mambo makubwa yaliyozungumzwa hapa ambayo watajibu waheshimiwa mawaziri watakapokuja kwanza waheshimiwa wengi walizungumzia matatizo ya uhifadhi wa nyaraka nafikiri yataleta majibu na wanajitahidi kufanya kazi zao. La pili walizungumzia pongezi kwa Wakuu wa Mkoa, Wilaya na Wakurugenzi waheshimiwa wengi nafikiri tumeridhika na kazi ambao wanazifanya Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi na maana yake nini pamoja na matatizo yaliyozungumzwa maji, ubovu wa barabara lakini changamoto zinashughulikiwa ndio maana yake watu wanawasifu Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi.

Jengine ukosefu wa maji na salama limetawala sote tunalitambua tatizo hili nafikiri wizara zinazohusika kwa kupitia wizara hii watalifanyia kazi, ubovu wa barabara zaidi za *feeder road* halmashauri sasa ni kazi yao na lengine uwekaji wa watu mahabusu kwa muda mrefu nalo hili limezungumzwa kwamba ni tatizo Mhe. Waziri na Katiba nafikiri atakuja kutuletea majibu kipindi kitakachofika.

Lakini pia serikali isaidie vikosi kupatiwza dawa vikosi vyetu vya SMZ vinafanya kazi kubwa katika huduma za afya Mhe. Waziri wa Afya bahati nzuri upo, wajumbe wengi wamezungumzia umuhimu wa Wizara ya Afya kuangalia kutoa mgao kwa vikosi vya SMZ kwasababu vinahudmia wananchi wengi. Kuna kipindi

ilikuwa sababu kubwa kwamba wafadhili DANIDA hawataki kama vikosi wapewe lakini tunalotambua sasa kwamba kwa kupitia Mhe. Rais wetu Serikali ya SMZ inatoa fedha nyingi kwa ununuaji wa madawa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, mufikirie kuvisaidia vikosi vya SMZ kupata dawa kwa sababu naamini kwamba asilimia arubaini au hamsini ya wagonjwa wote wanahudumiwa na vikosi zaidi kwa Mkoa wa Mjini Magharibi.

Jengine Wizara ya Kilimo nayo isaidie shughuli za kilimo kwa JKU hili nalo lilizungumzwa na halafu pia walizungumzia umuhimu wa kuhamasisha, kuimarisha Manispaa, Mabaraza maji na Halmashauri ili wafanye kazi zao lakini pia umuhimu wa ugatuzi uendelee na pia barabara ziendelee kuweka katika hali nzuri.

Jambo jengine lilizozungumzwa kwa sana hapa ni hati miliki kwa vikosi vyetu zaidi hili tatizo Mhe. Waziri wa Ardhi kwa kushirikiana na Waziri wa Tawala tunaomba mulipatie ufumbuzi, tatizo la hati miliki bado ingawa tunashukuru wizara tawala kwamba kulikuwa na tatizo kubwa katika kambi ya KMKM Makombeni ile kambi ilikuwa ya eneo la mtu binafsi lakini kwa taarifa tulizozipata tayari suala lile limewekwa sawa na sasa hivi ni eneo la KMKM rasmi kwa hivyo, tunawapongeza sana kwa hatua ambayo wemefikia.

Suala lengine tatizo ambalo limezungumzwa hapa mahitaji ya masoko waheshimiwa wengi wamesema kwamba kwenye maeneo yao kuna masoko yamejengwa mengine yameshamalizika lakini hayajazinduliwa rasmi mfano Mhe. Mgaza amezungumzia soko lake la Kakangani na maeneo mwengine watu wengi wamezunguzia masoko kwa hivyo, hili nalo ni la msingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo la madawa ya kulevya nalo limezungumzwa kwamba ni tatizo pamoja na juhudi za serikali kupambana nayo nafikiri mawaziri wataweka mikakati, lakini pia udhalilishaji wa jinsi na ubakaji ni tatizo nalo lilizunguzwa zaidi kwa mikoa miwili lakini hili ni la nchi nzima sio Kaskazini Pemba na Kaskazini Unguja tu hili ni tatizo la nchi zima pengine hiyo mikoa miwili ndio inayo chocheo zaidi.

Chengine mheshimiwa mmoja alizungumzia kwamba ukijenga msikiti ukisha jenga sio lazima uwe wako ukijenga halafu uwachie wenyewe wenye mitaa waendeshe msikiti wao na lengine Mhe. Raza kwamba yuko tayari na nafikiri waziri atakuwa yuko tayari na mimi mwenyekiti wa kamati niko tayari tufanye hayo mazingira ya kusaidia kama hao wafadhili wako ili Ofisi ya Mufti ipate hizo gari tano alizosema Mhe. Raza, nafikiri sio jambo baya kama itakuwa hayana masharti mengine kama masharti rahisi siyo na masharti mengine basi bila ya shaka tutakuwa vizuri.

Kuhusu wafanyakazi ambao hawatekelezi wajibu wao waheshimiwa wamezungumza kwamba hatua za kinidhamu zichukuliwe na nafikiri hili sio jambo baya na linaweza likafanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumalizia iliungumziwa pia tatizo la baadhi ya viongozi wa serikali kuwakimbia *CAG* hili lipo tumezungumzwa na uhalisia wenyewe ni kwamba siku ya kuingia wanakutana lakini anapokuwa anasema sasa nataka kutoka tuonane Katibu Mkuu au Maafisa wengine hawapatikani. Kwa hivyo, wakiandika ripoti baada ya ripoti ndio wanatokezea wanasema hatukushirikishwa kwa hivyo tunaomba tu Viongozi wa Serikali wawe karibu na *CAG* ili kazi ziende vizuri. *(Makofi)*

Imezungumziwa pia malipo ya *safety fee* kupata *commission* fulani kwa zimamoto kamati imepigia kelele sana na ninaomba

serikali waangalie kama zinazofanya wenzetu wa Tanzania Bara kwa zimamoto basi na Zanzibar nao wapate sehemu ya *safety fee*.

Lengine kujengwa kwa *parking* ya magari pale airport sasa hivi magari yapo ya zimamoto lakini yanaharibika kwa jua kwa hiyo, tunaomba Uongozi wa *Airport*, Wizara ya Fedha, Wizara ya Tawala na Wizara ya Ujenzi wakae waliweke sawa jambo hili ili *parking* ijengwe.

Suala lengine ni kuhusu wafanyakazi ambao hawapendi kazi wanadharau viongozi wa kazi waheshimiwa walitoa ushauri kwamba wafanyakazi kama hao wachukuliwe hata ya kufuzwa kazi. Lakini pia walizungumzia kuhusu masheha ambao wanafanya madili ya kuuza viwanja nafikiri hili sio jambo jipya nafikiri Mhe. Rais alishawafanyia semina masheha na madiwani kwamba kuuza viwanja sio kazi yao kwa hivyo nafikiri ni kukumbushwa tu kwamba hiyo sio kazi yao.

Suala la Kendwa na Paje kwa madawa ya kulevya nalo Mhe. Mawaziri mmelisikia wajumbe wamelizungumza, mafunzo kwa madiwani na wafanyakazi wa ugatuzi ni muhimu lakini pia Mhe. Naibu Waziri wa Elimu alimtoa wasiwasi Mhe. Simai kwamba tayari skuli ya msingi kidatu cha tatu katika Kikungwi tayari kwa hivyo hakuna shida na kutolewa fomu za maadili Mhe. Waziri wa Katiba kalijibu vizuri.

Waheshimiwa baada ya hayo mimi niwashukuru sana nawashukuru na tunashukuru kwamba ripoti yetu ya mwaka jana ilifanyiwa kazi vizuri na matarajio yetu kwamba ripoti ya mwaka huu nayo mawaziri wataifanyia kazi vizuri.

Basi nimalizie kwa kuwashukuru wajumbe na niwatakie kheri na Mwenyezi Mungu atubarikiri sote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ushatoa hoja maana sijakusikia, hoja mheshimiwa.

Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mwenyekiti naomba kutoa hoja sasa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante waheshimiwa hoja imetolewa na mwenyekiti na imeungwa mkono. Sasa niwahoji wale ambao wanakubaliana na hoja ya Mhe. Mwenyekiti, wanaokataa, wanaopinga wameshindwa.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuiwa na kuafikiwa)

Ahsante niwashukuru waheshimiwa wajumbe wote kwa kazi kubwa iliyokuwepo mbele yetu kuanzia tokea asubuhi hadi muda huu tukaichangia ripoti hii kwa upana sana na wajumbe takribani wa nusu ya Baraza wote wamechangia na wale waliokuwa hawakuchangia pia walisikiliza kwa umakini na kwa sababu hiyo kwamba imewagusa wananchi walio wengi wa nchi nzima na ndio ikawapata wachangiaji namna hiyo.

Niwashukuru sana na tuendelee kuwa na uzalendo kama huu ni imani yangu mawaziri wote wameahidi hapa kwamba ifikapo mwezi wa Septemba watatuletea majibu yalio muwafaka kutoka na kamati pia na kutokana na wajumbe waliochangia.

Baada ya hayo kwasababu shughuli za leo zimemaliza niseme nakhahirisha Baraza hili hadi kesho saa 3:00 asubuhi panapo majaaliwa.

(Saa 1:35 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 16/02/2018 saa 3:00 asubuhi)